USICHOKIJUA KUHUSU

# MOYO MGUMU



DEOGRATIUS SUKAMBI

**Mawasiliano na Mwandishi**

Simu: 0746104034

Email: dsukambi901@gmail.com

Facebook: @Deogratius Sukambi

Instagram: @Sukambideo

**Toleo la 1: 2022**

**ISBN: 978-9987-9860-5-7**

Haki zote zimehifadhiwa. Ni kosa kisheria kunakiri kitabu hiki bila idhini ya mwandishi

**Kimehaririwa na;**

Prisca Charles

0754393255

**Kimechapwa na;**

Denats Printing

0746104034

Dar es Salaam-Tanzania

# YALIYOMO

UTANGULIZI ........ 4

SURA YA 1 ........ 7

DHANA YA TALAKA ........ 7

SURA YA 2 ........ 13

CHANZO CHA MOYO MGUMU ........ 13

SURA YA 3 ........ 30

MOYO MGUMU NA AFYA YA AKILI ........ 30

SURA YA 4 ........ 34

MADHARA YA MOYO MGUMU ........ 34

SURA YA 5 ........ 39

DALILI ZA MOYO MGUMU ........ 39

SURA YA 6 ........ 63

SURA YA 7 ........ 71

VIASHIRIA KWENYE JAMII ........ 71

SURA YA 8 ........ 83

MFUMO WA MAISHA ........ 83

SURA YA 09 ........ 101

UNAISHI KWA MFUMO GANI ........ 101

SURA YA 10 ........ 112

MAISHA YA NDEGE NA MAUA ........ 112

SURA YA 11 ........ 116

JUKUMU LA MWANADAMU ........ 116

SURA YA 12 ........ 125

TABIA ZINAZOATHIRIWA ........ 125

# UTANGULIZI

Ulimwengu umekuwa na maswali mengi ya kujiuliza kuhusu mwenendo mzima wa tabia za watu. Maswali hayo yasiyokuwa na majibu yanazidi kuongezeka kila siku. Kwa sehemu tulianza na suala la mmong'onyoko wa maadili kabla hatujapata suluhu tumejikuta tunapambana na matatizo makubwa zaidi. Mipasuko ya familia, migogoro ya kimahusiano, talaka, unyanyasaji na ukatili wa kijinsia na kingono, mbaya zaidi tatizo la afya ya akili. Tatizo la afya ya akili limeonekana kuwa ndio kiini cha matatizo mengine mengi na isitoshe linazidi kushika kasi na kuongezeka ukubwa.

Bado ni vigumu kuelewa ni wapi jamii inakoelekea, pamoja na jitihada na harakati nyingi zinazofanywa na taasisi za kijamii, kiserikali na kidini; hazileti matumaini kama tupo karibu kupata suluhu ya matatizo haya. Swali gumu zaidi ni; Je! dunia hii itakuwa na hali gani miaka ishirini ijayo? Takwimu za matukio ya unyanyasaji na ukatili zitakuwaje? Takwimu za ndoa kuvunjika zitakuwaje? Takwimu za watoto wanaolelewa na mzazi mmoja zitakuwaje? vipi kuhusu maadili ya jamii? Hali ya tatizo la afya ya akili itakuwaje. Inawezekana tusiwe na picha kamili ya jinsi itakavyokuwa lakini uhakika uliopo ni kuwa hali itakuwa mbaya zaidi kuliko ilivyo sasa. Hata hivyo majibu yapo, ikiwa jamii itaamua kutafuta majibu, yanapatikana.

Habari njema ni kwamba mkononi mwako umeshika kitabu ambacho kitakupa majibu ya maswali mengi ambayo umekuwa ukijiuliza. Pia ni wazi kuwa hatuwezi kuyapata majibu ya kina nje ya Mungu aliyeumba mbingu na nchi. Kwa nini? Ni kwa sababu Yeye ndiye anayejua jinsi dunia ilivyopaswa kuwa, hivyo anaweza kutupa muongozo mzuri wa jinsi gani tunaweza kurudi katika uhalisia wa maisha yetu.

Hivi ndivyo tulipaswa kuishi? Kwa kuchukiana, kunyanyasana, Kukoseana adabu, kudharauliana, kutoheshimiana, kuumizana, kutengana, kuoneana wivu. La hasha kwa namna yoyote ile tunaweza kukubaliana kuwa sivyo ilivyopaswa kuwa tangu mwanzo.

"Tangu mwanzo" haikuwa hivi. Kauli hii inatupa sababu nyingi kuanza kutafuta njia yetu kurudi mwanzo. Kurudi mwanzo wa kila kitu na kuona jinsi mambo yalivyopaswa kuwa. Tukifanikiwa kuelewa mwanzo ilikuwaje na sisi tunaishije basi itaturahisisishia safari yetu ya kuleta suluhu.

Itoshe kusema kuwa tatizo sio yule ambaye tunamuona analeta madhara kwa wengine bali kile kilichotokea katikati ya safari ya maisha yake ambacho kimepelekea mtu huyo kuwa jinsi alivyo. Tunapozungumzia tatizo la Afya ya akili ni wazi kuwa hakuna mwanadamu ambaye kwa asili alizaliwa na tatizo la afya ya akili, hakuna aliyezaliwa mkatili na mnyanyasaji, hakuna mwanaume aliyezaliwa na tabia za kuzalisha wanawake na kuwaacha, hakuna ndoa iliyofungwa, watu wakikusudia kuacha baada ya muda Fulani. Swali, je ni nini kimetokea katika

safari, ambacho kimepelekea tumekuwa na matokeo ambayo hatukuyatarajia.

Kwa bahati mbaya tupo katika nyakati ambazo kumekuwa na harakati nyingi za kupambana na ukatili, unyanyasaji, talaka, maadili mabaya, tatizo la afya ya akili; lakini hizi harakati hazitilii maanani chanzo cha tatizo. Wakati harakati zinaendelea na kuanza kujiuliza nini hasa kilitokea, tukajikuta hapa tulipo. Yamkini tunaweza kuwa na harakati nyingi za kupingana na matokeo ya tatizo huku tunaendelea kuzalisha tatizo na mwishoye tukajikuta tunalazimika kuongeza nguvu kubwa kwenye kupingana na matatizo haya kila kukicha badala ya kuzuia yasitokee.

Moyo Mgumu ni dhana ambayo inakusudiwa kutoa majibu ni nini hasa kiini cha matatizo haya katika jamii na suluhuhisho lake kwa kina. Kuanzia talaka, migogoro ya kimahusiano, unyanyasaji na ukatili wa kingono na kijinsia, tatizo la afya ya akili. Kwa kusoma kitabu hiki unajihakikishia kuwa utakuwa salama dhidi ya hizi changamoto zote ikiwa tu utatilia maanani kila kilichoandikwa na kukifanyia kazi.

Kitabu hiki ni maalumu kwa ajili ya watu wote wanaotamani kuifanya dunia kuwa mahali pazuri pakuishi.

Asante sana!

SURA YA 1

# DHANA YA TALAKA

---

Talaka. Kwa wengi neno hili ni laana, uharibifu na pepo mchafu. Mjadala wa talaka ni miongoni mwa mijadala ambayo jamii imekuwa ikiikwepa sana mpaka nyakati za hivi karibuni baada ya kuonekana kuwa sio rahisi kuendelea kukwepa. Pengine ni baada ya kufika hatua ya kulazimika kuchagua kati ya kulinda ndoa ama uhai wa mtu, yawezekana ni kwa sababu hatuna namna nyingine isipokuwa kuanza kulizungumza kwa uwazi. Wakati mazingira yanatulazimisha kulizungumza, swali la msingi ni;

"Je, jamii ilikuwa imejiandaa kuwa na mjadala wa wazi kuhusu talaka?"

Ikiwa tukiamua kulijadili, tunayo dira ya namna nzuri ya kujadili kuhusu hili? Nani anaweza kutupa muongozo mzuri zaidi ili tusiruhusu mihemuko na hisia binafsi zikafunika ukweli kuhusu suala hili. Kwa watu wengi, talaka ni marufuku, kwa wengine uhalisia unawanyima ujasiri wa kusema ni marufuku, yawezekana hata kwa hawa ambao wanaona hakuna haja ya marufuku wengi wao wanabaki na hatia mioyoni mwao kwa kuwa sio jambo ambalo ni lakulionea fahari.

Habari njema ni kuwa mjadala kuhusu talaka hautakuwa mpya, hata katika biblia kulikuwa na mjadala mkubwa kuhusu uhalali wa talaka na hapa chini tunakutana mazungumzo baina ya "Yesu" na "Mafarisayo"

***MATHAYO 19: 6-8*** *"Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe. Wakamwambia, Jinsi gani basi Musa aliamuru kumpa hati ya talaka, na kumwacha? Akawaambia, Musa, kwa sababu ya* ***ugumu wa mioyo*** *yenu, aliwapa ruhusa kuwaacha wake zenu; lakini tangu mwanzo haikuwa hivi"*

Mafarisayo walikuwa wakitafuta namna ya kumtega. Hata hivyo hilo halikuwa muhimu sana kuliko suala la kutafuta uhalali wa Musa kuruhusu talaka.

Yesu alichofanya ni kuhamisha mjadala. Tusijadili kuhusu "talaka" na "maamuzi ya Musa" bali suala la "ugumu wa mioyo ya watu". Kimsingi Mafarisayo walitaka kumtwisha lawama Musa kwa uamuzi alioufanya lakini ni wazi kuwa uamuzi aliofanya Musa ulikuwa kwa faida yao baada ya kuonekana wazi kuwa kulikuwa na tatizo ndani ya mioyo ya watu na ikiwa wasingeruhusiwa kuwaacha wake zao madhara yangekuwa makubwa.

Tupo kwenye jamii ambayo inapotokea watu kupeana talaka anatafutwa mtu wa kulaumiwa nje ya hawa walioshindwana, yaweza kuwa ni viongozi wa dini, wazazi, marafiki ama pengine mamlaka kwa kile kinachosemwa kuwa *"aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe".* Ni kweli kabisa lakini Musa alishindwa kutowatenganisha. Wakati unajaribu kutafuta nani wa kumlaumu basi ni vyema kujua kuwa Musa alishindwa akaona yafaa watu watengane na Yesu mwenyewe alikuwa na ujasiri wa kutosha kumtetea Musa.

*Musa na Wayahudi*

Talaka ya kwanza ilitolewa na Musa na aliitoa kwa wayahudi. Ikiwa pengine unahitaji kuelewa zaidi, nikukumbushe kuwa Musa ndiye nabii wa kwanza kwenye historia ya masuala ya kiimani, ndiye aliyeandika vitabu vitano vya sheria za Mungu, ndiye mwanadamu pekee mwenye historia ya kumuona Mungu kwa macho yake mubashara. Musa ndiye aliyeandika kitabu cha Mwanzo wakati yeye alizaliwa kitabu cha Kutoka.

Kimsingi zile habari zote za bustani ya Edeni kuhusu Adam na Eva, Nuhu na gharika, mnara wa Babeli, Ibrahimu na Sara; Isaka, Jakobo na watoto wake kumi na mbili ambao ndio waliunda makabila kumi na mbili ya taifa la Israeli, habari za Yusufu kuuzwa Misri na mpaka wanaingia kwenye utumwa. Musa aliandika hizi taarifa zote kwa usahihi kwa uweza wa Mungu. Musa ndiye mtu ambaye mwili wake walikuja malaika kuupigania ili usichukuliwe na shetani alipofariki. Kimsingi hakuwa mtu wa kawaida kabisa tena hajakuwepo mwanadamu wa kufananishwa na yeye. Sasa mwanadamu mwenye kiwango hiki cha kutumiwa na Mungu alishindwa kupambana na wanadamu kiasi kwamba akaruhusu wapeane talaka.

Hawa wanadamu aliowashinda sio wanadamu wa kawaida, ni wayahudi, taifa teule la Mungu. Watu ambao Mungu aliwatenga na kusema katika wanadamu wote hawa ndio taifa langu na mimi ndio Mungu wao. Wayahudi walishuhudia Farao akipigwa mapigo kumi na Mungu wakiwa Misri.

Mbele za macho yao waliona mkono wa Mungu jinsi ulivyokuwa na nguvu na uwezo wa hali ya juu mpaka Farao akawaruhusu waondoke. Pamoja na hayo walishuhudia bahari ikigawanyika nao wakapita katika nchi kavu, bado watu wa hawa wakawa na mioyo migumu kiasi kwamba Musa hakuwa na budi kuwaacha waachane, akawapa hati ya talaka.

Ikiwa tunahisi kuwa suala la talaka ni jambo rahisi kiasi kwamba tunakuwa na mijadala ya kubishana basi hatujaelewa vyema Musa ni nani na wayahudi ni watu gani. Tukielewa hili tu inatosha sana kutufanya tubadili namna tunavyolijadili suala la talaka. Kama Musa na wayahudi walishindwana kiasi cha kufikia hapa basi sisi hatupo salama sana, kuendelea kuwa na mjadala mwepesi ni kuendelea kuangamizana sisi kwa sisi.

*Hapo mwanzo haikuwa hivyo,*

Kuna jambo lilitokea katika katikati ya safari ikapelekea Musa kufanya maamuzi magumu. Hatuoni suala la talaka katika historia ya ulimwengu mpaka wakati wa Musa. Kwa sasa tunaweza tusiwe na maelezo ya kina lakini ni wazi kuwa kuna jambo lilitokea ambalo halikumpa Musa mwanya wa kuruhusu watu kuendelea kubaki pamoja, kwa maneno mafupi Yesu anasema “Ugumu wa Mioyo”

Je, kuna mtu au mamlaka inayopaswa kulaumiwa kuhusu suala la talaka? Kwa maelezo ya Yesu, Hapana. Talaka ni idhini inayotolewa kwa watu ambao kwa hiyari yao walioana na kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao

wameshindwa kuendelea kuishi pamoja, ukitaka kujiridhisha kwenye hili utagundua kuwa hakuna mke na mume wanaoishi kwa Amani, upendo na furaha huenda kuomba talaka. Tunapofikia hatua hii basi ni wazi kuwa watu hawa wameshindwa kuishi pamoja. Hii haimaanishi kuwa talaka ni jambo jema. Yesu mwenyewe alionyesha wazi kuwa "mwanzo haikuwa hivyo" na tena kuna athari mbaya za kiroho na kijamii kwa watu kupeana talaka lakini hata hivyo viongozi wa dini, wazazi, jamii na mamlaka kama ilivyokuwa kwa Musa, hazipaswi kulaumiwa pale wanapoona ni vyema watu kutengana. Tatizo sio wao bali ni ugumu wa mioyo ya huyu mke na mume.

Kama Mungu alivyowaunganisha, mwanadamu hapaswi kuwatenganisha na Yesu anaonyesha wazi kuwa tatizo halikuwa kwa Musa aliowatenganisha bali ugumu wa mioyo. Hivyo basi tatizo la Moyo Mgumu ni suala ambalo lipo nje ya uwezo wa mwanadamu. Katika hili tujue basi kuwa tunawajibu wa kujifunza kwa undani sana dhana nzima ya moyo mgumu.

Hapa kuna haja kubwa ya kubadili mwenendo wa mjadala. Badala ya kujadili kuhusu talaka inapaswa tujadili kuhusu "moyo mgumu". Tunajua wazi kuwa tatizo sio talaka. Talaka haikuwahi kuwa tatizo na wala haikuwahi kuwepo isipokuwa pale ambapo watu walianza kuwa na mioyo migumu. Talaka ni matokeo tu, tatizo la msingi ni mioyo migumu. Ikiwa tunahitaji kutibu tatizo la talaka basi tunapaswa kusahau kuhusu talaka kwanza na tuelekeze nguvu na jitihada kwenye kiini cha talaka ambacho ni mioyo migumu. Tunapaswa kuogopeshwa na

ugumu wa mioyo ya watu kuliko tunavyoogopeshwa na takwimu za talaka katika mahakama. Tunapaswa kupunguza vikao vya kusuluhisha watu wasiachane na kuelekeza nguvu kwa kuponya mioyo ya watu husika.

Hakuna kiwango cha mjadala kuhusu talaka kinachoweza kutatua tatizo hili, ndio maana Yesu alihamisha mjadala. Tunaweza tukatumia muda mwingi na rasilimali nyingi kupambana na talaka lakini hakutakuwa na matokeo chanya, ikiwa wanaofunga ndoa wana mioyo migumu tunapaswa tutarajie talaka na kama tutawazuia kuachana basi tutarajie wao kuumizana, kunyanyasana, kuuana kihisia, kifikra na kiroho pia.

Ikiwa viongozi wa dini na mamlaka zinafungisha ndoa watu wenye mioyo migumu halafu tunashangaa ama kuzuia wakitaka kuachana basi tutakuwa hatuwatendei haki. Lakini je, tunajua nini kuhusu moyo mgumu? Nini dalili za moyo mgumu? Nini kiini chake?

## SURA YA 2

# CHANZO CHA MOYO MGUMU

---

Moyo mgumu ni matokeo ya mwanadamu kuacha kabisa kumtegemea na kumtumaini Mungu na kuanza kutegemea na kutumaini akili, uwezo na mazingira yake. Mwanadamu alipoumbwa alisanifiwa kwa namna ambayo uhai wake unategemea uhusiano wake na Mungu. Pale ambapo mwanadamu anashindwa kumtegemea Mungu basi anaanza rasmi safari ya kutengeneza moyo mgumu. Kuna mambo mawili tu humpelekea mwanadamu apoteze Imani kwa Mungu na kuanza kuamini katika uwezo na mazingira yake.

1. Hali ngumu anayopitia
2. Maarifa makubwa ya kidunia

HALI NGUMU

Mwanadamu hakuumbiwa uwezo wa kukabiliana na shida na hali ngumu kwa muda mrefu. Kila mwanadamu amepewa ustahimilivu wa mambo magumu kwa kipindi fulani lakini ikiwa hali hiyo itakuwa yakudumu kwa muda mrefu athari zake zinapelekea kuwa na moyo mgumu. Hili linaweza kuwa jambo la kustaajabisha lakini ni ukweli.

Habari ya moyo mgumu uliopelekea watu kupeana talaka ilianza baada ya wana wa Israeli kuwepo utumwani Misri kwa miaka takribani mia nne na thelathini. Kabla ya huu

uzoefu wa kuwepo utumwani kwenye mateso mengi hatuoni habari ya watu kuwa na mioyo migumu na wala hatuoni suala la talaka.

Safari ya tatizo la moyo kuwa mgumu kwa mwanadamu ilianzia pale alipoondolewa bustani ya Edeni. Maisha yake yakaanza kutegemea mazingira ambayo hayakuwa yameandaliwa mahususi kwa ajili yake kama ilivyokuwa ndani ya bustani. Huku walipaswa kujiandalia mazingira wenyewe na kisha kuyatumia mazingira hayo kuendesha maisha yao. Walipaswa kuanza kufanya mambo ambayo kwa asili hawakuumbwa nayo na pengine hawakuwa na uwezo wa kuyafanya; kulima, kufuga na kufanya kazi kwa jasho ili kupigania uhai wao. Hapa ndipo kwa mara ya kwanza tukashuhudia athari za moyo mgumu kwa Kaini kumuua ndugu yake kwa sababu ya wivu uliokomaa mpaka kuzaa chuki.

Hata hivyo kuna namna ambayo Mungu aliyarahisisha maisha ya watu wachache aliowateua kwa ajili ya kusudi lake mwenyewe na hivyo hatulioni tatizo la moyo mgumu kwao hata baada ya Adam na Eva kufukuzwa bustanini. Hii ni kusema kuwa kuna namna ambayo Mungu alirahisisha maisha yao ndio maana hawakupatwa na madhara ya kuishi katika hali ngumu.

Hata hivyo katika kipindi hicho hicho ambacho Mungu alitenda kazi na watu wachache utaona wale ambao hawakuteuliwa na Mungu bado walipatwa na tatizo hili la kuwa na moyo mgumu. Hapa ndipo upokutana na suala la gharika la Nuhu ambalo biblia inaeleza wazi jinsi watu walivyokuwa na mioyo migumu kiasi kwamba Mungu

akaamua kuangamiza ulimwengu mzima na kumteua Nuhu na familia yake tu.

Tatizo hili halikukoma kwa kuwa bado wanadamu waliishi maisha ya kutegemea watu na mazingira, hivyo tukaliona tatizo hili likiwa dhahiri sana katika mji wa Sodoma na Gomora. Watu walikuwa na mioyo migumu kiasi kwamba ikampelekea Mungu kuangamiza mji wote kwa moto. Ukisoma mazungumzo baina ya malaika na Ibrahimu wakati malaika wakielekea Sodoma na Gomora utaona vile ambavyo hali ilivyokuwa mbaya.

Kitu ambacho utagundua ni kuwa wateule wa Mungu akiwemo Habili, Henoko, Nuhu, Ibrahimu na uzao wake walikuwa na kibali fulani kwa Mungu ambacho kiliwapa kufanikiwa kirahisi sana katikati ya hali ngumu ambazo wengine walipitia na hata pale walipokuwa wanapitia hali ngumu kuna namna Mungu aliwapa njia rahisi ya kuvuka na iliwalinda na tatizo la kuwa na moyo mgumu. Hali zao za maisha ziliwasaidia sana kumwamini na kudumu katika kumtegemea Mungu, sio kwa sababu walikuwa watakatifu na wakamilifu bali Mungu aliamua kujidhihirisha kwao kwa makusudi yake na hivyo ikawa rahisi wao kumcha Mungu. Utaliona hili pia kwenye mazungumzo baina ya Mungu na shetani kuhusu Ayubu;

***Ayubu 1:8-11***..*"Kisha BWANA akamwuliza Shetani, Je! Umemwangalia huyo mtumishi wangu Ayubu? Kwa kuwa hapana mmoja aliye kama yeye duniani, mtu mkamilifu na mwelekevu, mwenye kumcha Mungu na kuepuka na uovu. Ndipo shetani akamjibu BWANA, na kusema, Je! Huyo Ayubu yuamcha BWANA bure? Wewe hukumzingira kwa*

*kingo pande zote, pamoja na nyumba yake, na vitu vyote alivyo navyo? Kazi za mikono yake umezibariki, nayo mali yake imeongezeka katika nchi. Lakini nyosha mkono wako sasa, uyaguse hayo yote aliyo nayo naye atakukufuru mbele za uso wako."*

Unaweza kuona wazi kuwa kulikuwa na uhusiano wa moja kwa moja baina ya suala la Ayubu kumcha Mungu na Mungu kumlinda, kumbariki na kuongeza mali za Ayubu. Maisha mazuri aliyokuwa anaishi Ayubu ndio yalichochea yeye kumcha Mungu na kutokea kwenye haya mazungumzo ndipo makubaliano ya Mungu na shetani yakawekwa kumjaribu Ayubu. Majaribu hayo yakalenga kumfanya apite kwenye hali ngumu na lengo likiwa kumfanya awe na moyo mgumu.

Ukisoma habari za Ibrahimu, Isaka, Yakobo utaona vile ambavyo Mungu aliwajibu kirahisi maombi yao yaliyohusiana na maisha yao na ikawasaidia sana kuepukana na tatizo la moyo mgumu.

Katika habari ya wateule wa Mungu, tatizo la moyo mgumu lilianza walipokuwa wahamiaji Misri na akazaliwa Farao asiyemjua Yusufu. Na wao kwa mara ya kwanza kama taifa teule wakaondolewa kwenye maisha ya kumwamini na kumtegemea Mungu, kubarikiwa na kuongezewa mali zao na Mungu, wakashurutishwa kuwategemea mabwana zao yaani wa Misri kwa kuwa sasa walikuwa hawawezi kufanya kazi zao kwa sababu ya utumwa. Hata chanzo cha wao kuingia utumwani ni kilekile cha Ayubu, waliongezeka idadi, wakawa wana nguvu kuliko wa Misri, hofu ya Farao ikamfanya awadumbukize kwenye utumwa. Wao nao

wakawa kama mataifa mengine ambayo hawakuishi kwa Baraka za Mungu bali kwa kutegemea mazingira na watu wengine.

Hawakuwa na uhuru wa kuabudu, hawakuwa na kazi za mikono ambazo Mungu angewabariki kwazo, maisha yao yakaegemea utawala wa Misri. Chakula chao, mavazi yao na kila kitu chao wakategemea wamisri. Utegemezi wa lazima juu ya mazingira na watu waliowazunguka ukaua Imani yao kwa Mungu. Tumaini lao likawa juu ya mazingira na wanadamu wenzao, wakajeruhiwa nafsi zao na kisha ukazaliwa moyo mgumu ndani yao. Huu moyo mgumu ndio ukapelekea safari yao kurudi Kanani ikawa ngumu, wakajichongea sanamu kama za Misri, wakamkufuru Mungu wao, wakatamani matango, nyama na makaburi ya Misri, wakashindwa kuhusiana wao kwa wao kiasi cha kudai talaka.

Kimsingi tunapozungumzia moyo mgumu suala la talaka ni jambo dogo sana katika athari za jumla za tatizo hili. Athari zake zilipelekea mpaka kizazi chote cha waliotoka Misri kuangamizwa jangwani kama ilivyokuwa katika gharika wakati wa Nuhu na moto wakati wa Lutu. Kama wangepona tatizo hili basi wangeingia Kanani, wasingechonga sanamu na ndoa zisingevunjika.

Hivyo basi tunavyozungumzia moyo mgumu tusiishie kwenye talaka bali tunapaswa kuona athari kubwa zaidi japo talaka inaweza kuwa ni kiashiria mojawapo.

Mioyo migumu ya watu hawa ilikuwa ni matokeo ya shida, mateso, njaa, kunyanyaswa, kufanyiwa ukatili wa kimwili, kififikra na kihisia. Kunyang'anywa uhuru na kutwezwa utu wao, uzoefu huu ulizaa mioyo migumu. Sifikiri kuwa ikiwa mmoja kati ya hao alijua kuwa kunaweza kuwa na athari mbaya zaidi kuliko zile za kuumia na kuchoka mwili. Wengi walichoona ni mateso ya nje lakini ambacho hawakujua ni kuwa athari za kifikra na kihisia zilizojitokeza zilikuwa ni mbaya zaidi na madhara yake yalibaki hata baada ya wao kutoka utumwani.

Miaka arobaini baada ya kutoka utumwani wakiwa jangwani athari za mateso na maumivu waliyopitia ziliendelea kuwatafuna. Ziliendelea kutafuna amani na furaha za ndoa zao kiasi kwamba wakalazimika kuachana. Ghafla unaanza kugundua kumbe wakulaumiwa hakuwa Musa wala mke wala mume bali Farao. Kuna kitu unaanza kukielewa?

Ukirudi kwenye asili ya kuumbwa mwanadamu utagundua miongoni mwa mambo ambayo hayakukusudiwa kuwa fungu la mwanadamu ni maisha ya shida na mateso. Shida na mateso ilikuwa ni adhabu aliyopewa mwanadamu baada ya kumuasi Mungu kwenye bustani ya Edeni. Ukitazama vizuri jinsi Mungu alivyoandaa mazingira mazuri kabla ya kumuumba mwanadamu utagundua kuwa nje ya mazingira ya utulivu, amani na furaha zipo athari ambazo humpata mwanadamu kwa kuwa tangu mwanzo hakuumbwa kukaa kwenye mazingira magumu. Hili linawezekana lisionekana kwa haraka lakini ukichunguza kwa undani utagundua kuwa kadri wanadamu walivyoishi maisha

magumu ndivyo tabia zao zilivyozidi kubadilika na kuanza kufanya vitendo ambavyo vilikuwa sio vya asili ya kibinadamu.

Kwa dhana hii itoshe tu kusema kuwa;

*“Mazingira yoyote ya shida, mateso na manyanyaso ni hatari sana katika moyo wa mwanadamu. Athari zake hudumu kwa muda mrefu hata baada ya kuondokana nayo. Na hayo ndio chanzo cha Moyo kuwa Mgumu”*

Mtu anapopitia hali ngumu kwa muda mrefu inaanza kumfanya ndani ya moyo wake kupoteza tumaini la uwepo wa Mungu na kuanza kujipambania mwenyewe. Kadri anavyozidi kujipambania anaongeza utegemezi juu ya uwezo wake, juu ya mazingira yaliyomzunguka na juu ya watu waliomzunguka. Utegemezi huu unamuweka kwenye mazingira ya kuumizwa zaidi na kujikuta yupo kwenye hali ngumu zaidi na mzunguko unaendelea tena na tena na hata tatizo kuongezeka. Hivyo kadri anavyozidi kuweka utegemezi ndivyo anavyozidi kuwa kwenye hali ngumu na ndivyo Imani yake kwa Mungu inavyozidi kufa na ndivyo moyo unavyozidi kuwa mgumu zaidi.

*Tathimini ya Uzoefu wa maisha ya watu wengi*

Nyakati hizi wengi hupitia manyanyaso na ukatili ikiwa ni wa kijinsia, kimwili, kingono na hata kihisia, Kuanzia kwenye malezi, safari ya elimu, mahusiano hata sehemu za kazi. Asilimia kubwa ya watu, ikiwa ni kwa kujua ama

kutojua hujikuta katika mazingira magumu kwa namna moja ama nyingine. Wapo ambao hufanikiwa kutoka haraka kwenye hali ngumu, hawa huwa wanakuwa salama. Wale ambao hudumu katika hali hizo ngumu kwa muda mrefu ndio hudumbukia kwenye tatizo la kuwa na moyo mgumu.

Hatuwezi kukwepa hali ngumu. Duniani mna dhiki, lakini ikiwa mtu atashindwa kuepukana na hali ngumu ama kuwa na maarifa sahihi ya kumfanya asiathiriwe na hali hiyo na kudumu katika hali hiyo kwa muda mrefu basi hatari ni kuwa atakuwa muhanga wa moyo mgumu.

*Mfano;*

Mtoto ambaye amejikuta ananyanyaswa na mzazi wake ikiwa ni kihisia ama kifikra. Ama amefanyiwa ukatili wa kimwili ama kingono ama kifikra na akakosa msaada wa karibu wa kusaidiwa na hali ile ikadumu kwa muda mrefu kwa maana ya kuendelea kutendewa ubaya huo ama kumbukumbu ya vitendo hivyo vya unyanyasaji na ukatili vikabaki kwenye fikra na hisia zake pasipo msaada wa haraka basi mtoto huyu atatengeneza moyo mgumu. Imani yake kwa Mungu inakufa na anaona katika ulimwengu huu ni vyema kujilinda na kujipambania mwenyewe maana hakuna usalama. Anakuwa akiamini kuwa dunia haina usalama na hakuna anayejali maisha yake.

Mzazi anamkalipia mtoto, anampiga mtoto, anamtesa mtoto, anamuumiza mtoto. Baba anamtelekeza mtoto, mama anamtamkia mtoto maneno magumu. Ndugu anambaka au kumlawiti mtoto. Mtoto anapewa kazi ngumu kuliko uwezo wake, ananyimwa chakula, hana pa

kulala. Jamii inachoona ni unyanyasaji na ukatili kwa watoto lakini athari za hayo huwa ni za kudumu hata baada ya matukio hayo kupita.

Wazazi na walezi lazima kujua kuwa vitendo vibaya vya unyanyasaji kwa watoto athari zake huwa mbaya na hupelekea hawa watoto wawe hatari sana kwa jamii. Tunapoona wimbi la watoto wa mtaani, watoto yatima, watoto wanaolelewa kwa taabu na mzazi mmoja; tunachopaswa kujua tunatengeneza watu wenye mioyo migumu ambao watakuja kuharibu dunia hii siku za usoni. Tunapopambana na ukatili na unyanyasaji dhidi ya watoto tutazame miaka ishirini ijayo pia ni matokeo ya hayo ambayo watoto wanapitia leo. Kizazi kinachotengenezwa ni kizazi hatari ambacho haijalishi wataona Mungu akitenda matendo makuu kiasi gani ni vigumu sana wao kumuamini kama ilivyokuwa kwa Wayahudi enzi za Musa.

*Mfano;*

Mume na mke wameoana kwa kupendana kabisa hawakulazimishwa na mtu. Mume ameamua tu kumnyanyasa mke na kumfanyia ukatili. Hajali kuhusu maumivu ya mke. Akiamua kumpiga, anampiga, akiamua kumbaka, anambaka. Akiamua arudi nyumbani alfajiri sawa tu. Akiamua kuwa na wanawake wengine kwake sawa tu. Amuhudumii kwa hali wala kwa mali. Ahudumii mama wala watoto. Kaamua kuishi kama mseja wakati ameoa. Mume mjeuri, mgomvi, mkali, anapiga, muhuni, asiyejali; kwake anaona ni sawa tu ila asichokijua ni kuwa hayo maumivu anayompatia mke wake yanamtengenezea

mwanamke kuwa na moyo mgumu. Na athari za huo moyo mgumu kwa mke wake zitakapoanza kujitokeza atajikuta ana wakati mgumu sana kuishi na huyo mwanamke na pengine ndio kufikia kwa mkewe kuomba talaka. Nini kimetokea? Amempitisha mwanamke kwenye hali ngumu kwa muda mrefu na mwisho wa siku amekuwa kama walivyokuwa Wayahudi enzi za Musa.

Ama sasa ndo mwanamke kaamua tu kuwa kichomi. Hajali, hana adabu, hana heshima, sio mtii, mwenye kutukana, mgomvi, mpiganaji, mlevi.. katoka alipotoka na tabia zake na kaamua kuwa kwazo kwa mume wake. Anaona ni kawaida tu kutokuwa mwaminifu. Tena anajisifu mwanaume anavyomnyenyekea na kumlilia. Jeuri yake inaongezeka. Asichokijua ni kuwa kadri muda unavyozidi kwenda mbele moyo mgumu unaumbika ndani ya huyo mumewe. Mara ghafla unashangaa mwanaume amekuwa kiumbe tofauti na anaanza kukufanyia matukio ya ajabu. Yule uliyedhani unammudu hummudu tena bali anageuka mwiba kwako. Nini kimetokea? Umemfanya kuwa na moyo mgumu, hana cha kupoteza. Matokeo yake unapoteza kilichokuwa bora kwako.

*Mfano;*

Mwanamke na mwanaume wapo kwenye mahusiano. Mmoja wao ameamua kumuumiza tu mwenzake bila sababu za msingi, kumuacha hataki ila kila kukicha kumnyanyasa. Watu wapo kwenye mahusiano lakini mpaka wanapigana, wanaumizana, wanasalitiana.. lakini kuachana hawataki. Wanatesana tu mchana na usiku na kuvunja mahusiano hawataki miaka inaenda. Hayo

maumivu wanayopitia wasichokijua ni kuwa wanatengenezeana mioyo migumu na mwisho wa siku ikiwa uhusiano huo utavunjika au utadumu tayari wameshaharibiana mioyo.

Uhusiano wao ukivunjika ndio wanaoenda kuwatesa watu wengine huko kwa tatizo walilojisababishia wenyewe kwa kupenda kukaa kwenye shida kwa hiyari wakati wangeliweza kuachana tu yakaisha. Wakioana wakati tayari walishaumizana na mioyo ishakuwa migumu ndoa inaanza kusumbua. Wanadhani tatizo la leo lakini kumbe ni wakati wakiwa wachumba walishatengeneza tatizo muda mrefu sana. Ndoa inayumba tunadhani shida ni ya leo kumbe ni ya muda mrefu.

*Mfano;*

Mwanamke hujaolewa unaamua tu kuzaa mtoto, eti mwanaume aliomba nimzalie. Na mwanaume naye anaomba azaliwe mtoto bila kuoa. Je Mnajua mnachokifanya kwenye maisha ya huyo mtoto ni Kumtengenezea moyo mgumu. Mtoto anayekosa malezi ya wazazi wote wawili yupo kwenye hatari kubwa ya kupata tatizo la moyo mgumu.

Mwanamke naye anataka kuzaa, hana rasilimali za kutunza hata hiyo mimba, mkataba na huyo mwanaume kutunza mimba hana. Huku ni kujiingiza kwenye hali ngumu tu halafu upate tatizo la moyo mgumu uanze kulaumu wanaume kuwa wana matatizo kumbe wewe ndo unapenda shida. Matokeo yake tunakuwa na mwanamke mwenye moyo mgumu kwa sababu ya shida za kulea na kutunza mimba na mtoto peke yake na mtoto mwenye

moyo mgumu kwa sababu ya shida ya maisha, msongo wa mawazo wa mama na kukosa malezi ya wazazi wawili. Haya mambo ya kuzalishana bila mpango ni kututengenezea tu kizazi cha watu wenye mioyo migumu.

*Mfano;*

Biashara ni ngumu kila siku kuna hasara ila kwa kuwa umeizoea basi umekazana na hiyo hiyo. Usichokijua ni kuwa hizo hasara za kila siku na kufanya biashara isiyo na faida na kujichosha kila siku taratibu unajitengenezea moyo mgumu. Kwani kuna ugumu gani kutafuta namna ya kuboresha ama kubadili biashara? Kwa nini ushikamane na hali ngumu kwa muda mrefu.

*Mfano;*

Kazi huipendi, mwajiri wako humpendi, wafanyakazi wenzako huwapendi, mazingira ya kazi huyapendi na bado kila asubuhi unaamka unaenda kwenye mazingira hayo. Msongo wa mawazo upo juu kila siku. Ukiulizwa nini unasema ni shida tu ya hela. Sasa unapata pesa lakini unajitengenezea moyo mgumu. Matokeo yake unaanza kuwa na tabia zisizoeleweka kazini, watu wanashangaa kuwa una matatizo gani kumbe tayari ushakuwa na moyo mgumu.

*Mfano;*

Kozi huipendi na hutaki kusoma lakini kwa sababu huna namna umeenda chuo kusoma. Kubadili mtazamo wako dhidi ya kozi hiyo hutaki. Moyo umeikataa, hupendi

mazingira ya chuo, hupendi walimu wote, hupendi kila kitu. Na unaona fahari kusema hupendi. Unachoona wewe ni kutopenda chuo na kozi ila usichoona ni kwamba unajitengenezea moyo mgumu. Ukianza kusumbua watu baada ya muda fulani ndipo unajishangaa una shida gani kumbe ni kujiweka kwenye shida kwa hiyari yako mwenyewe.

*Mfano;*

Kiongozi wa dini ameamua kuwalemea waumini wake na mzigo wa mafundisho ya uongo, vitisho na kufanya mambo yaliyo nje ya uwezo wao kifikra, kiimani na kiuchumi. Ndiyo tunapaswa kuijenga kazi ya Mungu lakini ikiwa ni nje ya uwezo wao na Imani yao kwa Mungu ni haba unaweza kuwaingiza washirika kwenye moyo mgumu. Ikiwa uwezo wao wa kiuchumi ni mdogo na kuna kazi kubwa ya kufanya wekeza kwanza kwenye kuijenga Imani yao kwa Mungu vinginevyo utawalemea na kile kilichokusudiwa kuwa Baraka kwao kitageuka laana kwa kuwa hawatafanya kwa moyo wa kupenda.

Jipe muda, acha Imani yao ikue ili wasijikute suala la kumtumikia Mungu linageuka mateso kwao. Mwisho wa siku hata kile kidogo walichonacho wataacha kutoa na kwenye ibada wataanza kukwepa kuja kwa kuwa sasa wanaona Mungu ni muonevu. Nini kimetokea? Umewafanya kuwa na mioyo migumu.

Ama sasa washirika ndio wameamua kugoma kukua kiimani. Wanamlemea kiongozi wao kwa kila kitu. Kiongozi hali kwa amani, hapumziki; usiku na mchana anakimbizana na washirika. Huyu anaumwa, huyu ana

msiba, huyu kavamiwa na pepo, huyu kajifungua, huyu haji kanisani. Kiongozi anapitia hali ngumu. Wanachokiona washirika ni upendo wa kiongozi kwao ila wasichojua ni kuwa wanamtengenezea kiongozi huyo moyo mgumu. Ghafla anaanza kuwa na hasira juu yao, mahubiri ya kuwasema na kuwakaripia, ufunuo hakuna tena, anaanza kuwalemea na mambo magumu. Nini kimetokea? Mmempitisha kwenye hali ngumu mkamfanya kiongozi kuwa na moyo mgumu.

Unaona mlolongo wa mambo ulivyo? Unagundua kuwa suala la moyo mgumu ni jitihada za jumla za jamii nzima. Kuanzia wazazi, jamii, viongozi wa dini, walimu, mtu mmoja mmoja mpaka serikali. Lazima tuwe na jitihada za makusudi za kila mmoja kumlinda mwenzake asiingie kwenye hali ngumu kutokana na maamuzi yake mabaya.

Serikali inaweza kuweka sera tu za kiuchumi, kiafya na kielimu, ijapokuwa ni kwa nia njema, ikiwa hazitatolewa ufafanuzi mzuri, zinaweza kuleta hali ngumu kifikra, kihisia na kiuchumi kwa wananchi na wakajikuta wanapata mioyo migumu na kuanza kuisumbua serikali.

Mtu anaweza kusalimika kwenye malezi akapata shida shuleni akadumbukia kwenye moyo mgumu. Anaweza akawa salama malezi na shuleni akapata shida kwenye mahusiano na ndoa, yawezekana huko pia anaweza kuwa salama akapata shida kazini au kwenye biashara. Na anaweza kufanikiwa kote lakini akapata shida kutokana na hali ya uchumi wa nchi.

Jumla ya mambo haya ni kuwa kila mahali mwanadamu amesongwa na hatari ya kukutana na mazingira ya hali ngumu. Katika hayo machache niliyoorodhesha hapo juu waweza ongeza vita, njaa, ukame, mabadiliko ya hali ya hewa dunia. Tuyaonapo hayo tutambue kuwa mkakati nyuma ya hayo ni kuwafanya watu kuwa na mioyo migumu na mwanadamu akishakuwa na moyo mgumu anakuwa wakala mzuri sana wa kuendelea kuiharibu dunia.

Tukisema tunapambana dhidi ya umasikini, vita, maradhi, ukame na njaa, uharibifu wa mazingira, ufisadi na rushwa, unyanyasaji na ukatili wa kijinsia, watoto, kingono na kimwili, talaka na jukumu hilo tunalikabidhi kwa watu wenye mioyo migumu basi tuna safari ndefu sana ya kuelekea.

## MAARIFA YA ULIMWENGU

Mwanadamu anapokuwa na uwezo mkubwa wa maarifa ya jinsi ya kuishi ulimwenguni, utegemezi wake kwa Mungu hupungua, Imani hufa. Hilo humfanya ategemee zaidi mazingira yake na watu na kwa kadri anavyozidi kutegemea hivyo anajiweka kwenye mazingira ya kuwa na hali ngumu na matokeo yake ni kuwa na moyo mgumu.

Kimsingi mwanadamu anapoteza hali ya kumtegemea Mungu, anapoteza uwezo wa kujitawala kutokea ndani yake na kuruhusu mazingira ya nje kumtawala. Hali yake ya ndani inaanza kutegemea matukio ya nje.

Mazingira ya nje yanaanza kuwa na ushawishi juu ya hali yake ya ndani. Mazingira ya nje yakikosa utulivu na ndani yake kunakosa utulivu. Hali yake ya ndani inaanza kuamriwa na kile kinachoendelea nje. Mahusiano, hali ya kiuchumi, hali ya teknolojia, taarifa anazopokea zinakuwa na ushawishi mkubwa zaidi kwake. Anapoteza maisha yake na kuanza kuishi kulingana na mawimbi ya matukio yanayotokea nje. Na huu unaanza kuwa mwanzo wa kuharibikiwa kwa kuwa chochote kinachoharibika nje kinamuharibu yeye ndani.

Kutumia maarifa na ujuzi mwingi kuishi dunia bila kumtegemea Mungu inaweza kuonekana ni jambo la kifahari mpaka pale utakapojikuta umekuwa mtu wa mazingira ambayo unayategemea kuishi. Pale utakapogundua kuwa hayo mazingira nayo yanatawaliwa na watu wengine ambao sasa wana uwezo wa kuamua hali yako ya ndani kwa kucheza tu na hali ya mazingira.

Ni kama tu unapokuwa na mpenzi ambaye unamtegemea sana kihisia. Akikasirika siku yako imeharibika. Kifuatacho ni kuanza kufanya kila kinachowezekana ili umfurahishe maana furaha yako inategemea furaha yake.

Sasa umeweka tumaini juu ya maarifa na ujuzi wako na maisha yako yanategemea hapo. Maarifa na ujuzi huo umeshikamanishwa na mifumo ya kiuchumi, mifumo ya kiteknolojia, intaneti, mifumo ya afya, mifumo ya elimu na taratibu mifumo hadi ya chakula. Maana yake utegemezi wetu wa maarifa ya dunia umetufanya tuweze kutawaliwa hali zetu na mifumo iliyotengenezwa na watu wachache.

Siku wakiamua kuvuruga mifumo ya uchumi wote hatuna hela. Siku wakiamua kuvuruga mifumo ya teknolojia wote hatuna umeme, hatuna mawasiliano, hatuwezi kufanya kazi, hatuwezi kulala wala hatuwezi kula.

Kimsingi wingi wa maarifa umefanya maisha yetu yawe kiganjani mwa watu wachache. Sasa utegemezi wetu unapokuwa kwa hawa watu wachache na wao wakaamua kuvuruga mifumo wanaweza kutufanya tuingie kwenye hali ngumu na kuwa na mioyo migumu.

Wakati ambapo watu wa bara la Afrika wana mioyo migumu kwa sababu ya Hali ngumu zitokanazo na shida na mateso, Ulaya pia watu wana mioyo migumu kwa sababu ya kutegemea Maarifa ya kidunia na hivyo mifumo inatawala maisha yao. Wote hatupo huru dhidi ya mioyo migumu ila tu tumefikia hapo kutokana na njia tofauti.

## SURA YA 3

# MOYO MGUMU NA AFYA YA AKILI

---

Afya ya akili imekuwa mjadala wa ulimwengu mzima. Madhara ya tatizo la afya ya akili ni dhahiri sana. Jamii imepigwa na janga hili kiasi cha kuanza kuona athari zake wazi kabisa. Hatuwezi kupuuzia tena uwepo wa tatizo hili. Na lazima hatua za makusudi zianze kuchukuliwa ili kutatua tatizo hili. Jambo gumu kuliko yote kuhusu tatizo la afya ya akili ni kuwa tunaona zaidi matokeo kuliko kiini cha tatizo hili.

Tusichojua kuhusu tatizo la afya ya akili ni kwamba ni tatizo ambalo linaanzia pale mtu anapopoteza mawasiliano na yeye mwenyewe. Anapopoteza utawala dhidi yake yeye mwenyewe yaani utashi, fikra, hisia na maamuzi yake na kujikuta mazingira ya nje yana ushawishi mkubwa zaidi kwake. Pale anapojikuta anategemea mahusiano ili maisha yake yaende na hivyo stamina ya maisha yake inategemea huruma za wale anaohusiana nao. Pale anapotegemea hali ya uchumi, ajira ama biashara na hivyo stamina ya maisha yake inategemea stamina ya mambo hayo.

Hali ya kupoteza kabisa uwezo wa kuwa na amani na furaha akiwa mwenyewe bali lazima kuwa na mtu ama kitu ama kichochezi fulani kitakachomfanya aipate hiyo furaha na amani. Hajioni kama amekamilika isipokuwa kuwa kichochezi kutokea nje. Mwanaume hajioni kuwa mwanaume mpaka amekuwa na mwanamke, mwanamke

hajioni mwanamke mpaka amekuwa na mwanaume. Sintofahamu mbaya ya kwanza kuhusu tatizo la afya ya akili inaanzia hapa na kama hatutawezi kumfanya mtu ajipate mwenyewe basi kamwe hatutaweza kumsaidia kupona tatizo hili.

Na hapa ndipo utata unakuja maana hata wataalamu wa saikolojia wakati mwingine hufikiri kuwa tatizo la afya ya akili linaweza kuondoka kwa kumshauri mtu kubadili tabia fulani fulani. Kwa jinsi hiyo unafanikiwa kukata matawi ya tatizo lakini mizizi bado inakuwa pale pale.

Kutibu tatizo la afya ya akili linaanza kwa mtu kujipata yeye mwenyewe. Ili kujipata lazima mtu kuondoa utegemezi wake kwenye mazingira ya nje na kuanza kujitegemea mwenyewe kutokea ndani. Aweze kuishi pasipo kumtegemea mtu ama mfumo wowote. Hapa sizungumzii kutohusiana na watu ama mifumo ya ulimwengu bali kutoitegemea. Aweze kuwa na maisha yake pasipo kuwa na utegemezi wa watu na mazingira ya nje.

Sasa moyo mgumu, ikiwa ni kwa kutokana na hali ngumu ama maarifa ya ulimwengu, humfanya mtu kutegemea mazingira ya nje. Hali hii ya kuacha kumtumaini Mungu na kuanza kutumaini mazingira ndio humuweka mtu kwenye hatari ya kupata tatizo la afya ya akili.

Kimsingi Moyo Mgumu huzaa tatizo la afya ya akili. Moyo mgumu ndio kiini haswa cha tatizo hili na hakuna kiwango cha tiba ya tatizo la afya ya akili kinachoweza kukomesha tatizo ikiwa hatujaweza kutibu tatizo la moyo mgumu.

Ndio maana utagundua kuwa chanzo cha tatizo la moyo mgumu hakitofautiani na chanzo cha tatizo la afya ya akili kwa sehemu kubwa. Wengi wenye matatizo ya afya ya akili ni matokeo ya unyanyaswaji na ukatili waliowahi kukutana nao. Tunachokiona kwa nje ni tatizo la afya ya akili kwa watu hawa lakini kilichofichika ndani ya tatizo hili ni suala la moyo mgumu.

Hapa unaweza sasa kuelewa kwa nini kadri tatizo la afya ya akili linavyozidi kuwa kubwa ndivyo migogoro ya mahusiano, ndoa na talaka zinavyozidi kuongezeka, kinachoonekana kwa wengi wao ni migogoro na talaka. Kwa wataalamu wa saikolojia kinachoonekana ni tatizo la afya ya akili lakini kwangu mimi ninachoona ni mioyo migumu kama alivyoona Yesu. Kila mmoja kwa kadri ya kiwango cha ufahamu wake anaweza kuona kwa ukomo wake.

Kimsingi kuna uhusiano mkubwa sana baina ya moyo mgumu na tatizo la afya ya akili. Na namna nzuri ya kutibu tatizo la afya ya akili ni

- Kuhakikisha tunachukua hatua za makusudi za kila mtu kumlinda mwenzake dhidi ya hali ngumu kuanzia ngazi ya mtu binafsi, familia, jamii na hata serikali. Ikiwa tutaweza kuhakikisha kila mmoja anahakikisha hampi mwenzake hali ngumu kutokana na tabia zake au maamuzi yake basi tutakuwa tumepiga hatua moja kubwa kuelekea kutatua tatizo.
- Kuanza kupunguza utegemezi wa kifikra, kihisia na kiutashi kwa watu, mifumo ama mazingira ya nje.

> Kutoruhusu maisha yako kutawaliwa na mazingira na watu. Furaha na amani ya maisha itegemee wewe mwenyewe na sio mazingira ya nje kiasi kwamba chochote kikibadilika basi unakuwa kwenye msukosuko.

Kushindwa kupata suluhu la moyo mgumu ni kushindwa kupata suluhu la tatizo la afya ya akili. Matokeo yake unyanyasaji na ukatili utaongezeka, watu wataendelea kuumizana, migogoro itazidi kuwa mingi kwenye jamii na tatizo litazidi kuongezeka. Sifikiri kama tuna mbadala wa hili, Mbadala wake ni kuufikisha ulimwengu mwisho. Dunia haitakalika. Tunapoelekea ni kubaya kuliko tulipotoka. Tuliyoshuhudia ni mwanzo wa mambo ya hatari zaidi. Wakati wa maongezi na majadiliano umepita. Kujua ukweli kuhusu dhana ya moyo mgumu inapaswa kuwa mwitiko mkubwa kwa ulimwengu mzima kuwa sasa ni wakati wa kurudisha utegemezi wetu kwa Mungu. Kuinua Imani yetu na kumtumaini yeye aliye chanzo cha maisha yetu. Kutumaini watu, mazingira na mifumo ya ulimwengu huu inatuweka sisi kwenye hatari ya kuharibiwa na vivyo hivyo sisi nasi kuwaharibu wengine.

## SURA YA 4

# MADHARA YA MOYO MGUMU

---

Nini humpata mtu mwenye moyo mgumu? Kujibu swali hili kunaweza kukuonyesha kwa nini uwepo wa mtu mwenye moyo mgumu duniani unakuwa tishio kwa ustawi wa dunia na inawezekana kabisa akapoteza vigezo vya kuendelea kuwepo duniani, ndio maana wapo wengine ambao hufikia hatua ya kutamani kuondoka duniani ikiwa ni kwa msingi wa kwenda mbinguni ama kwenda jehanamu. Kivyovyote vile ni kwamba wanapoteza kabisa sifa ya kuwepo duniani na ujumbe anaopata akilini mwake ni kuwa bora aondoke aende huko asipopajua yamkini atapumzika dhidi ya shida na mateso. Sasa mtu mwenye kuwaza kuondoka duniani tukitegemea kuwa anaweza kuitunza dunia na mazingira yake na uchumi wake na kuwajali watu wake ni kujidanganya bure. Mtu ambaye ameshapoteza tumaini la kuishi duniani na kisha tunamuweka kuwa kiongozi, tunatarajia nini. Ama anakuwa mume au mke wa mtu, ataweza kweli kumthamini mwenzake? Ama amekuwa mzazi ana watoto kadhaa na unamwambia awalee watoto, atakuelewa kweli wakati yeye mwenyewe anatamani kuondoka. Ndiyo, anatamani kuondoka japo hajasema.

Tunajua kuwa anatamani kuondoka duniani kwa sababu ya tabia zake na vitendo vyake vya kujiua. Hajiui lakini ana tabia na vitendo vya kujiua. Ikiwa anakunywa pombe kiholela tena kila siku anakesha huko kunywa pombe hadi

alfajiri na anaona fahari, huko siko kujiua? Ni dalili kuwa amechoka kukaa duniani. Tunamwona anavyovuta sigara, na madawa ya kulevya; hajasema lakini tabia na vitendo vinaongea.

Ikiwa analala na kila mwanamke au kila mwanaume habagui wala hachagui basi sisi twajua kuwa ameshachoka kuishi duniani na anatamani aondoke. Ameambiwa akibaka au kulawiti atafungwa kifungo cha maisha jela na bado anathubutu kufanya vitendo hivyo kwa hiyo twajua kuwa amechoka kuishi. Anakimbiza sana gari tena hana tahadhari hata katika sehemu za hatari, twajua tu hizo ni dalili kuwa amechoka kukaa duniani. Mwizi, mla rushwa, fisadi; twajua hawezi kututunza sisi walimwengu kwani yeye mwenyewe ameishachoka kuishi humu hivyo haoni umuhimu wa kuifanya dunia kuwa mahali pazuri pa kuishi.

Mtu anapokuwa na moyo mgumu hupoteza mambo makuu matatu;

- Uwezo wa kuhusiana na yeye mwenyewe
- Uwezo wa kuhusiana na watu wengine
- Uwezo wa kuhusiana na Mungu

Anapoteza Imani na tumaini lake kwa Mungu, anashindwa kutumia uwezo wake wa asili alioumbiwa na anaanza kutumaini na kutegemea watu na mazingira.

Mazingira na watu hawakuumbwa kubeba mizigo ya mtu mwingine, hivyo anageuka kuwa tatizo kwa watu wengine. Watu wanaanza kumuona ni tatizo wanamkwepa, wengine wanamuumiza kwa kutotimiza matarajio yake. Hata hivyo

kwa kuwa bado anamahitaji, kuumizwa na kukwepwa na watu hakutamfanya aache kuwategemea watu na hivyo utegemezi wake ndio huongezeka maradufu kadri anavyozidi kuwa muhitaji.

Kama ilivyo kwa yule anayepitia hali ngumu, kwenye elimu utagundua kuwa tuna mifumo ya elimu ambayo haimsaidii mtu kuona uwezo wake wa asili alioumbiwa na Mungu ambao akiutumia na kufanikiwa utamfanya amtukuze. Mifumo ya elimu inamtengenezea mtu utegemezi wa mazingira. Kumuaminisha mtu kuwa ukisoma sana basi utafanikiwa sana. Mtu anasoma sana akishamaliza anagundua hafanikiwi sana anaenda kuongeza elimu zaidi. Asichokijua mtu huyu ni kuwa kadri anavyozidi kuongeza hizo elimu ndivyo utegemezi wake juu ya hiyo elimu unaongezeka na unamfanya anakuwa na moyo mgumu. Anazidi kupotea kabisa mbali na uwezo wake wa asili alioumbwa nao ili kufanikiwa.

Ni uwezo wa asili ndani ya mtu ambao mtu akifanikiwa kuhusiana nao na kuutumia na kufanikiwa humfanya amuelewe na kumuamini Mungu kirahisi. Mifumo ya ulimwengu humuondolea mtu uwezo wa kumwamini Mungu kwa kuwa ni wazi amefanikiwa kwa mazingira na mifumo iliyowekwa na wanadamu. Kama ni mifumo ndio iliyomfanikisha kuna umuhimu gani wa kumtegemea na kumwamini Mungu.

Huyu mtu ambaye kwa sababu ya changamoto nyingi na kutengenezewa utegemezi wa mazingira na mifumo ya duniani, anapoteza uwezo wa kuhusiana na vipawa alivyonavyo na hiyo inamfanya apoteze fursa ya kumjua

Mungu aliyemuumba kwa kuwa anayatafuta mafanikio nje ya asili yake na utegemezi wake kwa mazingira na watu unamuingiza kwenye mtego wa kuwa mzigo kwa watu na kupoteza uwezo wa kuhusiana na watu.

Mtu aliyepoteza uwezo wa kuhusiana na Mungu, uwezo wa kuhusiana na yeye mwenyewe na uwezo wa kuhusiana na watu wengine, anapoteza sifa za kuwa raia wa duniani. Kimsingi anakuwa kiumbe ambaye hapaswi kabisa kuishi duniani. Uwepo wake dunia huiweka dunia katika hatari kubwa. Na hawa ndio aina ya watu ambao wamejaa duniani sasa hivi. Wanafanya matukio ya ajabu ya kuharibu dunia na uumbaji wake, wengine ni wanasiasa wanatunga sera mbovu,

Wengine wanatengeneza silaha za hatari kuua watu, wengine wanaanzisha vita kila kukicha, wengine wanatengeneza virusi vya mgonjwa, vyakula vyenye viambata sumu. Wengine ni wezi, majambazi, wala rushwa, mafisadi. Tunatarajia jema gani kutoka kwao? Tunajidanganya. Kwa nini watende mema wakati wamepoteza uthamani wao tokea zamani. Tunawapa mamlaka na tunatarajia tutakuwa salama. Tunawakabidhi watoto wetu na tunatarajia wawalinde na kuwalea, wasiwanyanyase na kuwafanyia ukatili. Wametoa wapi huo uwezo wa kuwathamini wengine.

Mtu wa namna hii ndio anakuwa mume wa mtu ama mke wa mtu na tunatarajia hakutakuwa na migogoro, unyanyasaji na ukatili. Tunatarajia watavumiliana katika shida na raha. Tunatarajia watazaa watoto na kuwalea katika njia iwapasayo. Tunatarajia hawatatishiana uhai na

pengine kuuana. Na wanapokuja kuomba talaka tunataka kuwazuia wasiachane. Kwa nini wasiachane?

Musa aliliona hili na pengine alijiuliza lakini akajikuta amekosa majibu. Hawawezi kuheshimiana, kuthaminiana, kupendana, kulindana, kufadhiliana, kuhudumiana. Je, hapo tutasema ni Musa amewatenganisha? La Hasha. Hawa kuwaacha pamoja ni sawa na kutafuta kesi ya mauaji. Bado hatuwezi kuhalalisha talaka lakini pia hatuwezi kuhalalisha unyanyasaji wa kijinsia, kifikra, kiuchumi; ukatili na hata mauaji. Mungu anayechukia kuachana ndiye anayeagiza watu wasipigane, kuchukiana na hata kuuana.

Tunapojua kuwa mtu amepoteza kitu kikubwa sana ndani yake kwa hiyo inatakiwa ni aidha kukitafuta kwanza akipate ama akae mbali na nafasi ama mamlaka alizonazo ili wengine wawe salama. Hatuwezi kuona kuwa mtu hana uwezo wa kulinda na kuthamini wenzake lakini tukamkabidhi nafasi ama mamlaka inayompa nguvu ya kuumiza wengine.

Kufanya hivyo ni kumuweka mwingine kwenye hatari ya kupoteza maisha yake. Hapa inatupa kuelekeza nguvu zaidi kwenye kutibu mioyo kuliko kutaka kuwaweka watu pamoja. Akiwa tayari kupona basi atastahili kubaki na wenzake lakini ikiwa hayupo tayari basi ni muhimu kujua kuwa alipoteza sifa za kuchangamana na wenzake muda mrefu, ikiwa yupo kwenye mahusiano basi aliingia kimakosa kwani hakupaswa kuingia tangu mwanzo kwa kuwa sifa hizo hakuwa nazo.

# SURA YA 5

# DALILI ZA MOYO MGUMU

Mpaka sasa pengine unaweza kuwa umeshatishika na suala la moyo mgumu. Swali linaweza kuwa namjuaje mtu mwenye moyo mgumu? Je, ikiwa ni mimi? Nitajitambuaje. Dalili hizi zinaweza kukusaidia kupata mwanga kuhusu hali yako na hali ya wale walio karibu nawe. Lengo halipaswi kuwa wewe kujihukumu ama kuwahukumu na kuwatenga wale ambao inaonekana wazi kuwa wana hali hii ya moyo mgumu bali ni kutafuta suluhuhisho binafsi na kujilinda dhidi yao ili usije ukaishia kuwa muhanga.

Wakati unaendelea kujifunza kuhusu dalili hizi za moyo mgumu kuna mambo ya msingi ni muhimu kuyafahamu,

- *Moyo Mgumu ni matokeo ya hali ngumu mtu aliyopitia ama maarifa makubwa aliyonayo na sio tabia ambayo anafanya makusudi.*

  Kuna mfumo uliomkuza na matukio aliyokutana nayo mtu kwenye maisha yakamfanya akawa hivyo alivyo, hivyo hapaswi kuhukumiwa na kutengwa kwa jinsi alivyo.
  Katika mazingira fulani unaweza kuhisi aidha mtu anafanya kwa makusudi ama anakufanyia vitendo hivyo wewe kwa sababu zake binafsi lakini sio kweli. Katika nafasi yako hiyo hata yeyote ambaye angekuwepo hapo angefanyiwa vitendo hivyo hivyo.

Kama ni unyanyasaji au usaliti au kukuumiza kwa namna yoyote ile ikiwa ni katika mahusiano ya kimapenzi, ndoa ama kazini, tambua kuwa tatizo sio wewe bali ni yeye isipokuwa wewe unakuwa muhanga tu wa tatizo lake na yeye wala hajui kama anakuumiza.

- *Tatizo la Moyo Mgumu huambukiza*

  Ukiishi na mtu mwenye tatizo hili kwa muda mrefu bila kujua na hukuchukua hatua ya kujilinda unaweza kuingia kwenye tatizo hili pia. Mara nyingi watu huwa wanauliza ikiwa tatizo la afya ya akili linaweza kuambukizwa. Hapa unaweza kupata jibu. Ni kweli linaweza kuambukizwa. Mtu mwenye moyo mgumu anaweza kupelekea kukufanya uishi katika hali ngumu kwa sababu ya matendo yake kwa kuwa anakuwa hana namna nzuri ya kuelezea kwa nini anafanya anachofanya ili kukupa uelewe wa kina utakaokusaidia wewe kujilinda badala yake anakuweka kwenye sintofahamu ya kihisia na kifikra na baada ya muda hali ngumu unayopitia inakutengenezea na wewe moyo mgumu. Hivyo kuelewa tu kuwa unaishi na mtu mwenye moyo mgumu itakupa ahueni na kupelekea wewe kujilinda ikiwa ni pamoja na kujua kuwa hafanyi makusudi.

- *Baadhi ya watu wenye mioyo migumu wanaweza tishia uhai wako*

Kuna hali inafikia mtu anaweza kupoteza tumaini la kuishi na wakati mwingine kuwa na hasira na vitendo ambavyo vinaweza kutishia uhai wako. Muhimu kujua kuwa hata wagonjwa huwa na hatua mbalimbali kuanzia homa ya kawaida mpaka wale ambao ni mahututi kabisa. Tunapolitazama suala la Musa kuruhusu talaka ni vyema kujua kuwa sio kila mwenye moyo mgumu amefikia hatua ya kuwa hatari kwa usalama wa mwenzi wake kiasi cha wao kuachana.

Kuna dalili za kawaida kabisa ambazo utaona masumbufu ya kawaida lakini yanaweza kuvumilika na ikiwa utayaelewa basi kuna nafasi pia ya kuweza kumsaidia mtu husika. Hata hivyo wapo wengine ambao uvumilivu wako unaweza kukupatia zawadi ya mauti na watu wa namna hii hatuna budi kukubali kuwa inapaswa kukaa naye mbali kwa usalama wa maisha yako.

Hapa ndipo inaondoka fikra na Imani kuwa talaka ni kitu kiovu. Ukweli ni kuwa talaka ilitumika kama njia mbadala ya kuokoa maisha na uhai wa watu baada ya kuonekana kuwa ni usalama wa mtu upo mashakani kulingana na hali ya moyo wa mwenzi wake.

Ukifikia hatua ukajiridhisha kuwa uhai wako upo mashakani basi ni vyema ukachagua uhai kuliko ndoa. Kumbuka kuwa mtu huyo anatatizo ambalo yamkini hata yeye hajui kuwa analo na ni matokeo ya hali ngumu aliyowahi kupitia nyakati fulani kabla hata hujaja kwenye maisha yake.

Kama Musa alishindwa kutibu hilo tatizo kiasi cha kuruhusu watu kutengana, sisi hatupaswi kudhani kuwa inaweza kuwa kitu rahisi kwetu. Je, hawezi kupona? Anaweza kupona ila hatua ya kwanza ajue kuwa ana tatizo. Kama kwa kujitenga mbali naye itamfanya atambue kuwa ana tatizo basi hiyo yaweza kuwa hatua nzuri ya kuchukua lakini usijaribu kumtengeneza kwa namna unayotaka kwa kuwa uwezekano ni kuwa wewe nawe unaweza kuishia kwenye kuwa na moyo mgumu na mkishakuwa wagonjwa wawili ndani ya nyumba hatari ya kudhuriana ni kubwa zaidi.

- *Ni hatari zaidi mwanaume akiwa na Moyo Mgumu kuliko mwanamke*

Umegundua kuwa kauli ya Yesu kuhusu talaka alikuwa anaongea na wanaume (Mafarisayo) na akasema "Kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu aliwapa ruhusa ya kuwaacha wake zenu". Ni kana kwamba hapa waliokuwa na mioyo migumu ni wanaume pekee lakini pia talaka ilikuwa inatolewa na wanaume kwa wake zao na sio kinyume chake. Ndio ilivyokuwa nyakati hizo ya kuwa mwanamke ndiye aliyekuwa anapewa talaka.
Sasa Je, ni kwamba wanawake hawana mioyo migumu? Hapana. Wanawake pia wana mioyo migumu kwani nao hupitia hali ngumu na huwa na maarifa mengi isipokuwa tu katika muktadha wa kibiblia mwenye mamlaka ni mwanaume na

mwanamke aliagizwa kumtii mwanaume katika mambo yote.
Sasa ikiwa tu mwanamke anaweza kuwa na "utii katika mambo yote" kwa mwanaume, hali ya moyo wake mgumu haiwezi kuwa na athari zozote kwenye mahusiano yake na mwanaume katika familia kwa kuwa hana uhuru wa kuishi vile anavyotaka. Lakini kwa jinsi mambo yalivyobadilika na harakati za kumuwezesha zaidi mwanamke, wamekuwa na uhuru na maamuzi makubwa na maisha yao hata ndani ya ndoa na matokeo yake sasa suala la wao kuwa na mioyo migumu limeanza pia kuathiri mahusiano.
Ninaposema kuwa athari za mwanaume kuwa na moyo mgumu ndio kubwa zaidi unaweza kuhusianisha na matukio mengi ya unyanyasaji na ukatili katika jamii. Mwanaume ndiye anayeonekana kufanya zaidi matendo hayo kuliko mwanamke. Kwa hali ngumu moja wanayopitia mwanamke na mwanaume, mwanaume anakuwa katika hatari ya kuleta madhara makubwa zaidi siku za usoni kuliko mwanamke.

Na kama kuna mahali ambapo dunia ilikosea ni pale ambapo iliona wanaume wanafanya ukandamizaji na unyanyasaji kwa wanawake na badala ya kuwasaidia wanaume waweze kupona dhidi ya moyo mgumu wao wakaenda kuwapa wanawake maarifa. Kilichofanyika hapa ni kuwa wanaume walikuwa na mioyo migumu kutokana na hali ngumu ya mambo waliyopitia ikasababisha

wawanyanyase na kuwafanyia ukatili wanawake (sio kwamba walikuwa na tatizo na wanawake), ulimwengu ukatengeneza dhana ya mfumo dume kana kwamba wanaume walikaa chini wakapanga kuwa sasa waanze kuwanyanyasa wanawake.

Badala ya kutibu tatizo la msingi, ulimwengu ukatengeneza mkakati wa kuwawezesha wanawake kwa kuwapa maarifa makubwa tena yaliyowekwa juu ya msingi wa hali ngumu walizosabishiwa, wanaume nao wakajikuta wamekuwa na moyo mgumu. Sasa tumetengeneza dunia yenye wanaume wenye mioyo migumu kwa sababu ya hali ngumu na wanawake wenye mioyo migumu kwa sababu ya hali ngumu na maarifa mengi. Hawa wawili wanapokutana vita yake sio rahisi kuiamulia. Kila mmoja anamuona mwenzake ni adui yake japokuwa wanaishi pamoja. Mwanaume ana moyo mgumu na mwanamke ana maarifa anathubutu kumtengeneza mwanaume.

## Dalili za Moyo Mgumu

1. *Hali ya kutojiamini na kutoamini watu wengine*

Hii ni hali ya mtu kuishi katika hofu na mashaka ambayo hayana maelezo ya msingi na humkwamisha kufanya mambo mengi ya msingi ya maisha yake. Anatishwa na vitu vya asili ambavyo hana mamlaka ya kuvibadili. Kwa asili kila mwanadamu ameumbiwa hali ya kuogopa hasa pale anapokuwa katika mazingira ya ugenini ama

anapofanya jambo jipya lakini ikiwa hofu hiyo inaua kabisa uwezo wake wa kufikiri na kuchukua hatua basi hiyo ni dalili kuwa ameingia kwenye shida ya kuwa na moyo mgumu. Ataogopa kufanya jambo jipya, ataogopa kusafiri, ataogopa giza, anaweza kuamka usiku akawa anaogopa na mbaya zaidi anaogopa kutengeneza mahusiano na watu kwa kuwa hawaamini watu.

Hofu yake hii inaweza kujidhihirisha kwa kutowaamini watu wengine. Watu tukidhani kuwa hawaamini watu lakini ukweli ni kuwa tatizo halipo kwa watu bali kiini chake kinaanzia kwake. Ikiwa yeye binafsi hana Imani juu ya uwezo wake na nia yake ya kufanya mambo je anawezaje kuwaamini watu wengine. Matokeo yake anakuwa ni mtu ambaye ni mwepesi sana kuumizwa na kukwazwa na watu wengine, pia anakuwa ni mwepesi sana kuhukumu watu kwa mambo ambayo hayana msingi wowote. Kwa sababu ya hofu zake hujikuta kwenye mtego wa kutaka kutawala maisha ya wengine kwa kuwa anataka mambo yaende kwa namna anayotaka yeye ili awe salama na watu wanaanza kumuona anawatawala.

Katika mchakato wa kujinasua wanaishia kumuumiza na kumuongezea tatizo la kutowaamini watu. Hapa ndio utakutana na watu ambao wanataka vitu vifanyike kwa ukamilifu (*perfectionist*), utakutana na watu ambao mara nyingi wanahisi kutosikilizwa, kutoeleweka, wanajitenga na watu, wenye hasira na msongo mawazo, watu ambao wanapenda sana kupendwa na wanaogopa sana kuumizwa.

Muhimu kujua ni kuwa jukumu letu ni kuwaamini watu na jukumu la watu ni kuwa waaminifu. Lazima kila mmoja kubaki katika mpaka wake. Unapoingilia mpaka wa mtu mwingine kuanza kumfundisha namna anavyopaswa kuenenda ili kujilinda wewe hiyo inatafsirika kama kumtawala mtu kinyume na utashi wake.

Mtu binafsi anapaswa ajiimarishe kwenye suala la kuwaamini watu na kuwapa nafasi watu kuishi wanavyoona vyema. Je, watu watakuwa waaminifu kwako? Sio mara zote unaweza kuwa na bahati ya kukutana na watu waaminifu lakini kutokutana na waaminifu haipaswi kukufanya kudhani kuwa waaminifu hawapo.

Baada ya kukutana na watu wengi wasio waaminifu na watakaokuumiza na kukufanyia mambo mabaya lazima ujue dunia imejisazia maelfu ya watu waaminifu watakaokufaa. Unapobaki na hali ngumu ya kuumizwa inakutengenezea moyo mgumu na hivyo wale waaminifu wakija wanakuta tayari moyo wako umeharibika na hivyo na wao pia wanashindwa kufanyika Baraka kwako. Hivyo mwanzo ilikuwa tatizo ni watu wasio waaminifu ndio walikukwamisha ila baada ya hao wakakuachia tatizo ambalo sasa ni wewe mwenyewe unajikwamisha. Habari mbaya ni kuwa Baraka na mafanikio yako yameshikamanishwa na watu. Huwezi kufanikiwa bila watu na ikiwa huwezi kuwaamini basi umefanikiwa kukwamisha mafanikio yao milele.

Tumekuwa na watu wengi nyakati hizi ambao wana ndoto na maono makubwa lakini ukitazama mwenendo wao

dhidi ya watu unaweza ukajua tu kuwa hakuna namna ambayo anaweza kufanikiwa. Kiwango chako cha mafanikio kinategemea uwezo wako wa kufanya kazi na watu. Unaweza kuanza peke yako lakini ili kukua lazima utoe nafasi kwa watu wengine kufanya kazi na wewe. Ikiwa ni kampuni, shirika ama kanisa.

Kiongozi mzuri ni yule ambaye anaweza kuwa na ujasiri wa kuwapa wengine majukumu ya kufanya na mamlaka ya kuamua pia kwa kadri anavyozidi kukua, sasa kama unashindwa kuwaamini watu hauwezi kukua na huwezi kufanikiwa. Hauhitaji kumsingizia shetani kuhusu kutofanikiwa kwako na wala hupaswi kuwalaumu watu. Unapaswa kujifunza kuchagua vyema na ikitokea ukaumizwa uzoeshe moyo wako kuamini tena na tena na tena. Ndio njia ya mafanikio yako na huwezi kujiepusha nayo.

2. *Hali ya kujali zaidi mambo yake (ubinafsi)*

Pale mtu anapoanza kujali mambo yake zaidi kuliko wengine ni dalili ya tatizo la kuwa na moyo mgumu. Apendwe yeye, atafutwe yeye, asikilizwe yeye, aeleweke yeye, atiwe moyo yeye, ajaliwe yeye. Hela apewe yeye, vizuri vyote viwe vyake. Mtu asiyejitafuta kuona anafanya nini kwa ajili ya wengine bali siku zote anaangalia yeye anafanyiwa nini. Mtu wa kupokea asiyejali kuhusu kutoa. Mtu mwenye shauku ya kutendewa mema asiyejali anawatendea vipi wengine.

Hapa ndipo unapokutana na mtu ambaye siku zote huwa analalamikia wenzake, analaumu na kunung’unika jinsi ambavyo anaonewa na kutotendewa sawa na mara nyingi

wengine ndio huwa wanamkosea yeye bali yeye haonagi kosa lake. Ni mwepesi wa kuona kibanzi kwenye jicho la mwingine kuliko boriti katika jicho lake. Ni mtu anayependa kutendewa yale ambayo yeye hawezi kuwatendea wengine. Ni kama mti unaokula matunda yake wenyewe kitu ambacho ni kinyume na kanuni ya uumbaji. Unataka kutendewa je, una nini cha kuwatendea wengine? Unataka kupewa je, unacho cha kutoa? Dunia hii ilitengenezwa kuwapa wanaotoa. Kipimo kile kile unachowapimia wenzako ndicho hutumika kukupimia wewe kwa kiwango cha kujaa, kusukwasukwa hadi kumwagika. Unatoa nini kinachotengeneza kipimo cha wewe kupokea. Sio lazima utoe kama huna lakini hupaswi kutarajia kupewa ikiwa wewe huwezi kutoa. Pale unapoona una kidogo unachotoa na unaumia usipofanyiwa ama unakuwa na mtu ambaye yeye hafanyi ila anaumia sana asipofanyiwa basi tambua kuwa huyo ana moyo mgumu.

3. *Hali ya kulinda hadhi na heshima yake kupita kawaida*

Yupo tayari kusema uongo na kuongea mambo ya kuzushia wengine ili yeye aonekane hana hatia. Mtu asiyejali kuhusu kuwachafua wengine ili yeye aonekane msafi.

- ✓ Mtu ambaye hawezi kuficha uovu wa wengine tena yupo tayari kuongea kwa kila mtu ili kuonekana yeye ni bora zaidi.
- ✓ Mtu ambaye ukiongea uovu na ubaya wake atakuchukia.

- ✓ Mtu ambaye ukijua madhaifu na ubaya wake ni aidha akununue uwe rafiki yake ili usiseme ama uwe adui yake wa kudumu.
- ✓ Watu ambao hawawezi kustahimili ubaya wao kujulikana. Yupo tayari kutumia gharama kubwa kuwafumba watu mdomo na ufahamu wasione ubaya wake.
- ✓ Watu ambao siku zote wanajitahidi kuwa wema machoni pa watu. Maumivu anayoyapata kwa siri zake kujulikana hayavumiliki. Kwao hawa usalama wa moyo sio muhimu kwake bali muhimu kwake ni hadhi na heshima yake machoni mwa watu.
- ✓ Watu ambao ukiishi nao siku zote utaonekana wewe ndio mbaya, una matatizo, mgomvi ila yeye hana shida.
- ✓ Ukitaka kuwa adui yake basi ongea ukweli juu yeye alivyo na utoe siri za maovu na ubaya wake. Na hatimaye unalazimika kuishi kwenye utumwa wa kutoongea mabaya yake ili uwe salama.

Unajikuta nawe pia unaingia kwenye mtego wa kulinda hadhi na heshima yako ili hali unateketeza moyo na utu wako kwani ukifanya maamuzi yoyote yenye tija kwako dunia nzima itakugeuka na kukuona wewe ndio mwenye shida. Hapa ndipo unakuta mtu yupo kwenye mahusiano anafanyiwa unyanyasaji na ukatili wa kila namna lakini anakwambia hawezi kutoka kwa sababu dunia itamwonaje. Amekaa na mtu wenye moyo mgumu kwa muda mrefu mpaka naye amekuwa na moyo mgumu. Mtu anayelinda hadhi na heshima yake atakuweka kwenye mazingira ambayo utajikuta nawe unaanza kujali kuhusu

hadhi na heshima yako kuliko mustakabali mwema wa maisha yako.

Neno la Mungu halituagizi kulinda hadhi na heshima bali kulinda moyo.

***Mithali 4:23*** *"Linda moyo wako kuliko yote ulindayo, maana hapo ndiko zitokako chemchemi za uzima"*

Jukumu tulilopewa ni kulinda moyo sio hadhi na heshima. Kukiwepo hadhi na heshima za kulinda na moyo wa kulinda kwa wakati mmoja basi jukumu lako ni kulinda moyo na sio hadhi na heshima. Mungu ana namna yake ya kusafisha hadhi na heshima zetu. Tunapaswa kuwa makini na mwenendo wetu lakini tusiruhusu mazingira yatulazimishe kulinda hadhi na heshima hata kama mioyo yetu inaangamia. Bila kujali watu watasemaje unapaswa mar azote kuhakikisha moyo wako unakuwa salama. Ikiwa moyo wako utaumizwa sana kwa msingi wa wewe kuhofia watu watakuonaje unajiweka kwenye hatari ya kuwa na moyo mgumu. Kwa namna hiyo hutakuwa unapunguza tatizo bali kuliongeza. Kudhani kuwa kwa kuwapendezesha wanadamu wewe utakuwa salama ni kujidanganya nafsi yako. Ni heri moyo wako uwe salama hata wanadamu wasipokuelewa.

4. *Hali ya kukosa uvumilivu*

Hali ya kushindwa kusubiri wakati na majira sahihi kwa jambo fulani kutokea. Watu ambao hutaka mambo yatokee kwa jinsi wanavyotaka wao, wakati wanaotaka wao na namna wanavyotaka wao. Watu wenye matarajio yao na wanataka dunia nzima ijue na isimame

kuhakikisha wanachokitaka kinakuwa na kisipokuwa ni tatizo kwao na kwa watu wengine. Watu ambao ukimwambia una jambo unataka kumwambia basi umeshamuharibia utulivu wake, siku yake na usingizi wake. Hawezi kusubiri muda muafaka ufike. Ana tahayarika kirahisi sana na kuvurugikiwa kihisia kwa sababu ya matarajio yake. Ni watu ambao hawana subira.

Kukosa uvumilivu ni tabia ambayo inamfanya mtu kujiingiza kwenye hali ngumu zisizo za msingi na tena ambazo zipo nje ya uwezo na mamlaka yake. Anaweza kuumia, kuteseka, kupata msongo mawazo kwa mambo ambayo wala hayakupaswa kumpa shida. Ni namna fulani ya mtu kujiongezea tatizo la moyo mgumu. Watu wasio na uvumilivu hufungua mwanya wa mazingira na watu kuwatengenezea tatizo sugu la moyo mgumu. Ijapokuwa hii ni dalili ya moyo mgumu lakini ni mojawapo ya sababu zinazochochea watu wengi kuingia kwenye tatizo la moyo mgumu. Jifunze kuvumilia, jifunze kusubiri, jifunze kuruhusu mambo yafanyike kwa namna yake sio namna yako, jifunze kuruhusu muda ukamilishe mambo, jifunze kuwapa watu nafasi ya kuishi vile wapendavyo sio vile upendavyo wewe.

5. *Kuwa na majivuno*

Kujisikia bora kuliko wengine kwa sababu ya jinsi ulivyo, akili zako, elimu yako, uzuri wako, hekima yako, upako wako na ujuzi wako wa mambo. Hali ya kujilinganisha na wengine na kuona hawana thamani uliyonayo wewe. Ni kweli hawapo kama wewe lakini nani amekupa wewe mamlaka ya kujipimanisha na wengine. Kila mmoja wetu

anatofautiana na mwenzake. Nani kasema “utofauti” ni “ubora?”. Ulitaka wote wawe kama wewe? Ili iweje. Je, unafahamu kuwa kama wote tungefanana basi dunia ingekuwa mahali hatari sana pakuishi? Je, unafahamu kuwa wewe sio mzuri na wala yule sio mbaya bali ni mtazamo binafsi? Sio kwamba yule hana upako bali wito wenu ni tofauti. Sio kwamba yule hajui mambo ila anajua yale ambayo wewe huyajui. Hilo sio tatizo.

Tunaishi katika nyakati ambazo watu wanajisikia vizuri kwa kujifananisha na wengine. Anajiona ana akili kwa kujilinganisha na wajinga, mwenye hekima kwa kujilinganisha na wapumbavu, mzuri kwa kujilinganisha na wabaya. Huko ni kujivuna. Kila mmoja anapaswa amuhesabu mwingine kuwa ni bora kuliko nafsi yake. Kuheshimu tofauti zetu ni kiwango kikubwa cha ukomavu wa kifikra na kihisia. Hatupaswi kupimana na hatupaswi kuogopana. Kila mmoja ni bora kwa namna yake na anapaswa aishi katika mipaka yake kwa faida ya watu wengine.

6. *Tabia ya kujionyesha uwezo wake*

Kutoka kwenye mtu kujivunia kwa vile alivyo mpaka kwenye kujivunia vile alivyonavyo. Huu ndio utofauti wa dhana hii na dhana ya majivuno. Majivuno ni kujiona bora kwa jinsi mtu alivyo lakini wakati mwingine mtu anaweza asijivunie jinsi alivyo bali akajivunia vile alivyonavyo yaani anavyovimiliki. Kuna wajivuniao jinsi walivyo na wale wajivuniao vile wanavyovimiliki na wale wajivuniao vyote. Wote wanadhihirisha dalili ya moyo mgumu.

Ndani yake inawezekana asijione kuwa yeye ni bora lakini akatumia vile anavyovimiliki kuitafuta thamani na heshima ambayo anatamani kupewa. Hapa ndipo tunapokutana na wale ambao atajionyesha akipendeza, atajionyesha akiwa kwenye sehemu za starehe na kifahari, ataonyesha mali zake na utajiri wake, ataonyesha uzuri wake, uzuri wa mwenzi wake na watoto wake, ataonyesha jinsi alivyofanikiwa kiuchumi, kihuduma, kielimu. Ilimradi tu awafanye wengine wajione duni kuliko yeye na pengine wampe heshima anayodhani anastahili. Hatosheki peke yake mpaka apate msaada wa vile anavyovimiliki.

Hii ni aina ya watu ambao hujishikimanisha na vitu au watu, kwa maana maisha yao, heshima yao na hadhi yao hutegemea vitu na watu hao. Hawa maisha yao sio yao bali yanaendeshwa na vile walivyonavyo. Ukitaka kumuharibia maisha basi mnyang'anye vile anavyovimiliki ambavyo ndivyo humpa ujasiri mbele ya watu. Ujasiri wake hautokei ndani bali hutegemea alivyonavyo. Akivipoteza anaona ni kheri ardhi ipasuke azame ndani maana anahisi kuchekwa na kuzomewa kila mahali. Ndiyo! atahisi kuchekwa na kuzomewa kwa kuwa alivitumainia kumbeba ila peke yake hatoshelezi.

Jipime tu uone ikiwa ukipoteza vyote ulivyonavyo bado utakuwa na ujasiri wa kujiona hivyo unavyojiona. Ukiona unavilinda sana kiasi kwamba upo tayari kudanganya, kutweza utu wako, kufanya mambo ya ajabu ili kuvitunza unavyovimiliki basi ni dalili mojawapo kuwa una shida ya moyo mgumu. Unavitumia kama kinga yako.

7. *Tabia ya kuhesabu mabaya, makosa aliyotendewa*

Hawa ni wale watu wenye bidii ya kutunza kumbukumbu ya kila jambo baya analotendewa. Wanakumbuka mambo mabaya kuliko mema. Ukimfanyia mema litasahaulika haraka sana ila baya litatunzwa. Anahesabu makosa na mabaya uliyomfanyia. Moyo wake una nafasi ya kutosha kukumbuka mpaka makosa ya miaka kumi iliyopita na anajivunia kuwa yeye anakumbukumbu sana ila asichokijua ni kuwa ana tatizo la kuwa na moyo mgumu.

Kutunza makosa na mabaya ni namna nzuri sana ya kuruhusu maisha yako yatawaliwe na kuongozwa na matukio ya jana, hivyo unakosa fursa ya kuishi na kuifurahia leo yako na huwezi kuona uzuri wa kesho yako.

Wakati umri unaenda, fursa nyingi zinakuja, unakutana na watu wengi na mambo mengi yanabadilika; mtu unakuwa umefungwa na matukio yaliyopita tayari. Vilevile mtu huyu huwa anatafsiri watu kutokana na kile walichomfanyia jana na hivyo kukosa tafsiri sahihi ya yale anayotendewa leo. Ni watu ambao wanawakosesha wengine fursa ya kuwa bora machoni pao na hata kujikuta siku zote ni watu wa kujiona ni wakosaji haijalishi watajitahidi kwa kiwango gani.

Jaribu kumfikiria mtu ambaye siku zote anaona ubaya na makosa anayotendewa na watu. Watu wanaishi vipi na mtu huyu. Kwa sababu kwa asilia wanadamu wote hukosea. Na ikiwa najua wazi kuwa makosa yangu yataniingiza kwenye orodha ya watu wabaya wa kudumu moyoni mwako kifuatacho ni kujitenga na wewe. Matokeo yake watu wenye tabia hii ya kuhesabu makosa na mabaya ya watu wengine hujikuta wanazungukwa na watu;

- Waongo watakaojitahidi kukufurahisha
- Wanafiki ambao siku zote hujitahidi wasikosee
- Wakimya kwa maana ya kuogopa kuongea wasikosee
- Wanajifanya wakamilifu kumbe wana mambo ya ajabu

Kimsingi tabia hiyo itakuletea watu wengi wasiofaa na kwa kipindi fulani utaona kama umefanikiwa ila baada ya muda utagundua kuwa watu hao uliojenga tumaini nao sio watu wa kufaa maana walikuwa wanajifanyisha ili tu waishi katika wigo na mipaka ya matarajio yako. Si hutaki kukosewa na hutaki kuona ubaya wao basi watakupa unachotaka na matokeo yake ni kukuumiza wewe.

8. *Hali ya kuumizwa na mafanikio ya wengine*

Unaumia watu wengine hasa wa karibu yako wanapofanikiwa? Tafsiri yake ni kuwa unaona wewe ulistahili zaidi kuliko wao(majivuno) na pengine wao wamechukua kile ambacho ni stahiki yako(ubinafsi). Kwanini kudhani kuwa wasingefanikiwa wao basi ungefanikiwa wewe. Je, huko ni kusema kuwa wamemaliza rasilimali zote ambazo wewe unazihitaji ili kufanikiwa? Ama pengine mafanikio yao yanazuia uwezekano wa wewe kufanikiwa. Ungejisikiaje ikiwa wewe ndo ungekuwa umefanikiwa na wao waumie. Ama pengine unahisi watakudharau, ama pengine unahisi umepoteza rafiki maana ameondoka kwenye viwango vyako na hivyo mazungumzo yenu hayatafanana tena. Utagundua kuwa hii mitazamo yote haina uhusiano na mafanikio ya mtu

bali ni hali ya ndani ya moyo wa mtu ambayo ndio tatizo la moyo mgumu.

Kufurahi pamoja na wanaofurahi ni kiwango kikubwa sana cha ukomavu wa kiroho, kiimani, kififikra na kihisia. Hii anaipata mtu yule mwenye tumaini kuwa naye atafanikiwa kwa namna yake na wakati wake. Mtu mwenye kujua kuwa fursa ya yeye kufanikiwa haiwezi kuzuiwa na mafanikio ya mtu mwingine na wala mafanikio yake hayategemei mtu mwingine. Ikiwa ametangulia kufanikiwa basi ni kwa faida yetu sote. Pengine ni kwa ajili ya kunifanya nikifanikiwa tuzidi kudumu zaidi katika mafanikio yetu sote. Pengine ni kwa faida yangu pia.

Mafanikio ya mtu mwingine hayapaswi kuwa tatizo kwako na ikiwa unaona hilo ni tatizo basi tayari katika moyo wako umeshapoteza tumaini la kufanikiwa. Huoni fursa, huoni kama kuna rasilimali za kutosha na huoni kuwa ipo njia na wakati wako wa kufanikiwa.

9. *Tabia ya kutokuwa na adabu*

Mtu asiyejali mamlaka, asiyetambua mipaka, asiyekuwa na nidhamu. Asiyejali anavaaje, wapi; anaongea nini, na nani, kivipi. Mtu ambaye anajihisi kuwa ana mamlaka na uhuru usio na mipaka. Asiyetambua jinsi ya kuenenda mbele ya watu wengine na mwenye kupuuza tamaduni, mapokeo na mitazamo ya watu.

Katika hali ya kawaida kila mtu ana mipaka ya uhuru wake, kila jamii ina tamaduni na desturi, kuna aliye juu ya mwenzake na chini ya mwenzake. Mtu anapokuwa hajali, haheshimu wala kujizuia jinsi anavyoenenda kwa

msingi wa kuwa ana uhuru wa kufanya na kusema chochote, popote bila kumjali yeyote ni dalili tena hatari sana ya kuwa na moyo mgumu.

Mtoto hawezi kumjibu vyovyote mzazi wake na mzazi hawezi kumwambia chochote mtoto, mke hawezi kumwambia chochote mume na mume hawezi kumwambia chochote tu anachojisikia mke, mtu hawezi kumwambia tu mwenzake anachojisikia kumwambia tena kwa namna anavyojisikia. Hatuwezi kuishi kwenye jamii ambayo watu wanafanya mambo tu wanavyojisikia kwa kuwa wana uhuru wa kufanya. Ni lazima kuwe na nidhamu kwa kila upande.

Uhuru usiwe fursa ya kujifanyia mambo hovyo hovyo. Kwamba mimi "namchana tu sijali", "mimi navaa vyovyote tu watajijua watazamaji". Huko ni kukosa adabu na ni dalili mojawapo kuwa mtu ana shida kwenye moyo. Ukiona huna mwenendo mwema na tabia njema na hujali kabisa watu wanasema nini kuhusu wewe, hustuki na tena una ujasiri wa kuendelea kufanya basi moyo wako una shida. Yesu mwenyewe pamoja na kuwa mtu mkamilifu lakini wakati fulani alijali kuhusu watu kile ambacho watu wanawaza kuhusu yeye na akauliza wanafunzi wake "watu wanasema mimi ni nani?". Kutojali watu wanasemaje kuhusu wewe na kudumu katika mwenendo mbaya ni kuwa na moyo mgumu.

*10. Hali ya kuwa na uchungu*

Kuna jambo au mtu ambaye ukimkumbuka unajisikia maumivu makali sana ndani yako. Ama ni jambo ambalo lilikuumiza sana kwa kupoteza kitu ama mtu

uliyemthamini ama ni jambo ama tukio ulilofanyiwa likaacha kumbukumbu yenye maumivu makali ndani yako. Ikiwa kwa namna yoyote unayo kumbukumbu mbaya ambayo imebeba maumivu ndani yake na umeishikilia basi hii ni dalili mbaya.

Kila mwanadamu hukutana na mambo ya kukwaza katika kipindi fulani cha maisha yako. Makwazo hayana budi kuja. Makwazo yasipofanyiwa kazi huzaa "hasira" na hasira ikikomaa huzaa "uchungu" na uchungu huzaa "chuki na kisasi". Sasa utaona hatua ya "kukwazika" na "hasira" ni za awali ambazo mtu anaweza kujitawala na kurudi katika hali ya kawaida ila inapofikia hatua ya uchungu basi mtu huyu anakuwa ameishapoteza mamlaka juu ya hali hii na inamtawala.

Utashi na maamuzi yake yanaendeshwa na jambo fulani ndani yake. Wakati wowote anaweza kukosa furaha na amani, anaweza kushindwa kujizuia na kuanza kulia, anaweza kupoteza morali wa kufanya chochote anachofanya kutokana na uchungu ndani yake. Mtu huyu huwezi kukisia mwitikio wake kuhusu kile kinachoendelea kwenye maisha yake. Moyo wake umeshaathirika kwa sababu ya matukio fulani ambayo yaliwahi mtokea.

11. Hali ya kukosa tumaini

Huoni mbadala, huoni mlango wala mpenyo wa kutokea kwenye changamoto unayopitia. Baada ya kuachwa na mwenzi wako huoni kama unaweza kupata bora kuliko huyo. Kazi umefukuzwa huoni kama unaweza kupata nyingine nzuri kuliko hiyo. Biashara imekufa, umetapeliwa, umefiwa, umefilisika, umekataliwa; ghafla

unajihisi kufeli kabisa, unajihisi kama maisha yako yamefika mwisho, umekata tamaa kabisa na kuona sasa huna kingine cha ziada unachoweza kufanya.

Utegemezi juu ya mazingira na watu unamuuingiza mtu kwenye mtego mbaya wa kutoona mema pale anapokutana na mabaya. Mazingira na watu wakimsaliti na kushindwa kupata matokeo aliyoyatarajia haoni kama kuna mbadala. Na ukitilia maanani kuwa mazingira ndio yale yale na watu ndio wale wale, kama huyu niliyeona ni bora zaidi amenitenda hivi, kama hii kazi niliyokuwa naiweza zaidi ndio nimeipoteza, kama biashara ambayo niliona ndio bora zaidi imekufa, kama mpenzi aliyenipenda zaidi ndio kanisaliti, kama mwenzi aliyenithamini zaidi ndio kaniacha; kuna kipi cha ziada.

Hapa ndipo tunapokutana na watu ambao wana mawazo ya kujiua. Pia watu hawa mara nyingine huwa hawaoni thamani ya uhai hivyo wanaweza kuwaza kuua wengine. Hapa ndipo unapokutana na mume anamtishia mkewe kuwa nitakuua, ama mke anawaza nitamuuaje mume. Mzazi anawaza tu aue watoto wake naye ajiue. Unapokutana na mtu ana mawazo ama kauli hizi za aidha kutaka kujiua ama kuua mtu mwingine usipuuzie maana yamkini amepoteza tumaini ndani yake na haoni thamani ya maisha yake wala uhai wa mwingine.

Katika hili ndio unakutana na wale ambao haonyeshi wazi kutaka kujiua lakini ana tabia ambazo zina athari mbaya sana kiafya kwake kiasi cha kutishia uhai wake. Anakunywa na kutumia vilevi hovyo bila kujali afya yake, madawa ya kulevya, anatumia vidonge fulani kwa lengo la

kutuliza msongo wa mawazo kwa muda mrefu, anafanya vitendo vya kingono hovyo na watu wa hovyo bila tahadhari yoyote, barabarani anaendesha gari kwa fujo bila tahadhari; yaani kwa ujumla maisha yake yapo katika hatari ya kupotea muda wowote kutokana tu na tabia na mwenendo wake.

Mwingine haonekani kutojali uhai wa watu wengine na kutishia kuua lakini jinsi anavyofanya kazi zake kwa nafasi yake utaona kabisa kiwango chake cha kulinda uhai wa watu waliowekwa kwenye dhamana yake ni kidogo sana. Matokeo yake daktari hospitalini hajali kuhusu namna anavyohudumia wagonjwa wala hashtuki kuona watu wanapoteza maisha, mhandisi hana umakini na namna anavyojenga bila kujali kuwa makosa yake yatagharimu uhai wa mtu, kiongozi haoni shida sera anazoweka kwenye masuala mbalimbali yahusuyo muhstakabali wa taifa bila kujua kuwa kuna watu wataumia, vyakula vinatengenezwa bila kujali athari za kiafya. Watu wanajali Zaidi faida za bidhaa zao.

Hata makanisani kuna watu wanakesha na kuomba Mungu alirudi haraka na wanatamani maisha yao yafupishwe waende mbinguni kupumzika. Umewahi kuona mtu anayeishi maisha mazuri yenye utoshelevu hapa duniani anatamani Yesu arudi haraka ama kutamani aende mbinguni kupumzika? Haya yote ni matokeo ya kukosa tumaini na hujidhihirisha kwa namna tofauti tofauti. Hii ni dalili kuwa tayari mtu ameishakuwa na moyo mgumu.

*12. Hali ya kushindwa kustahimili magumu*

Uwezo wa kustahimili mambo na nyakati ngumu ni ulinzi mkubwa zaidi dhidi ya moyo mgumu. Kila mtu anapaswa kuwa na uwezo wa kujilinda na athari za hali ngumu anayopitia katika kipindi fulani. Pamoja na kwamba hali ngumu ni kipindi hatari kwa mtu na hakipaswi kudumu kwa muda mrefu lakini kila mwanadamu yupo kwenye hatari ya kukumbwa na nyakati hizo kwa namna moja ama nyingine. Ikiwa ni kutokana na matukio fulani, mazingira fulani ama hali fulani. Kwa kuwa tunaishi duniani na mazingira, watu na hali hubadilika na matukio ambayo yapo nje ya uwezo wetu hutokea bila hata taarifa,

Hivyo ni muhimu mtu kuwa na stamina ya kustahimili vipindi hivyo ili kuwa salama. Matharani ni kufeli katika jambo fulani, kufiwa, kuumizwa na mtu uliyemuamini, kunyanyaswa kijinsia ama kingono, kufanyiwa ukatili, kusalitiwa, kutengwa, hali mbaya ya kiuchumi, vita na mauaji, njaa, mambo kutoenda sawa sawa na matarajio yako; nyakati hizi zipo na hakuna mmoja ambaye yupo salama kwa asilimia mia. Chochote kinaweza mtokea yeyote pasipo kutarajia. Swali ni Je! Ameandaliwa kustahimili hali hizi ngumu ili zisiache athari mbaya kwenye moyo wake?

Kuandaliwa? Ndio, nimesema kuandaliwa. Uwezo wa kustahimili magumu ni hulka ambayo mtu anajengewa tangu akiwa mtoto katika safari ya malezi. Jinsi anavyolelewa inaweza kuamua stamina yake katika nyakati ngumu. Kuna watu ni wepesi sana kuumizwa na kukata tamaa kwenye hali ngumu kwa sababu katika maisha yao yote hawakuwahi kuandaliwa kwa ajili ya nyakati hizo. Walidekezwa na kupewa kila walichohitaji

wakati walipohitaji, walilindwa sana kiasi kwamba hawajui kuwa kuna ugumu wa mambo kwa wakati fulani na pindi wanapokutana nao wanashindwa kabisa kuvuka salama.

Katika hili wazazi na walezi wana jukumu kubwa sana la kuhakikisha wanawasaidia watoto wao wasidumbukie kwenye tatizo la kuwa na moyo mgumu kirahisi. Wanatakiwa kuvuka salama pindi wanapokutana na nyakati ngumu. Utulivu wanaoupata wanapokuwa wastahimilivu utapelekea kuweza kupata suluhu za changamoto kirahisi zaidi na hivyo kupelekea wao kuona mlango wa kutokea kwenye hali ngumu mapema zaidi ili wasipate tatizo la kuwa na moyo mgumu.

Hizi ndizo dalili kubwa na za msingi za mtu mwenye moyo mgumu. Ikiwa una moja tu kati ya hizo basi tambua kuwa una moyo mgumu. Tukikubaliana kuwa haujataka kuwa hivyo bali ni mazingira uliyopitia yalikufanya uwe hivyo basi hutakuwa na sababu ya kujisikia vibaya au kujihisi unyonge kwa kuwa na tatizo hili.

Huna sababu ya kujihami ama kujitetea dhidi ya hilo kwa kuwa huna hatia bali wewe umethiriwa tu na mambo fulani. Pia hata mwenzi wako, rafiki yako au jirani yako ambaye unaona wazi kuwa ana dalili hizi basi tambua kuwa sio makusudi bali kuna matukio yaliyotokea yakamfanya hivyo alivyo. Hii inatosha kabisa kutufanya tuweze kuchukuliana na kuishi kwa upendo japo kuna mazingira ambayo yanaweza kuhatarisha maisha yako, ikifikia hali hiyo basi ni vyema kuchukua hatua yenye manufaa kwako.

## SURA YA 6

# UPENDO NA MOYO MGUMU

Unapokuwa na moyo mgumu kitu kikubwa zaidi unachopoteza ni uwezo wa kupenda. Kujipenda mwenyewe, kupenda watu wengine na kumpenda Mungu. Huwezi kusema “unapenda” ikiwa una “dalili za kuwa na moyo mgumu”. Huna uwezo huo wa kupenda. Hicho unachokitafsiri kama upendo, kimsingi sio upendo bali ni vitendo unavyofanya ili upendwe. Kuna utofauti wa maneno haya mawili; “kupenda” na “kufanya ili upendwe”. Upendo ni kutoa sio kupokea. Huwezi kutoa usichokuwa nacho, ukiona unamtendea mtu jambo ili wewe utendewe na usipotendewa unaumia basi huo sio upendo. Anayependa haitaji kupendwa pia ili furaha yake itimie.

Tupo kwenye nyakati ambazo watu wanaamini kuwa wanapenda lakini ukiangalia mwitikio wao dhidi ya wenzi wao utagundua kuwa hawapendi ila walikuwa wanafanya vitendo vya kushawishi ili wao wapendwe. Ikiwa kweli unapenda basi jipime unajisikiaje ikiwa yule unayempenda hakufanyii chochote kinachohusiana na upendo. Yaani wewe unamfanyia kila kitu unachoamini ni upendo lakini yeye hafanyi chochote. Kama bado utadumu kufanya bila kuumia basi hapo kweli unapenda lakini ikiwa furaha yako inatimilika pale wewe unapofanyiwa basi upendo wako unategemea mwitikio wake na hivyo huo sio upendo.

Unaweza ukawa unajiuliza kuwa kuna uhusiano gani baina ya “Upendo” na “Moyo Mgumu”.

Sifa za upendo kupitia neno la Mungu;

***1 WAKORINTHO 13:4-7***..*”Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote, hustahimili yote”*

Kuna nini umekiona kwenye kifungu hiki? Rudia kusoma tena halafu rudi kwenye dalili za kuwa na moyo mgumu, Kuna jambo kubwa utaliona. Dalili za kuwa na moyo mgumu ni kinyume cha sifa za upendo. Soma tena na kisha husianisha kama bado unapata shida basi naomba nikusaidie kuona;

*Upendo huvumilia, huvumilia yote* – ni ile dalili ya “kukosa uvumilivu”. Mwenye upendo huvumilia na hivyo asiyeweza kuvumilia ni kwa sababu ya kuwa na moyo mgumu.

*Upendo hufadhili* – ni ile dalili ya “kulinda hadhi na heshima yake”. Mtu wa jinsi hii hawezi kuficha makosa na ubaya wa wengine ambayo ndio tafsiri ya kufadhili. Upendo humfanya mtu kuficha makosa na ubaya wa wengine bali mwenye moyo mgumu hujilinda yeye na hadhi yake.

*Upendo hautakabari* – ni ile dalili ya “kujionyesha uwezo wake”. Kujiona bora kwa sababu ya vitu na uwezo alionao. Mwenye upendo alivyonavyo sio kitu na wala havimfanyi

kuwa bora zaidi ya wengine bali mwenye moyo mgumu hutumia alivyonavyo kuwadunisha wengine.

*Upendo haujivuni* - ni ile dalili ya "majivuno". Kujiona bora kwa sababu ya jinsi mtu alivyo. Kwenye upendo tabia hii kamwe hautoiona haijalishi mtu yukoje.

*Upendo haukosi kuwa na adabu, haufurahii udhalimu* – Hii utaiona wazi kabisa kwenye dalili za kuwa na moyo mgumu. Udhalimu ni hali ya kufanya makosa halafu unaona ni sawa tu na hakuna kinachokustua, kwa sababu ya kukosa upendo na ugumu wa moyo pekee unaweza kumfanya hivi mwanadamu.

*Hautafuti mambo yake, hauhusudu* – hizi mbili zinazungumzia wivu na tamaa mbaya. Ile dalili ya "kujali mambo yake kuliko wengine". Tamaa inayoweza kufanya aone wengine hawakustahili ila yeye. Ukiwepo upendo hakuna anayekuwa mbinafsi na mwenye tamaa mbaya. Moyo mgumu ndio huleta ubinafsi na tamaa mbaya.

*Hauoni uchungu* – palipo na upendo uchungu huondoka, msamaha na kuachilia ndio huwa na nafasi. Hatufungwi na yaliyotokea jana bali tunatazama yajayo kwa matumaini. Katika moyo mgumu ndipo uchungu hukaa.

*Hauhesabu mabaya* – Hii ipo wazi sana kwenye dalili za moyo mgumu. Ukiwepo upendo hakuna kuhesabu mabaya ya mwingine.

*Huamini yote* - hapa ndipo tunakutana na dalili kutojiamini na kutoamini wengine. Katika upendo hakuna mashaka, hakuna hofu, hakuna kuona wengine kuwa wapo kinyume nawe. Katika upendo tunaamini kila kitu

na tunawapa watu nafasi ya kuwa waaminifu. Kwenye moyo mgumu huwa ni ngumu sana mtu kuamini wengine na hata kujiamini yeye mwenyewe.

*Hustahimili yote* – hakuna kinachoshindikana kustahimiliwa linapokuja suala la upendo. Kutokuwa na uwezo wa kustahimili hali ngumu ni dalili kuwa upendo hakuna ndani ya mtu.

*Hutumaini yote* – katika upendo hakuna kukata tamaa. Hakuna kuwaza kuua wala kujiua. Kila wakati tunaamini kuwa yajayo ni bora zaidi. Tunatumaini kila kitu.

Huwezi kuwa na moyo mgumu na kisha ukasema unampenda mtu. Sio kweli. Kutokana na ukweli huu, wataalamu wamejitahidi kutafuta namna ya kutetea hali hii kwa kuweka aina za upendo lakini ukweli ni kuwa hakuna aina za upendo. Upendo ni upendo. Ikiwa ni mke na mume, mzazi na mtoto, ama rafiki; sifa za upendo ni zile zile hazijawahi kubadilika. Ukizikosa maana yake una moyo mgumu. Mafundisho ya Aina za Upendo ni matokeo tu ya moyo mgumu. Sasa badala ya kutafuta tiba ya tatizo la msingi, wanadamu wakaamua kutengeneza aina za upendo ili kutetea mapungufu yao.

Ukiona unashindwa kuenenda katika upendo kwa misingi ya sifa hizo maana yake moyo wako una shida fulani inayotakiwa kushughulikiwa. Moyo wako ni mgumu, ndio maana unatamani nawe ufanyiwe.

Kumbuka kuwa sifa hizi za upendo zinamuhusu kila mwanadamu. Hivyo kila mmoja anapaswa awe na hizo sifa kwa mwenzake. Sasa pata picha tungekuwa kwenye

ulimwengu ambao kila mmoja ana sifa hizo. Mume kwa mke, mke kwa mume; wazazi kwa mtoto, mtoto kwa wazazi; mtu na mtu; kila mmoja kwa mwenzake. Je! Unafikiri kungekuwa na maumivu, vilio, usaliti, mauaji, kunyanyasana, kuumizana, kuoneana na hata kuachana?

Hapa sasa ndipo tunarudi kwenye kauli ya Yesu kristo, kupitia *Mathayo 19:7-8,*

*“Ni kwa sababu ya kukosa upendo (ugumu wa mioyo), ilimlazimu Musa kuwaruhusu kuwaacha wake zenu”*

Kilichomfanya Musa aandike hati ya talaka ili watu waachane ni kwa sababu “walipoteza kabisa uwezo wa kupendana”. Hawakuweza kupendana, kila mmoja alikuwa anaangalia mambo yake kama matokeo ya kuwa na moyo mgumu.

Kwa wengi tunajua kuwa upendo ni maamuzi lakini mtu anaamuaje kumpenda mtu ikiwa ameshapoteza utawala dhidi ya hisia za moyo wake. Hamuamini, hawezi kumvumilia, hawezi kumfichia makosa yake, ana majivuno, hana adabu, mbinafsi, mwenye uchungu na kuhesabu makosa anayofanyiwa, ameshakata tamaa. Anawezaje kuamua kumpenda mtu ikiwa hisia zake zina ugumu kuliko utashi wake. Hapa ndipo Musa alipokwamia ndipo akafanya maamuzi magumu. Watu walishindwa kabisa kupendana. Sio kwa sababu walikuwa hawataki kupendana bali walikuwa hawawezi kupendana. Uwezo wa kupenda uliuwawa na uwepo wa moyo mgumu.

Kimsingi ili uweze kupenda hupaswi kujitahidi kupenda bali unapaswa upone tatizo la kuwa na moyo mgumu.

Upendo ni hisia za asili. Hazipaswi kutafutwa kwa bidii wala mtu kufanya jitihada za kuzionyesha na kufanya. Hapaswi kutumia nguvu za ziada kupenda watu.

Kupenda ni jambo rahisi sana. Tatizo ni pale tunapotamani kupenda wakati ndani yetu tuna mioyo migumu. Unajikuta kadri unavyozidi kupenda ndivyo unavyozidi kuumiza watu na kujiumiza wewe mwenyewe. Ndivyo unavyozidi kufanya makosa na kuingia kwenye mahusiano mabaya na watu hatari.

Ikiwa umegundua kuwa una tatizo la kuwa na moyo mgumu ni vyema kuacha kwanza harakati za kuwapenda watu na kufanya vitendo vyenye viashiria vya kupenda na uwekeze nguvu zaidi kwenye kupona kwanza moyo kisha urudi kuendelea kupenda. Ukishapona utagundua kuwa ulikuwa unatumia nguvu nyingi sana kufanya jambo ambalo ni la asili sana na haikupaswa ujiumize. Hukupaswa kutumia rasilimali nyingi sana kumthibitishia mtu upendo wako kwa kuwa ndani yako una uhakika mwingi sana na kile unachojisikia kuhusu mtu huyo.

Je! Inapaswa watu ndio waseme kuwa tunawapenda au sisi tunapaswa kujua kuwa tunawapenda? Wewe unayependa unapaswa kuwa na uhakika na kile unachojisikia hata kama mwingine hatoamini. Ikiwa wewe mwenyewe huna uhakika basi kuna uwezekano ukatumia nguvu, mbinu na rasilimali nyingi kumuonyesha mtu unampenda. Kama unampenda mtu na ameshindwa kuamini basi haiwezi kukumiza kwa kuwa wewe una uhakika na hilo. Ikibidi kumuacha aende mbali nawe

itakuwa ni sawa pia maana “upendo hauangalii mambo yake”.

Hauwezi kusema unampenda mtu ambaye miaka mingi ameshindwa kuamini kuwa unampenda na wewe unang’ang’ania kuwa naye. Hapo mmekutana watu wawili wenye mioyo migumu. Yeye “haamini kuhusu upendo wako” na wewe “unaangalia mambo yako”. Mkioana kwa kulazimisha, hiyo ndoa lazima italeta shida. Kama unampenda utamuacha aende kwa kuwa “una tumaini” utampata mwingine bora zaidi. Pengine unamng’ang’ania kwa sababu “huwezi kustahimili” kukataliwa. Unaona mlolongo wa athari za moyo mgumu unavyofanya kazi ndani ya mtu? Ni hatari sana kiasi kwamba tunaumizana wenyewe kwa wenyewe bila kujua.

Tukiwa katika kujitahidi kupendana tunajikuta tunaumizana. Katika jitihada za kuboresha mahusiano, tunajikuta tunayaharibu zaidi. Katika jitihada za kuwalinda wenzi wetu, tunajikuta ndo tunawaumiza. Jitihada ya kuonyesha upendo, tunaonekana tunajipendekeza. Jitihada za kupata mtu sahihi, tunajikuta kwenye mahusiano na watu hatari kuliko tulipotoka. Ni kama vile jitihada zetu zinatuponza na kutuingiza kwenye tatizo zaidi.

Ni kweli kabisa, kujitahidi kutatua tatizo kwa lililosababishwa na utegemezi wako wa mazingira na watu kwa kuyategemea mazingira na watu hao hao waliolitengeneza tatizo hilo ni jambo lisilowezekana. Huwezi kutibu tatizo kwa kutumia kile kilicholitengeneza.

Ni busara zaidi kujiweka mbali na mahusiano na kuvunja uhusiano wako na mazingira kisha utafute tiba kwanza.

Hatua kubwa na ya msingi ili kupona moyo mgumu ni kujitenga na mazingira na watu kisha kutengeneza mfumo wa kuishi kwa kujitegemea mwenyewe na kutatua matatizo yako binafsi. Kuanzia hapo tunaweza kupata suluhu la kudumu. Pale ambapo hutakuwa na mtu ama mazingira ya kuyalaumu kwa changamoto unazopitia na kukubali kuzikabili changamoto zako binafsi.

## SURA YA 7

# VIASHIRIA KWENYE JAMII

Tunaitambua vipi jamii ya watu wenye moyo mgumu? Mkusanyiko wa watu wengi wenye moyo mgumu katika jamii upelekea kuwepo kwa jamii ya namna fulani. Baada ya kuona dalili ya mtu mmoja mmoja ni muhimu kujua taswira ya nje ya jamii ya watu wenye moyo mgumu. Uonapo moja kati ya hivi viashiria basi tambua kuwa jamii hiyo imeshavamiwa na tatizo la watu wengi kuwa na moyo mgumu.

Tunapozungumzia jamii maana yake ni mkusanyiko, hivyo kusema kuwa uonapo hivi viashiria basi tatizo hilo limeshakuwa sugu miongoni mwa watu katika jamii husika. Viashiria hivi ni ishara kuwa tatizo limeshafika hatua mbaya na idadi kubwa sana ya watu wanaosumbuliwa na tatizo hili. Viashiria hivi ni kama vile;

1. Kushamiri kwa huduma za kinabii
2. Watu kujivunia maarifa
3. Ugumu wa watu kuwasiliana

Angalia anachokisema kwenye mstari huu wa nane baada ya zile sifa nane za upendo

***1 WAKORINTHO 13:8****…"Upendo haupungui neno wakati wowote; bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika. "*

Pale ambapo kuna upendo mambo haya matatu hukoma. Pale palipo na mioyo migumu mambo haya matatu huchanua na kushamiri sana.

*KUSHAMIRI HUDUMA YA KINABII*

Unachopaswa kujua ni kuwa moyo mgumu hupelekea Mungu kukosa utawala ndani ya mioyo ya watu na mara zote Mungu anapokosa utawala na nafasi ndani ya mioyo ya watu hutumia zaidi huduma za kinabii. Huduma za kinabii hutumika zaidi mahali ambapo Mungu amekosa kabisa utawala na nafasi kwenye mioyo ya watu. Kuna mitazamo isiyo sahihi kuwa huduma ya kinabii haipo kwenye agano jipya lakini tunaona wazi kuwa katika huduma tano katika mwili wa Kristo na manabii wapo. Unachopaswa kujua ni kuwa unapoona mahali kuna manabii wengi ujue hali ya mioyo ya watu ni mbaya. Mungu anaongea na watu kutokea nje sio kutokea ndani ya mioyo yao. Sheria yake haipo mioyoni mwao na hivyo anainuliwa mmoja wa kuzungumza nao kutokea nje.

Hapa utaelewa kwa nini nabii wa kwanza kwenye historia ya biblia alikuwa ni "Musa" na ndio wakati wa huyu Musa tulikutana na suala la mioyo migumu kwenye taifa la Mungu. Musa alikuwa nabii kwa sababu ya ugumu wa mioyo ya watu. Ugumu huu ndio ulipelekea atumike kama nabii wa Mungu. Watu hawakuwa na Mungu mioyoni mwao, hawakuwa na Imani na hawakuwa wanamcha Mungu.

Baada ya Musa, Mungu alipowaua watu wote waliotoka Misri hatuoni Joshua kupewa jina la kinabii na wala hatukutani tena na nabii katika kipindi cha miaka mingi

mpaka wakati wa mwamuzi wa mwisho Samweli. Huyu Samweli ambaye alikuwa mwamuzi ndiye aliyekuwa pia na cheo cha kinabii. Katika namna nyingine huwa anaitwa "Nabii Samweli" pamoja na kwamba alikuwa pia kwenye orodha ya waamuzi. Kwa nini Yeye alikuwa na hadhi ya nabii? Jibu utalipata hapa kwenye mstari huu

***1 SAMWELI 8:5-7****…"Wakamwambia, Angalia, wewe umekuwa mzee, na wanao hawaendi katika njia zako; basi tufanyie mfalme atuamue, mfano wa mataifa yote. Lakini neno hilo likawa baya machoni pa Samweli akamwomba BWANA. BWANA akamwambia Samweli, isikilize sauti ya watu awa katika kila neno watakalokuambia; kwa maana hawakukukataa wewe, bali wamenikataa mimi, ili nisiwe mfalme juu yao."*

Katika kipindi cha waamuzi tunakutana tu na nyakati ambazo, baada ya watu wa Mungu kufanya uovu, Mungu alikuwa akiruhusu watu wake kuingia kwenye mikono ya watesi ili waweze kumrudia yeye kisha anainua mwamuzi wa kuwaamulia dhidi ya watesi wao, wakishatubu uovu wao; baadhi ya falme zilizowatawala Israeli na waamuzi wao kwenye mabano; Wamesopotamia (waliamuliwa na Othnieli), Wamoabu (Waliamuliwa na Ehudi), Wamidiani (waliamuliwa na Gideoni), Wakanani (waliamuliwa na Debora), Waamoni (waliamuliwa na Yeftha), wafilisti (waliamuliwa na Samsoni).

Katika kipindi hiki chote wana wa Israeli walikuwa hawajamkataa Mungu mioyoni mwao bali walikuwa wanaenda katika njia za mataifa yaani kufanya uovu na ilikuwa kuna urahisi fulani wa kuwarejesha baada ya

kupitia kipindi fulani cha mateso. Ilipofikia hatua ya wao kusema wazi "wanataka mfalme awatawale kama mataifa mengine" hiyo ilikuwa ni ujumbe kuwa "mioyo yao imemkataa Mungu rasmi na hawamtaki". Hii ndio maana Samweli akageuka kutoka kuwa muamuzi na kuwa nabii.

Utagundua pia kuanzia wakati huu ndipo tunaanza kuona manabii wakiwa kazini kuanzia wakati wa mfalme Sauli mpaka nabii wa mwisho Malaki. Wana wa Israeli walipotangaza kutomtaka Mungu ndipo manabii wakashamiri zaidi na huduma hii ikadumu mpaka alipokuja Yesu. Hatukuona wakati wowote huduma hii kupotea kwani watu bado hawakuwa wamerejeza mioyo yao kwa Mungu, mpaka Mungu alipoamua kumleta mwana wake kutuokoa.

Wokovu tafsiri yake ni Mungu kuingia ndani ya moyo wa mwanadamu na akishaingia kusudi lake ni kuondoa moyo mgumu. Kusudi hili likitimia mwanadamu haitaji tena kuishi kwa kutumia unabii. Nimesema kusudi kutimia kwa kuwa kumpokea Kristo moyoni pasipo kuijua kweli kunaweza kusiondoe moyo mgumu ndio maana tuna watu wengi wanasema wamempokea Kristo kuwa Bwana na mwokozi lakini wanaishi kwa kutegemea kutolewa unabii. Hii ni dalili kuwa bado Mungu hajapata nafasi moyoni.

Unapoona watu wanatamani kuishi kwa unabii ni dalili kuwa hawana Mungu ndani ya mioyo yao. Mungu akiingia ndani ya mtu unabii unakosa nguvu maana nabii anayatoa yaliyo ya Mungu na Mungu anakaa ndani yako. Sasa kama Mungu anayemtuma nabii anakaa ndani ya

mtu, mtu anahitaji unabii ili iweje? Ndio maana katika mstari hapo juu anasema;

“Upendo ukiwepo unabii hukoma”

Maisha ya mtu mwenye Mungu ndani yake na anayeishi katika upendo, kwa kuwa Mungu ni pendo, haitaji unabii na hawezi kutegemea unabii. Unabii ni kwa ajili ya watu wasio na Mungu ndani yao ambao Mungu anaongea nao kutokea nje na sio kutokea ndani ya mioyo yao.

Tukisema kuwa katika agano jipya hakuna manabii ama huduma ya kinabii, huko ni kusema kuwa hakuna watu wenye mioyo migumu, kitu ambacho sio kweli. Watu wenye mioyo migumu hata sasa wapo na hao wanahitaji unabii ili kumsikia Mungu. Swali la msingi ni je! Manabii wa nyakati hizi wanafanya wajibu wao huu wa kuwaonya na kuwakemea watu kuhusu uovu wao kama ilivyokusudiwa kuwa nabii awe?

Huduma ya kinabii ni huduma nzuri ila inabeba taarifa mbaya. Tunapoona huduma hii imeshamiri kwenye jamii fulani basi ni ujumbe kuwa watu wa kwenye jamii hiyo wamekithiri kwenye tatizo la ugumu wa mioyo. Sio huduma ya kuisheherekea sana kwa kuwa inaonyesha vile ambavyo huduma za kitume, uchungaji, uinjilisti na ualimu zimefeli kufanya wajibu wao wa msingi wa kufundisha watu na kuwafanya kuwa wanafunzi wa Yesu.

Ukiangalia vizuri utagundua huduma za kinabii zimekithiri na kushamiri zaidi kwenye nchi na jamii ambazo watu wanaishi maisha duni, ya shida, mateso, njaa, vita, maradhi, kukata tamaa na maumivu mengi.

Kwa nini huduma hizo zimeshamiri zaidi barani Afrika kuliko ulaya? Unaweza kuhusianisha uwepo wa huduma hizi na ugumu wa maisha? Angalia vyema takwimu utaona wazi kuwa penye shida na hali ngumu ya maisha ndipo kuna manabii wengi. Hivyo utaona kumbe si kwamba unabii unaendana na moyo mgumu tu bali moyo mgumu uliotokana na shida na hali ngumu. kana kwamba hali ngumu wanazopitia watu huvutia huduma za kinabii ila ukweli ni kuwa kinacholeta manabii ni ugumu wa mioyo uliosababishwa na hali ngumu za maisha watu wanazopitia. Hivyo tukitaka kufanya huduma za kinabii kutokuwepo ni lazima tuhakikishe mioyo ya watu inalainika kabisa na kumrudia Mungu.

*WATU KUJIVUNIA MAARIFA*

Jamii ambayo watu wanaheshimiana na kusikilizana kwa kuangalia wewe ni nani, umesomea nini, umesomea wapi, una kiwango gani cha elimu, una uzoefu wa miaka mingapi kwenye fani ipi. Jamii ambayo kama mtu hana elimu ya kimfumo hawezi kusikilizwa kwa kuwa wote tumekuwa tegemezi wa mfumo wa elimu fulani. Jamii isiyokaribisha jambo na mawazo mapya kwa kuwa tumeaminishwa kuwaza kwa namna fulani, kiasi kwamba watu wanalazimika kutumia miaka mingi darasani kutafuta elimu ili waweze kusikilizwa na kupewa heshima fulani.

Tusichokijua kuhusu elimu ya ulimwengu huu ni kuwa inatupa maarifa ambayo yanatufanya tunakuwa tegemezi wa mazingira yetu wenyewe na tunashindwa kuona zaidi ya mazingira hayo. Mungu alipotuumba alitupa uwezo wa kuona zaidi ya mazingira na elimu inatufanya tuwe na

ukomo wa kuona. Sio vibaya kusoma, hata mimi nimesoma lakini pale tunaporuhusu elimu na maarifa ya dunia yatufungie uwezekano wa kuliishi kusudi la Mungu na kufikia hatima ya maisha yetu basi elimu zetu zimeshatupa maarifa yaliyotufanya kuwa na mioyo migumu. Maarifa ambayo yameua uwezo wa asili ndani yetu kiasi kwamba Mungu hawezi kututumia kwa jinsi alivyokusudi.

Ikiwa ni elimu ya mfumo wa dunia ama elimu ya kibiblia, kama inakuzuia kuona uwezo wa asili ndani yako basi tayari imekufanya kuwa na moyo mgumu. Wapo waliosoma thiolojia na zikaua wito wao. Thiolojia zikawafanya wakawa na mioyo migumu kwa kuwa hakuna tena nafasi ya ufunuo wa Roho Mtakatifu.

Soma elimu zote na pata maarifa yote lakini usiruhusu elimu na maarifa hayo yakufunge fikra na ufahamu wako na kukujaza hofu ya kufanya zaidi ya kile ulichosoma. Wewe ni zaidi ya taaluma uliyonayo. Niliwahi kujiambia mimi ni zaidi ya taaluma yangu ya uhandisi wa umeme na baada ya hapo nikagundua kuwa mimi ni mzuri kwenye saikolojia kuliko kwenye uhandisi. Ningeweza kuruhusu maarifa yangu ya uhandisi yanifanye kuwa na moyo mgumu na matokeo yake dunia nzima ingekosa fursa ya kusoma kitabu hiki.

Jaribu kuwaza ni mambo mangapi umeshindwa kuyafanya kwa sababu ya kuweka tumaini na utegemezi wako kwenye elimu na maarifa uliyopata kwenye mifumo ya ulimwengu. Ni vitabu vingapi havijaandikwa, nyimbo ngapi hazijatungwa, makampuni na mashirika mangapi

yameuwawa ndani ya watu kwa sababu tu ya maarifa waliyopata yaliyowaaminishwa kuwa wao ni kile walichosomea.

Kwa sasa ugomvi mkubwa ni vyeti vya elimu zetu na historia ya nini tumesoma. Watu wanatupima kwa hivyo ili kutupa nafasi ya kutusikiliza. Hiyo ndio jamii ambayo tunaishi ya kwamba ukiongea nje ya kilichoandikwa kwenye vitabu watu wanaona hicho sio sawa. Ukiwa na mawazo nje ya kile kilichowekwa kwenye mfumo wa elimu unaonekana unakosea. Tunatarajia kuleta mabadiliko kwa kutumia maarifa yaliyoleta matatizo tuliyonayo. Nani anaweza kuwa na ujasiri wa kwenda kinyume na maarifa yaliyopo vitabuni ili kuiboresha dunia.

Inasikitisha kuona kuwa asilimia kubwa ya watu waliofanikiwa duniani katika Nyanja nyingi kuanzia uchumi, siasa, afya, elimu na hata teknolojia ni wale ambao walienda kinyume na kile kilichoandikwa kwenye vitabu. Je! Hiyo haitoshi kutufundisha kuwa sisi ni zaidi ya taaluma tunazopata kwenye vitabu? Pengine kuna haja ya kuanza kuongeza jitihada za makusudi kupingana na mifumo iliyotulea na kutukuza.

Tatizo la ajira ni kubwa lakini vijana bado wanaamini kuwa ni maarifa wanayopata shule yatawapa ajira. Tatizo la uchumi linaongezeka lakini tunaamini kuwa ni maarifa pekee ya taaluma tuliyonayo yanaweza kutatua tatizo hili. Changamoto za kimaadili ni kubwa na tunaamini kuwa ni maarifa ya saikolojia tunazosoma darasani pekee zinaweza kutusaidia. Changamoto za njaa, ukame, umasikini, maradhi zinaongezeka na bado tunafikra kuwa maarifa ya

taaluma pekee yanatosha. Changamoto ya afya ya akili na magonjwa ya akili yanazidi kukomaa na tunafikiri ni taaluma pekee zinaweza kusuluhisha.

Tunashuhudia unyanyasaji wa kijinsia, kingono na kimwili kwa wanawake na watoto wa kike na wa kiume unazidi kuongezeka maradufu, matendo ya kikatili na mauaji yanazidi kushamiri, bado tunaamini tu maarifa ya taaluma zetu yanatosha. Watu hawana muda wa ibada wala kwenda kwenye nyumba za ibada, idadi ya vijana huko inapungua na hata waliopo ni kama wanakamilisha tu ratiba na bado wachungaji na viongozi wa dini tunaamini kuwa ni maarifa tu ya thiolojia yanatosha kuleta suluhu. Huu sasa ndio moyo mgumu utokanao na maarifa ya taaluma. Mioyo na fikra za watu hazipo tayari kuwaza nje ya boksi. Tunafanya mambo yale yale kwa njia ile ile na tunatarajia matokeo tofauti.

Ni wakati sasa wa kuondokana na moyo mgumu wa maarifa na kuanza kuona zaidi ya hapo. Paulo mtume anasema;

“Ukiwepo upendo, maarifa hukoma”

Haijalishi watu watakuwa na maarifa kiasi gani lakini hayatawazuia kuwa wabunifu, kuwaza zaidi ya mifumo, kuenda kinyume na mifumo ya taaluma. Watu watamsikiliza Mungu na kupata majibu ya changamoto zao bila kujali shahada zao za uzamili na uzamifu na hata uprofesa. Hatutajali ubobezi na uzoefu bali kila mmoja atajifunza kumsikiliza mwingine kwa umakini kwa kuwa Mungu hana upendeleo na anaweza kumtumia yeyote

ikiwa ni msomi au mjinga, bwana ama mtumwa, tajiri au masikini, shemasi ama askofu.

Kutumia maarifa kama wigo wa kupata heshima ndio hupelekea watu kuwa na vyeo na hadhi nyingi nyuma ya majina yao. Hakuna ubaya lakini huwa tu nawaza kwa nini Yesu hakuwa na hadhi na cheo chochote nyuma ya jina lake? Kwa nini ilitosha tu yeye kujiita "Yesu Kristo". Pengine labda hakusoma sana elimu ya dunia hii lakini kuna wakati walimuita "rabi" na wakati mwingine "mwalimu mwema" na mara zote aliwaonya wasitumie majina hayo. Angeweza pia kujiita mtume, nabii, mchungaji, mwinjilisti au mwalimu. Alikuwa vyote hivyo kwa wakati mmoja na alifanya vyema kuliko wote waliokuja nyuma yake lakini kwa nini alichagua kubaki na jina lake pekee?

Kwa nini sisi tunapambana na hadhi nyuma ya majina yetu? Huyu *"Prof",* huyu "*Dr*" na mwingine "Rev" (mchungaji), na "Askofu", "mtume", "nabii" na mwingine *"ev" (*mwinjilisti). Wapo wale wa *"Eng"* (mhandisi) na wengine wa *"Hon" (*muheshimiwa). Nitakwambia kwa nini wanajiita hivyo, ni kwa sababu ya ugumu wa mioyo ya watu, hivyo hizo ni hadhi na vyeo nyuma ya majina ndivyo vinasaidia wao kutuheshimu na kutusikiliza, hivyo hatuna budi kuviweka. Pindi watu wakipona mioyo utagundua kuwa hivyo vyote havitakuwa na umuhimu maana watu hawatakuwa wanakusikiliza kwa sababu ya hadhi na cheo chako bali kwa kuwa ndani yako lipo suluhisho la matatizo yao bila kujali cheo na elimu yako. Hivi vyeo na hadhi vimepelekea wasio na suluhu ya matatizo kupewa heshima na kusikilizwa zaidi kuliko wale wenye uwezo wa kusaidia

watu. Vile moyo mgumu unavyoweza kuwadanganya watu hadi kuwapa nafasi watu wasio na msaada wowote kwao ila tu kwa sababu wana hadhi, cheo na uzoefu fulani kwenye maisha.

## UGUMU WA WATU KUWASILIANA

Mgongano wa lugha. Watu huongea lugha moja lakini hushindwa kuwasiliana. Mke na mume nyumba moja lakini hawawezi kufungua mioyo na vinywa vyao kuongea yaliyo moyoni. Ukimya unatawala na kila mmoja anapofungua kinywa kunena basi hamuachi mwingine salama na anaweza kuambulia maumivu. Tunafanana lugha lakini namna tunavyowasiliana ni kama tunaongea lugha tofauti. Hatukubaliani, hatuafikiani, hatuelewani. Fikra zetu na mawazo yetu na mitazamo yetu imefarakana na hakuna mahali ambapo tunakutana.

Tunaelewa kuwa ulimwengu bila mawasiliano haiwezekani kwenda. Mahusiano bila mawasiliano ni vigumu kufika salama. Tunajua tunapaswa kuwasiliana na tunajua umuhimu wa mawasiliano ila tusichokijua ni kuwa tunaongea lugha tofauti sana. Tupo pamoja ila tunatofautiana agenda na nia za mioyo yetu. Tupo kwenye ndoa lakini kila mmoja ana nia yake tofauti ya kuwepo hapo na aliingia akiwa na mipango yake, kampuni moja lakini kila mmoja ana agenda yake, biashara moja lakini kila mmoja ana nia yake, kanisa moja ila kila mmoja ana nia yake, nchi moja na serikali moja ila kila mmoja ana jambo lake. Lugha zetu zinagongana kwa kuwa nia za mioyo yetu zinapishana sana.

Ukirudi kwenye dalili za moyo mgumu utagundua kwa nini lugha zetu zinapishana sana. Kwa nini tunashindwa kuelewana na kwa nini mawasiliano ni jambo gumu sana. Biblia inasema;

“Kwenye upendo, zikiwepo lugha, zitabatilika”

Moyo mgumu ukipona kila mmoja ataelewana na mwenzake na atamuelewa mwenzake. Tutania mamoja na kujenga familia, mashirika, makampuni na hata nchi. Tunazungumzia uzalendo. Haiwezekani kukawa na uzalendo kwenye nchi ikiwa watu wana mioyo migumu. Kupona moyo mgumu itawafanya watu wawe wazalendo bila kushurutishwa. Watatii sheria bila shuruti. Tutaondoa mafisadi na wala rushwa. Hakutakuwa na wahujumu wa uchumi. Nje ya hapo tutakuwa tunapiga kampeni isiyo na tija na hakuna atakayeelewa lugha hizi.

## SURA YA 8

# MFUMO WA MAISHA

Mungu alipomuumba mwanadamu kulikuwa na mfumo ambao aliutengeneza ili mwanadamu aishi na kufanikiwa ndani ya mfumo huo. Mungu aliandaa mazingira na rasilimali zote ambazo mwanadamu anazihitaji awapo duniani kabla hajamleta duniani. Mungu kamwe hamleti mwanadamu kabla hajamuandalia mazingira bora na rasilimali anazohitaji ili aishi.

Awali nilisema kuwa mwanadamu hakuumbiwa uwezo wa kuishi katika hali na mazingira magumu. Huu ndio msingi wa dhana hii, kwamba Mungu huandaa mazingira bora na mazuri na kila rasilimali kwa ajili ya mwanadamu kuishi kwa amani na furaha. Hivyo basi kamwe haikukusudiwa mwanadamu aishi maisha ya shida na hali ngumu kwa asili hakuwa amejengewa uwezo huo maana ni nje na mpango wa Mungu.

Maisha ya shida na hali ngumu ilikuwa ni matokeo ya mwanadamu kutoka nje ya mpango wa Mungu kinyume na matarajio na maagizo ya Mungu. Na kama ilikuwa kinyume na maagizo na matarajio ya Mungu basi ni wazi kuwa kusingekuwa na uwezekano wa wao kupewa uwezo wa kukabiliana na hali ngumu maana kwa kufanya hivyo ni sawa na kwamba Mungu alitarajia kuwa wanadamu wangeenda kinyume na mpango wake.

Kilichotokea kwenye bustani ya Edeni ni kuwa kabla ya kuumba mtu, Mungu aliandaa mazingira ya kuishi mtu

huyo kwa furaha na amani. Katika bustani kulikuwa na kila alichokihitaji mwanadamu. Hii ilifanya maisha yake yategemee kile ambacho Mungu alikuwa amekiandaa kwa ajili yake na sio kutegemea mfumo mwingine nje ya kile kilichoandaliwa na Mungu. Mwanadamu, ndani ya Edeni, hakuwa na mbadala zaidi ya kutegemea rasilimali ambazo zilikuwa zimeandaliwa na Mungu. Amani, furaha, chakula na kila alichohitaji kwa ajili ya maisha yake kilitokana na mazingira na mfumo ambao Mungu alikuwa ameutengeneza kwa ajili yake.

Nyoka alipomdanganya mwanadamu kimsingi alimtambulisha mwanadamu kwenye mfumo mwingine wa kuishi kwa kutegemea mazingira nje ya mfumo wa Mungu. Na mwanadamu alipoondolewa bustanini ndio ukawa mwanzo wa maisha yake kutegemea mfumo mwingine ili kuishi maisha yake. Hivyo basi hapa tunakutana na Mfumo halisi wa Mungu ambao kila mwanadamu aliumbwa atumie huo kuishi awapo hapa duniani na Mfumo Feki (wa shetani) ambao shetani huanza kuutambulisha na kufanya kila jitihada mwanadamu autegemee huo awapo hapa duniani. Ni vita inayopiganwa baina ya Mungu na shetani kuhusu mfumo utakaoendesha maisha ya mtu. Ama ategemee mfumo alioandaliwa na Mungu ama ategemee mfumo ambao shetani ameutengeneza humu duniani.

Muhimu kujua kuwa baraka za Mungu ni matokeo ya mwanadamu kuishi katika mfumo ambao uliandaliwa na Mungu kwa ajili yake. Nje ya mfumo huo hakuna kiwango cha maombi, kufunga, kuvunja laana, kiwango cha sadaka, kuhudhuria ibada, bidii ya huduma na uaminifu na jitihada za kazi; kinaweza kufungua baraka za Mungu. Hizi hufata mfumo na sio jitihada za mtu. Kile

alichokifanya Mungu cha kuandaa mazingira kwanza kisha kumleta mwanadamu katika bustani kinadumu hata sasa na hivyo huwezi kunufaika na vya bustanini ikiwa upo nje ya bustani.

Kila mwanadamu huzaliwa kwa kusudi fulani na hivyo Mungu huandaa kila rasilimali ambazo anazihitaji mtu ili aweze kuliishi kusudi hilo. Mungu huweka tayari kila kitu ambacho mtu anakihitaji kufanikisha kusudi la kuumbwa kwake ndipo humleta duniani. Tatizo ni kuwa anapofika duniani, mwanadamu hukutana na mifumo ambayo inamtoa kwenye mfumo wa asili ambao anapaswa kuuishi. Kuanzia kwenye malezi, makuzi, elimu, kazi, mahusiano hadi ndoa kote anakutana na fikra, mitazamo, mawazo na mafundisho ambayo kwa pamoja yanamtoa kabisa kwenye mfumo ulioandaliwa yeye auishi badala yake anaanza kuishi kwa kutegemea mifumo iliyopo hapa duniani. kazi kubwa inayokuwepo kwake ni kuanza kujitafuta na kuishinda nguvu ya mfumo huu wa duniani uliowekezwa kuanzia akiwa mdogo na kumfanya aamini mfumo huo. Na mfumo huu wa duniani, kwa kuwa sasa ameanza kuutegemea, unakuwa na nguvu ya kumfanikisha ama kumfelisha, kumpa amani ama huzuni, kumpa kilio ama furaha. Kwa vyovyote vile kufanikiwa kwake sasa hakumtegemei Mungu na mfumo aliotengeneza kwa ajili ya mtu bali kunategemea shetani na mfumo aliotengeneza hapa duniani.

Hapa ndipo kuna kile kitendawili cha “wana wa ulimwengu huu wanaonekana wenye hekima na wanafanikiwa zaidi kuliko wale wanaomcha Mungu”. Ndio wanamcha Mungu lakini wanaishi ndani ya mfumo wa dunia hii na wanautegemea mfumo huo kwa habari ya kufanikiwa maisha yao. Nambie ni ufalme gani utakufanikisha ikiwa

hauishi kwa sheria zake? Unatumia sheria za mbinguni kutaka kufanikiwa kwenye mfumo wa duniani.

Ikiwa unahitaji kufanikiwa kwa kanuni za kiMungu safari lazima ianze na suala la kuanza kuutegemea mfumo wa ufalme wa Mungu. Mungu ana mfumo wake na shetani ana mfumo wake. Tatizo ni kwamba watu wanatarajia kufanikishwa na Mungu ndani ya mfumo wa shetani. Ndio maana tunapambana na laana za mababu, na vifungo vya umaskini, tunakomboa nyota, tunakomboa ardhi na anga, tunapigana sana na roho za ufukara na laana za ukoo. Hivyo vyote vipo ila vipo kwenye mfumo wa shetani na kama wewe ni mwana wa Mungu na unataka kufanikiwa kwa kutumia mfumo wa shetani basi utavipiga sana hivyo vita na uwezekano wa kushindwa na mkubwa maana ni mfumo ndio unaamua kukufanikisha ama laa.

Hivyo vyote vipo ni kweli kabisa lakini ukiwa kwenye mfumo wa Mungu wa kuishi vyote vinakosa nguvu juu yako maana upo nje ya mfumo ambao vitu hivyo vinafanya kazi. Kuna mazingira ambayo nguvu ya ushawishi na hizo laana na vifungo vinafanya kazi na ikiwa upo kwenye mazingira hayo lazima vikuumize. Hivyo vinakuwa na nguvu na madhara kwako kwa kuwa upo kwenye mfumo wake. Suluhisho sio kupigana navyo bali kuondoka kwenye mfumo ambao vyenyewe vitakuwa na nguvu juu yako.

Moyo mgumu ni mkakati thabiti wa shetani kukufanya uwe tegemezi kwenye mfumo wake hapa duniani. Ni namna ya kukufanya utegemee mifumo na mazingira ambayo yeye ana nguvu nayo na anaweza kuamua kuhusu mustakabari wa mafanikio yao. Ikiwa una mwamini Mungu ama laah hiyo haikuondoi kwenye uwezekano wa

mafanikio yako kuamuliwa na shetani ikiwa atafanikiwa kuongozo maisha yako kwa mfumo wake. Ndio maana tuna watu wanamcha Mungu na kumpenda Mungu lakini wanafeli katika huduma zao, kazi zao, biashara, mahusiano, ndoa na hata familia. Ni kwa sababu shetani ana ushawishi ndani yao kwa kuwa wanaishi kwa kutumia mifumo yake. Kadri mtu anavyotamani kufanikiwa ndivyo changamoto zinavyozidi ni kama Mungu hamsikii na ameshindwa kumsaidia lakini ukweli ni kuwa hakuna namna ambayo Mungu anaweza kumsaidia mtu aliye nje ya mfumo wake Mungu.

Shetani anapomfanya mtu kuwa na moyo mgumu anakata mawasiliano baina ya mtu huyo na mfumo wa asili ambao Mungu alimtengeneza mwanadamu autumie kuishi. Na kwa kuwa mahitaji ya mtu bado yanakuwepo pale pale basi mtu analazimika kuongeza utegemezi juu ya mazingira na mfumo ambao sio wa asili ili maisha yake yaende mbele. Hana uwezo tena wa kupata mahitaji yake kupitia mfumo wa Mungu na bado anahitaji chakula, mavazi, pesa, watu, mwenzi; anavipata wapi hivi? Anakuwa hana budi bali kutumia mfumo feki uliopo hapa duniani. Utegemezi wake unavyozidi ndivyo anavyozidi kujiingiza kwenye hatari ya moyo wake kuwa mgumu zaidi.

Kwa kuwa mfumo huu sasa unakuwa na nguvu zaidi ya kuendesha maisha ya watu, mwenye mfumo huu yaani shetani anakuwa na nguvu ya kuamua hali za mioyo ya watu duniani. Akitaka mioyo ya watu kuwa migumu anaongeza hali ngumu za maisha hivyo anakuwa amefanikisha nia yake. Ndio maana unaona shetani huyu aliyeweka mifumo hii ambayo tunaitegemea ndio huyo

anawatumia watu kuharibu mifumo ili kuongeza ugumu wa maisha.

Ni kama kile ambacho Farao aliwafanyia wana wa Israeli. Maamuzi ya mtu mmoja yakaamua hatima ya taifa nzima na wote wakaingia kwenye mateso na utumwa, ndicho ambacho shetani anafanya sasa hivi. Anazidi kututengenezea utegemezi kwenye mifumo ya kiuchumi, technolojia, siasa, elimu, afya, vyakula; na kisha anaweza kumtumia mtu mmoja tu kuharibu maisha ya watu wengi kwa wakati mmoja. Mmoja tu anaweza kucheza na teknolojia na dunia nzima tukawa kwenye hali ngumu. Pata picha leo hii intaneti ikazimwa dunia nzima, nini kitatokea? Watu wachache ndio wanalisha dunia nzima, wachache ndio wameshikilia teknolojia, wachache ndio wanaamua kuhusu afya za watu, watu wachache ndio wanatunga sera za mwelekeo wa dunia. Mustakabali wa mambo ya msingi ya dunia yanaamuliwa na watu wachache sana. Tafsiri yake ni kuwa hawa wachache wakiamua dunia iteseke na kuwa na hali ngumu wana uwezo huo. Huu ndio mtego ambao tumekwisha ingia na tunaishi humo kwa sasa na inasikitisha kuwa watu wengi hawajui kuwa tupo kwenye mazingira hatari.

ROHO, MWILI NA NAFSI

***MWANZO 2:7****…"BWANA Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai."*

Hivi ndivyo vinamfanya mwanadamu aitwe mwanadamu;

- Mwili (mavumbi ya ardhi)
- Roho (pumzi ya uhai)
- Nafsi

Nafsi ni hali ya muunganiko baina ya mwili na roho. Mwili na roho vikiwa vimeungana mtu anaitwa “nafsi hai”. Mwili na roho vikitengana mtu anaitwa “nafsi mfu”. Kila mwanadamu ambaye anapumua hata kama anatumia mashine kwenye chumba cha wagonjwa mahututi huyo ni nafsi hai. Kila aliyezikwa ni nafsi mfu.

Sasa tukitaka kujua ikiwa mtu ni nafsi hai ama nafsi mfu huwa tunapima mapigo ya moyo. Moyo ukiwa unadunda tunafahamu kuwa mtu huyu ni nafsi hai (mzima), moyo ukiwa haudundi tunafahamu kuwa mtu ni nafsi mfu (amefariki). Hivyo basi;

*“Hali ya muunganiko baina ya mwili na roho ambayo inaitwa nafsi ilihifadhiwa kwenye moyo wa mwanadamu”*

Hapa tunaona uhusiano mkubwa baina ya moyo na nafsi.

Nafsi ya mtu inapojeruhiwa ndipo huzaliwa moyo mgumu.

“Moyo mgumu” ni “nafsi iliyojeruhi”

Tunapozungumzia moyo mgumu kimsingi tunazungumzia majeraha ya nafsi. Naelewa kuwa kwa wengi lugha ya majeraha ya nafsi inaweza kuwa imezoeleka zaidi kuliko lugha ya moyo mgumu lakini hivi viwili ni kitu kimoja. Shetani anapotaka kumfanya mtu kuwa na moyo mgumu anachofanya ni kutengeneza majeraha kwenye nafsi ya mtu. Atampiga mtu na matukio ya kuumiza, kunyanyaswa, ukatili, kufeli, misiba, kuonewa, kukataliwa, taarifa mbaya na za uongo; lengo lake ni kutengeneza jeraha na jeraha hili linaenda kuua Imani ya mtu kwa Mungu na kufanya ajiondoe kwenye kutegemea mfumo wa Mungu na kuanza kutegemea mfumo wa duniani katika kuendesha maisha yake.

Nafsi ni daraja linalounganisha roho na mwili. Ni geti linalopitisha taarifa kutoka mwilini kwenda rohoni na kutoka rohoni kwenda mwilini. Mungu ni roho. Katika roho, taarifa zinatakiwa kupita kwenye hili daraja na kuzifikisha mwilini. Rasilimali zote alizoandaa Mungu kwa ajili ya kila mmoja alipomuumba lazima zipite kwenye hili daraja(nafsi) ili ziweze kudhihirika katika jinsi ya mwili. Majeraha ya nafsi yanavunja hili daraja na kufunga hili geti ambalo linapitisha hizi taarifa. Moyo mgumu ni matokeo ya daraja hili kuvunjika na geti hili kufungwa.

Shetani anapompiga mtu na shida na hali ngumu lengo lake ni kujeruhi hii nafsi ili daraja livunjike na moyo wa mtu uwe mgumu. Daraja likivunjika mtu hupoteza uhusiano wake na Mungu na mawasiliano baina yake na Mungu. Mawasiliano baina ya roho na mwili yanakatika na hakuna kinachoweza kuvuka ng'ambo nyingine. Mwanadamu huyu anayehitaji rasilimali za chakula, mavazi, malazi, gari, nyumba; amevunjiwa daraja lililotakiwa kusafirisha rasilimali hizi kutoka rohoni (kwa Mungu) na sasa analazimika kuzitafuta yeye mwenyewe kwa nguvu zake kwa kutumia mifumo ya duniani kwa kuwa hana namna. Asipozitafuta atakufa na njaa na kiu, atatembea uchi, atalala nje.

Katika hali ya kawaida mazingira yanamshurutisha kuvitafuta hivi vyote kwa kutumia mifumo ambayo haikutengenezwa kwa ajili yake. Hapa ndipo ugumu wa maisha unapowapata wengi.


MWANADAMU ALIVYOPASWA KUISHI

*LUKA 12: 22-31.."Akawaambia wanafunzi wake, Kwa sababu hiyo nawaambia, MSISUMBUKIE MAISHA YENU, MTAKULA NINI; WALA MIILI YENU, MTAVAA NINI. Kwa*

*kuwa maisha ni ZAIDI YA CHAKULA, na mwili ni ZAIDI YA MAVAZI. Watafakarini kunguru, ya kwamba HAWAPANDI wala HAWAVUNI, hawana ghala wala uchaga, na MUNGU HUWALISHA. Bora ninyi mara nyingi kuliko ndege! Na yupi kwenu ambaye akijisumbua aweza kujiongeza kimo chake hata mkono mmoja? Basi, ikiwa hamwezi hata neno lililo dogo, kwa nini kujisumbua kwa ajili ya yale mengine? Yatafakarini maua jinsi yameavyo; HAYATENDI KAZI WALA HAYASOKOTI; nami nawaambia ya kwamba hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo la hayo. Basi ikiwa Mungu HUVIKA hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo na kesho hutupwa kalibuni, je! HATAWATENDEA NINYI ZAIDI, enyi wa IMANI HABA? Ninyi msitafute MTAKAVYOKULA; WALA MTAKAVYOKUNYWA; wala MSIFANYE WASIWASI, kwa maana, hayo yote ndiyo WATAFUTAYO MATAIFA YA DUNIANI, LAKINI BABA YENU ANAJUA YA KUWA MNA HAJA NA HAYO. Bali utafuteni UFALME WA MUNGU, na hayo MTAONGEZEWA."*

Mataifa ya dunia wanahangaika na kujisumbua na suala la wana kula nini, wanavaa nini, wanakunywa nini, wanaishi wapi, watamuoa ama kuolewa na nani, watafanya kazi gani; lakini ninyi mlio wana wa ufalme wa Mungu, Baba yenu wa mbinguni anajua kuwa mna haya na hayo yote. Tafsiri yake ni kuwa Mungu alipotuumba alijua kuwa vyote hivyo tunavihitaji ili maisha yetu yawe na utulivu. Na kama anavyowalisha ndege wa angani na kama anavyoyavisha maua ya kondeni je! Anashindwa kufanya hivyo kwetu sisi? Tatizo ni Imani haba. Kuwa haba ni matokeo ya moyo kuwa mgumu baada ya nafsi kujeruhiwa na hali ngumu za maisha. Ikazaliwa hofu na mashaka, hivyo mtu anaamua kujipambania.

MZUNGUKO WA ASILI NA MZUNGUKO FEKI




MZUNGUKO FEKI

***YEREMIA 17:5-6****…"BWANA asema hivi, AMELAANIWA mtu yule AMTEGEMEAYE MWANADAMU, Amfanyaye mwanadamu kuwa KINGA yake na MOYONI MWAKE AMEMWACHA BWANA. Maana atakuwa kama FUKARA NYIKANI, HATAONA YATAKAPOTOKEA MEMA; Bali atakaa*

*JANGWANI PALIPO UKAME, katika NCHI YA CHUMVI ISIYOKALIWA NA WATU"*

Athari anazopata mtu kwa kumtegemea mwanadamu yeyote kwa namna yoyote (kuishi kwenye mzunguko feki) ni kupata laana. Laana hii itamfanya;

- Aishi maisha ya ufukara (asiye na muelekeo kiuchumi, kimalengo, kimaisha)
- Mema yakija, hataona (fursa sahihi, watu sahihi, mwenzi sahihi, kibali)
- Atakuwa kama mtu aishie kwenye jangwa na ukame (njaa, shida, uhitaji, kiu, madeni)
- Atajihisi mpweke na aliyetengwa (nchi isiyokaliwa na watu)

Unaweza kuhusianisha mambo haya na maisha ya watu wengi nyakati hizi? Unaweza ukaelewa ni wapi tatizo la Afya ya Akili linatokea? Kwa nini watu wanaumwa magonjwa ya ajabu; presha, kisukari, vidonda vya tumbo, msongo wa mawazo, sonona, hofu. Watu hawapati usingizi, wamekata tamaa ni wapweke mno. Watu wanafanya kazi kwa bidii lakini hakuna mpenyo. Kila akiingia kwenye mahusiano, mara zote anaingia kwa watu wenye tabia zile zile za kumuumiza na kumnyanyasa (akija mtu sahihi haoni). Utegemezi juu ya wanadamu ndio umekuwa chanzo cha haya maumivu na changamoto ambazo wanadamu wanapitia.

Inawezekana kabisa utegemezi ambao wengi wanao ni wa kimfumo. Waliaminishwa hivyo tangu utotoni. Furaha yako inatokana na mume au mke wako, hujakamilika mpaka uoe au uolewe na ukishaingia kwenye ndoa hujakamilika mpaka uwe na watoto.

Kutoka furaha ya mtu kutegemea mume ama mke na sasa inaanza kutegemea watoto. Aliaminishwa kuwa mafanikio yako yapo kwenye elimu yako. Soma sana ufanikiwe na akiwa anasoma anaaminishwa kuwa mafanikio yako yapo kwenye kufaulu vizuri maana hapo utapata kazi nzuri. Amemaliza chuo ila hana furaha kwa kuwa sasa hana kazi. Na akipata kazi anaambiwa mafanikio yako ni kufanya kazi kwa bidii ili uongezwe cheo na mshahara. Ukiwa na hela nyingi utakuwa na furaha. Anaona kazi haiwezi mpatia furaha bora aache aanzishe biashara.

Ghafla anagundua kuwa hawezi kupata hela mpaka apate mkopo wa benki kuanzisha biashara. Bado mafanikio ya biashara yake yanategemea mifumo na wanadamu. Unaona kabisa kuwa tunaishi maisha yetu lakini asilimia kubwa ya kuishi na kufanikiwa kwetu tunategemea wanadamu wenzetu. Hatuna namna ambayo tunayaona mafanikio nje na utegemezi wetu kwa watu. Tunalazimika kutumika na kuwatumia wengine ili kufanikiwa, kuwa na furaha na amani. Pale inapotokea hawajafanya kama tunavyotarajia tunajikuta kwenye hali ngumu na mwisho moyo mgumu unazaliwa ndani yetu.

Laana inayozungumziwa hapa sio kwamba Mungu analaani mtu bali mtu anakuwa ametengwa na Baraka za Mungu. Geti la kupitishia rasilimali zilizoandaliwa kwa ajili yake awapo hapa duniani limefungwa. Kwa kuzikosa hizo baraka inamuweka kwenye kundi la waliolaaniwa. Sio kwa sababu Mungu anataka kumlaani ila ni kwa kuwa mfumo anaotumia kuishi haumruhusu kuzifikia Baraka za Mungu. Ni laana ya kimfumo.

Kama shetani amelaaniwa tangu mwanzo na wewe mwanadamu unatumia mfumo wa aliyelaaniwa unakuwa

umelaaniwa pia. Hapa hakuna kiwango cha maombi na maombezi kitakutoa maana kila wakati unapotaka kwenda mbele unampa nafasi shetani kutumia mifumo yake unayoitegemea kukukwamisha kwenda.

*Mzunguko Feki unafanyaje kazi?*

Husika na mchoro hapo juu;

Shetani anaanza kwa kuvunja daraja (kujeruhi nafsi) na kufunga geti (kufanya moyo mgumu) ili kuhakikisha Baraka za rohoni hazivuki kuja mwilini. Hata hivyo, mahitaji ya mwili yapo palepale; chakula, mavazi, maji, makazi, usafiri, pesa, mwenzi, familia. Umezuiwa kuyapata kutoka kwenye mfumo halisi ambao Mungu aliutengeneza lakini bado unayo mahitaji yote. Na shetani anahakikisha anachochea mahitaji yako yawe makubwa zaidi. Anakuongezea shida, njaa, maumivu ya kihisia na kifikra, anakuongezea mizigo ya watu wengine wanaokutegemea. Mahitaji yako yanageuka kuwa ndio mtego wako. Mahitaji yanaua kusudi kwa kuwa adui namba moja wa kusudi la Mungu kwenye maisha ya mtu ni mahitaji yake mwenyewe.

Mwanadamu analazimika kuanza kujipigania mwenyewe ili kupata mahitaji yake. Huku kujipigania ndiko kuna muweka kwenye kutegemea watu na mfumo feki wa maisha. Mahitaji yake yanamsukuma kuwa na tabia (vitendo) fulani. Tabia na vitendo hivi ndio humletea rasilimali anazohitaji ili kukidhi mahitaji yake. Tabia na vitendo vilivyochochewa na mahitaji sio kwa kusudi la Mungu.

Hapa ndipo tupokutana na wale ambao wanaingia kwenye mahusiano na ndoa kwa kusukumwa na upweke, maumivu, msongo wa mawazo, changamoto za kiuchumi, hofu ya umri, hofu ya kuchekwa na watu, aibu ya kupewa mimba, ama kwa sababu wazazi na ndugu wanamuuliza sana, wanataka wajukuu. Kashindwa maisha yake anafikiri ndoa itamtatulia changamoto zilizomshinda. Matokeo yake tunakuwa na ndoa na mahusiano yenye migogoro mingi maana kilichowaingiza humo ni mahitaji yao binafsi sio kusudi la Mungu. Anaonekana ana tabia njema na upendo kumbe ndani yake ipo hila ya kutaka kuwa na mwenzi ili amtumie kutimiza mahitaji yake.

Hapa ndio tunapokutana na watu ambao wanatafuta ajira kwa sababu ya shida na njaa ya hela. Anaanzisha biashara kwa sababu ya mahitaji ya kiuchumi. Anaingia kwenye siasa kwa kusukumwa na njaa na shida zake. Anaanzisha huduma na kanisa kwa kusukumwa na shida na njaa. Anapigania nafasi za uongozi ili kinachomsukuma ni mahitaji ya kiuchumi, kutaka heshima na hadhi. Anatafuta wafuasi hata kwenye mitandao ya kijamii ili kinachomsukuma ni mahitaji yake ya kihisia na kiuchumi. Msukumo wa tabia na vitendo vyake unatokana na mahitaji yake badala ya kusudi la Mungu. Mtu huyu hawezi kuthamini wengine, hawezi kuwalinda, hawezi kuwajali na kuwapenda. Anaithaminije kazi? Anakuwaje mbunifu kazini au kwenye biashara? Anawezaje kuwa mwalimu mzuri wa biblia? Anawezaje kuwa kiongozi mwenye uzalendo anayeweza kulinda rasilimali za nchi kwa manufaa ya wengi. Anawezaje kuwa kiongozi mzuri, mume mzuri, mke mzuri, mzazi mzuri? Anatoa wapi hiyo tabia ikiwa inachochewa na mahitaji yake. Hivi ndivyo

mzunguko wa juu (feki) unavyofanya kazi. Mahitaji ndio yanavuta rasilimali.

MZUNGUKO WA ASILI (MUNGU)

***YEREMIA 17:7-8…****"Amebarikiwa mtu yule ANAYEMTEGEMEA BWANA, Ambaye BWANA ni TUMAINI LAKE. Maana atakuwa kama MTI ULIOPANDWA KANDO YA MAJI, uenezao mizizi yake karibu na mto; HAUTAONA HOFU wakati wa hari ujapo, Bali JANI LAKE litakuwa BICHI; wala HAUTAHANGAIKA mwaka wa UCHACHE WA MVUA, wala HAUTAACHA KUZAA MATUNDA"*

Wakati ardhi ni kavu, kuna ukame, jangwani, hakuna mvua; mizizi ya mti huu imeenea katika mto na hivyo hauhangaiki na wala hauachi kuzaa matunda yake. Ndivyo alivyo mtu anayemtumaini Mungu na kuacha kabisa kuwategemea wanadamu. Kwa maana nyingine ni kuwa mtu huyu haathiriwi na mazingira wala wanadamu wenzake. Haathiriwi na kuyumba kwa uchumi, uchache wa ajira, mmonyoko wa maadili, ugumu wa maisha, migogoro ya mahusiano na ndoa.

Haathiriwi na mabadiliko ya tabia za watu, tabia ya nchi, sera za nchi, siasa za nchi, vita, njaa, na uharibifu mwingine wowote. Hakuna kilichopo katika ulimwengu huu kinachoweza kumkwamisha yeye kuzaa matunda aliyokusudiwa kuzaa.

Kwa lugha nyepesi ni kuwa kusudi la Mungu haliwezi kuzuiwa na mifumo ya dunia hii wala shetani. Mafanikio ya mwanadamu hayawez kuzuiwa na mifumo hii wala wanadamu wala shetani. Kile ambacho Mungu alikiweka

ndani ya mwanadamu ili aliishi kusudi la Mungu kitachipua tu bila kujali mazingira ya nje. Wakati wengine wanakwama, wanaumizwa, wanajuta, wanafilisika, wanashindwa kufanikiwa, hawana ajira, biashara zinakufa, ndoa zinavunjika, mahusiano yanawaumiza, wana vilio, majonzi, huzuni, upweke; anayemtumaini na kumtegemea Mungu atachipua na kufanikiwa.

Mungu habadilishi mifumo ya duniani ili iwafae wanadamu. Ni vyema tuache kuomba Mungu kubadili mifumo ya siasa, uongozi, uchumi, afya, sheria, dini ili iwahifadhi wanaomtegemea Mungu. Mungu haitaji mifumo hiyo kubadilika ili kufanikisha kusudi lake duniani. Mifumo hiyo sio kikwazo kwake. Mifumo hiyo sio yake ina mmliki wake anaitwa mungu wa dunia hii (shetani). Yeye ndio ana haki miliki za mifumo hiyo na ndiye anayeendesha anavyotaka yeye. Na Mungu hana uwezo wa kubadili hiyo mifumo ila kusudi lake hapa duniani na kwenye maisha ya mtu haliwezi kuzuiwa na mifumo hiyo.

Mifumo hii yote haina nguvu ya kuzuia kusudi la Mungu. Ukijua hili utapunguza kupigana vita vya kiroho vya kukemea na kuharibu mifumo na utaelekeza nguvu zako kwenye kumtegemea Mungu na kutafuta zaidi ufalme wake. Katika ukame utachipua na kuzaa matunda wakati wengine wananyauka na kufa. Katika mfumo huu wa duniani ambao wengi wanashindwa kufanikiwa wewe utafanikiwa. Utafanikiwa katika nchi ya ugenini, mahali ambapo hukustahili ufanikiwa. Huu ndio mzunguko wa asili.

*Mzunguko wa asili unafanyaje kazi?*

Rejea mchoro hapo juu;

Katika mzunguko wa chini, katika Roho; Mungu alifanya maamuzi ya kukuumba na kukuleta duniani. Ila kuumbwa kwako lengo lilikuwa uje kuliishi kusudi lake hapa duniani. Wewe ushughulike na kusudi lake, Yeye Mungu ashughulike na mahitaji yako hapa duniani. Huo ndio mgawanyo. Yeye anakuhitaji wewe kutimiza kusudi lake na wewe unamuhitaji Yeye kupata mahitaji yako yote hapa duniani. Na anajua kuwa una haja nayo (Luka 12:30) wala huhitaji kufunga na kuomba kuvipata. Anajua kuwa kwa kadiri unavyodumu hapa duniani una haja na hayo yote ila sio jukumu lako kuvitafuta bali jukumu lako ni kutimiza kusudi la kuumbwa kwako.

Rasilimali zote unazohitaji kwa ajili ya kutimiza kusudi na kupata mahitaji yako zipo Rohoni (kwa Mungu). Ili ziweze kufika mwilini taarifa lazima ipitie kwenye nafsi (geti, daraja). Hili geti lazima liwe wazi yaani mtu asiwe na moyo mgumu. Taarifa hizi zikifika kwenye nafsi (moyo) zinabadilishwa kutoka kwenye taarifa na kuzalisha tabia (vitendo) katika mwili. Hizi tabia na vitendo vinakuwa na majukumu mawili makubwa;

- Kukuwezesha kuliishi kusudi la Mungu na kuiendea hatima yako
- Kuvuta rasilimali zote unazozihitaji kwa ajili ya maisha yako

Wakati wewe unatumia tabia, vitendo na mwenendo uliozaliwa kutokana na taarifa kutoka Rohoni kuliishi kusudi la Mungu; Mungu anatumia tabia, vitendo na mwenendo huo huo kukuletea watu sahihi, mume ama mke sahihi, elimu sahihi, biashara sahihi, kazi sahihi, pesa, mali, nyumba, gari na kila unachohitaji ambacho

kitawezesha kufanikisha kusudi. Hapa sio suala la wewe kuhitaji bali kusudi lake kutimia kwa hiyo vyote unavyoletewa dhumuni ni kukusaidia wewe kutimiza jukumu lako la msingi.

Hivyo katika mzunguko huu wewe unabaki kwenye “duara la chini” la kutafuta ufalme wa Mungu ili kuishi kusudi lake Mungu na unamuachia Mungu kuyatumia mazingira kukupatia kila unachotaka kwa kutumia tabia zako. Hapa sio wewe unayatumia mazingira ya duniani bali Mungu (mwenye uwezo wa kupambana na shetani mwenye mfumo huu wa duniani) anayatumia mazingira hayo kukupatia kila unachohitaji. Hivyo wewe unajiepusha na vita ya kupigana na majini, mizimu, vifungo vya laana na ukoo, kukomboa nyota na ardhi na anga na udongo; unaacha kutumia vifaa vya upako ili kuvuta Baraka na mafanikio na unamuachia hiyo kazi Mungu akufanyie wewe wakati wewe unafanya kazi yake.

Ukiishi kwa mzunguko feki (Yeremia 17:5-6) unafanya kazi ambayo Mungu alipaswa kufanya. Ukiishi kwa mzunguko halisi (Yeremia 17:7-8) unafanya kazi uliyopaswa kufanya na kumuachia Mungu kufanya kazi aliyopaswa kufanya. Na ile ambayo Mungu alipaswa kufanya itakuletea rasilimali zote ambazo zinaitwa “nyongeza”. Ukiishi mzunguko feki unageuza nyogeza kuwa ndio halisi. Hakuna mnunuzi anayoenda kununua akiwa anawaza “nyongeza” bali kile anachopaswa kununua. Nyongeza ni jukumu la muuzaji na hapangiwi kipimo na mnunuzi. Ndio maana anasema “msiwaze mtakula na kuvaa nini”. Hivyo ni nyongeza. Akili zetu zinapaswa ziwaze kusudi la Mungu na ufalme wake na tumuache Yeye aamue vile anavyotubariki kwa kadri ya mapenzi yake kwetu.

## SURA YA 09

# UNAISHI KATIKA MFUMO GANI?

Unaishi katika mfumo halisi au feki? Ungali bado uko hai na unasoma kitabu hiki ni muhimu sana kupata majibu ya swali hili. Ni hatari sana kuishi maisha yako ukiwa hujui unamilikiwa na mfumo upi. Ni muhimu kujua mafanikio yako katika nyanja yoyote hapa duniani hayaamuliwi na bidii yako pekee bali mfumo ambao unaumiliki. Sio kiwango cha elimu, ujuzi, uzoefu, fedha ama fursa. Wapo wengi walio na fursa nyingi lakini hawafanikiwa; wapo wenye elimu, ujuzi na uzoefu kuliko wewe na walishindwa kufanikiwa. Wapo waliowahi kupata pesa nyingi zaidi yako na bado mwisho wao ulikuwa mbaya. Pengine unaweza kudhani kutofanikiwa kwako ni kwa sababu ya mazingira uliyopo, nchi uliyopo, kiwango cha elimu ulichonacho, ukoo au familia uliyozaliwa, kukosa fursa za namna fulani. Kuna wengi ambao wapo duni kuliko wewe na walianzia hapo na wakafanikiwa zaidi ya ulivyofanikiwa ikiwa ni kiuchumi, kitaaluma, kihuduma, kibiashara. Walianzia mahali pagumu kuliko ulipo wewe, wakafika mbali kuliko wewe.

Ukweli ni kuwa hakuna kati ya hivyo ambacho ndicho hasa mkwamo wako. Kuna jambo lingine kubwa na la muhimu zaidi. Mifumo; Kujua kuhusu mifumo inavyotenda kazi na jinsi ya kukaa humo ili ufanikiwe kupitia hiyo. Angalia wasanii na waimbaji, wachezaji, wanasiasa, wahubiri na viongozi wakubwa.

Ukisoma historia za watu hawa mashuhuri duniani, wengi wao walianzia zero hadi kuwa vinara. Siri waliyoigundua ambayo wengi hawawezi kuisema na kuelewa jinsi mifumo inavyofanya kazi. Wapo waliokuwa na bidii, elimu, ushawishi, uwezo mkubwa kuliko wao lakini walikwamia njiani.

Lazima umilikiwe na mfumo fulani hapa duniani. Mfumo unaokumiliki huamua kiwango gani ufanikiwe. Hakuna mtu anayefanikiwa bila kumilikiwa na mfumo fulani. Kuna mifumo ya elimu, siasa, uchumi, biashara, burudani, afya, huduma; na hii yote inamilikiwa na lazima umilikiwe na anayeimiliki kwanza kabla haijakufanikisha. Hii ndio hutoa idhini ya kiwango cha mtu kufanikiwa vinginevyo utaishi ukila mabaki. Huwezi kunufaishwa na mifumo hii ikiwa "haikumiliki". Unapotaka kufanikiwa ni lazima kujiuliza nafanikishwa na mfumo upi na je! Namilikiwa na mfumo huo?

Kila mfumo una agenda zake ili kutimiza kusudi fulani hapa duniani. Agenda hizi na kusudi hilo linajulikana na wamiliki wa mifumo na wengine jukumu lao ni kutekeleza agenda ili kutimiza kusudi. Kila mmoja analo jukumu lake analopewa na mmiliki wa mfumo husika na kila wakati anapofanikisha agenda anapata manufaa ambayo yanaweza kuwa ya kiuchumi, kihadhi, kiheshima, cheo ama nafasi. Inakuwa ni zawadi baada ya kutimiza kusudi la mfumo. Kwa bahati mbaya mtekelezaji wa jukumu hana nafasi ya kujua kusudi la mfumo isipokuwa ikiwa amepewa nafasi hiyo na mmiliki. Kusudi la mfumo linafahamika na mmiliki mkuu wa mfumo na pengine wengine wachache ambao ndio watekelezaji wakuu wa agenda. Tunachokiona sisi ni matukio, picha, video, shughuli ila tusichokijua ni kuwa nyuma ya kila tukio,

shughuli, picha, na video kuna agenda na kusudi ambalo hata wale wanaofanya hizo shughuli pengine hawajui. Wanatumiwa kufanikisha kusudi na wanazawadiwa kwa kulifanikisha.

Unakumbuka ile kauli ya Yesu ya "utafuteni kwanza ufalme wa Mungu na hayo yote mtazidishiwa?". Hapa utaanza kuelewa jinsi mifumo inavyofanya kazi.

Dunia hii inaendeshwa na mfumo halisi ambao unamilikiwa na Mungu; na mfumo feki unaomilikiwa na shetani. Wote, Mungu na shetani wana agenda zao na makusudi yao ambayo wanataka yatimie hapa duniani. Watekelezaji wa agenda na makusudi hayo ni sisi wanadamu ambao tulikabidhiwa hii dunia. Mungu hawezi fanikisha kusudi lake pasipo kumtumia mwanadamu na shetani hali kadhalika. Hapa utaelewa ni kwa nini ilimlazimu Yesu kuacha uungu wake akavaa mwili. Haikuwezekana kubaki katika hali ya kiungu na kufanikisha agenda ya kuuokoa ulimwengu.

Kila mwanadamu anapofanikisha agenda ya mfumo, anapewa zawadi. Mungu ana namna ya kuwazawadia wale wanaotekeleza agenda zake na shetani ana namna yake. Zawadi hizi sisi huziona katika taswira ya mafanikio ya mtu. Utajiri, hadhi, heshima, kibali, cheo, umaarufu. Nyuma ya mafanikio hayo mtu anakuwa amelipa gharama ya kufanikisha agenda fulani katika mfumo unaommiliki. Tunaweza kuyatamani mafanikio yake lakini ni muhimu kujua kuwa mafanikio hayo sio kitu bali kile alichokifanya kuyapata. Wengi waliofanikiwa na tunaotamani mafanikio yao wakikusimulia gharama wanayolipa kuyapata unaweza kushangaa na hata usiyatamani kamwe mafanikio yao. Tunatamani mali wanazomiliki, wafuasi

walionao kwenye mitandao ya kijamii, fursa za kibiashara wanazopata, mialiko wanayopata lakini hatujui kuwa kuna nini wanachokifanya.

Umewahi kujiuliza ni kwa nini wakati mwingine wenye vipaji vikubwa zaidi duniani hawaonekani kufanikiwa kuliko wenye uwezo wa wastani. Wale wanaoimba haswa sio wanaofanikiwa zaidi, wale wenye kipawa cha uongozi haswa sio ndio wanaotawala, wale wasomi na wajuzi wa mambo haswa sio wanaofanikiwa, sio wenye upako na mafunuo, maombi na kufunga haswa ndio wenye makanisa makubwa; sio wenye bidii na wafanya kazi sana ndio hufanikiwa; hivyo utaelewa kuwa kipawa pekee, elimu, uzoefu na bidii pekee haitoshi.

Kuna suala la kufanya kazi na mifumo ambayo ndio hasa imeshikilia mafanikio ya watu. Usinielewe vibaya, hivyo vyote ni muhimu na hata mifumo hutafuta watu wenye hizo sifa ili kuwatumia ila kuwa na hivyo na ukavitumia nje ya mifumo na bila kuwa na agenda ama kutimiza kusudi fulani unaweza usipate matokeo unayoyatarajia.

Imba sana tena kwa ubora, ikiwa ni nyimbo za injili ama za dunia; lakini swali unalopaswa kujiuliza ni unaimba kwa maslahi ya mfumo gani, unatekeleza agenda gani na kuna kusudi?

Fanya kazi, fanya biashara kwa bidii, ubunifu na kwa weledi mkubwa; ila jiulize hii ni kwa ajili ya manufaa ya mfumo gani, agenda ni nini na kusudi ni lipi?

Kuwa kiongozi, ikiwa ni wa dini, siasa ama taasisi yoyote lakini muhimu kujua ni kuwa unafanya kwa maslahi ya mfumo upi, agenda ni ipi na kusudi ni lipi?

Kipawa chochote ulichonacho, uwezo ulionao, karama uliyonayo kabla hujaanza kuitumia jiulize mfumo upi unanufaika, agenda ni nini na kusudi ni nini?

Soma sana, maliza viwango vyote vya elimu; elimu ya dunia na elimu ya dini ila kabla hujaendelea sana jiulize ni kwa manufaa ya mfumo gani, agenda ni nini na kusudi ni nini?

Hubiri, fundisha, ombea watu na fanya kazi ya huduma; funga, omba ila kabla hujaendelea mbele sana jiulize nanufaisha mfumo gani, agenda ni nini na kusudi ni lipi?

Chochote ufanyacho, popote ulipo, lolote unalolifanya kwa bidii na juhudi nyingi; Kumbuka wale wote waliofanikiwa hawakufanikiwa kwa kile walichokuwa wanalifanya bali walifanikishwa na mifumo ambayo walikuwa wakitekeleza agenda zake.

Tunajua una harakati nyingi, matukio mengi, kazi nyingi na hata hupumziki ila agenda yake ni nini na kusudi lake ni nini?

Hakuna mfumo unaotenda kazi bila agenda na kusudi. Wewe umejipambanua kwenye mfumo upi isije ikawa unafanya kazi ya kuchosha usiku kucha. Nje ya mfumo samaki wanaweza kukukimbia usiku lakini akiwepo anayemiliki mfumo hata mchana samaki wanavuliwa tena wengi wakukata nyavu, muulize mtume Petro siku ukikutana naye.

Kuna kumilikiwa na mifumo na wewe kuwa tayari kutekeleza agenda za mifumo na kutimiza makusudi ya mifumo husika. Kumilikiwa pekee pia haitoshi.

Mafanikio ni zawadi baada ya kufanikisha agenda. Ukimilikiwa na usitekeleze agenda utakula mabaki yanayoachwa na wale wanaotekeleza agenda. Utakuwa mtumwa na kibaraka wa wanaotekeleza agenda. Hutatumiwa na mifumo bali utatumiwa na wale wanaotumiwa na mifumo. Wanaotumiwa na mifumo wataamua mustakabali wa maisha yako na kiwango cha mafanikio yako. Utalazimika kukaa nyuma yao na kutegemea huruma yao ili maisha yako yaendelee.

Hapa unajitengenezea tatizo la Moyo Mgumu kwa kuwa sasa maisha yako hayategemei mfumo unaotakiwa kukulisha, kukuvisha na kukufanikisha bali unawategemea wanadamu ambao wamelipa gharama kubwa ili kuyapata mafanikio hayo. Cha kujiuliza ni kuwa je! Rasilimali zako unazipata kutokea kwenye mfumo ama ni mabaki yanayoanguka kutoka kwa wale wanaotumiwa na mfumo. Kwa mfano, kipato chako kinatoka kwenye chanzo ama unagawiwa kajisehemu ka mafanikio ya wale unaowafanyia kazi?

Mungu na shetani wanajua hili na ndio maana hawana shida na watu wa namna hii ila tu ni ukweli kuwa kamwe hawawezi kuwafanikisha watu wa jinsi hii. Kwenye mifumo hii kuna mabwana na watumwa. Ikiwa unapata mafanikio yako kutoka kwenye mfumo basi wewe ni “bwana” na ikiwa mafanikio yako yanategemea kile kinachobakizwa na mabwana basi wewe ni “mtumwa”. Sio vibaya kuwa mtumwa ila mabwana ndio wanaamua kiwango cha mafanikio yako na sio mifumo. Sasa kwa mfano unapoomba Mungu akufanikishe wakati unamtegemea muajiri wako na yeye ndio anaamua kiwango cha kufanikiwa kwako, Mungu atajibu vipi maombi yako? Inabidi amfanikishe muajiri wako na hawezi mfanikisha

kama hatekelezi agenda yake, hivyo Mungu atashindwa kukufanikisha si kwa sababu hataki bali kukufanikisha wewe lazima amfanikishe mwingine ambaye hana vigezo. Utaumia wewe kwa utegemezi wako kwa huyo.

Katika kumilikiwa na mfumo na kuwa tayari kutekeleza agenda na kusudi la mfumo ndipo tunakuta na makundi makubwa matatu ya watu ulimwenguni;

- Wanaomilikiwa na Mungu na kufanikiwa sana katika mifumo ya Mungu
- Wanaomilikiwa na shetani na kufanikiwa sana katika mifumo ya shetani.
- Wanaomilikiwa na Mungu au shetani lakini hawafanikiwi katika mifumo inayowamiliki bali wanaishi kutegemea wengine.

Makundi haya matatu unaweza kuyaona vizuri na kujifunza zaidi kutokea kwenye habari maarufu sana ya kwenye biblia ya Ibrahimu, tajiri na Lazaro masikini.

***LUKA 16:19-24****…"Akasema, Palikuwa na mtu mmoja, tajiri. Aliyevaa nguo za rangi ya zambarau na kitani safi, na kula siku zote kwa anasa. Na maskini mmoja, jina lake Lazaro, huwekwa mlangoni pake, ana vidonda vingi, naye alikuwa akitamani kushibishwa kwa makombo yaliyoanguka katika meza ya yule tajiri; hata mbwa wakaja wakamramba vidonda vyake. Ikawa yule maskini alikufa, akachukuliwa na malaika mpaka kifuani kwa Ibrahimu. Yule tajiri naye akafa, akazikwa. Basi, kule kuzimu aliyainua macho yake, alipokuwa katika mateso, akamwona Ibrahimu kwa mbali, na Lazaro kifuani mwake. Akalia, akasema, Ee baba Ibrahimu, nihurumie, umtume*

*Lazaro achovye ncha ya kidole chake majini, auburudishe ulimi wangu; kwa sababu ninateswa katika moto huu."*

Kwa wengi wanaosoma habari hii huwa wanaitazama katika muktadha wa Lazaro na tajiri lakini Ibrahimu huwa hawampi umakini, kwa nini hawa watu waliandikwa hapa. Tukiweka pembeni ufafanuzi wa kithiolojia kuhusu nia ya kifungu hiki, tutumie hawa watatu kuchambua dhana ya kumilikiwa na kutumiwa na mifumo inayoendesha dunia hii.

***Ibrahimu***

Alikuwa mtu tajiri na aliyefanikiwa sana katika wakati wake. "Alimtegemea" Mungu, "akabarikiwa" na Mungu na alikuwa na "watumwa" nyuma yake waliomtegemea yeye. Na alipokufa alienda "mbinguni". Hapa tunaona kuwa mtu ambaye alimilikiwa na mfumo wa Mungu, akatekeleza agenda za Mungu, akaliishi kusudi la Mungu, akafanikishwa na mfumo huo, akawa tajiri na akawa na watumwa waliomtegemea yeye hata alipokufa aliendа mbinguni kwa kuwa mbingu ni mali ya Mungu.

***Tajiri***

Alikuwa ni mtu aliyefanikiwa sana katika wakati wake. "Alimtegemea" shetani, "akafanikishwa" na mifumo ya shetani na alikuwa pengine na "watumwa" yake waliomtegemea yeye. Hata alipokufa alienda "kuzimu". Hapa tunaona kuwa mtu ambaye alimilikiwa na mfumo wa shetani, akatekeleza agenda za shetani, akaliishi kusudi la shetani, akafanikishwa na mfumo huo, akawa tajiri na akawa na watumwa waliomtegemea yeye na alipokufa alienda kuzimu kwa kuwa kuzimu ni mahali pa shetani. Si kwamba Mungu hakuwa anataka tajiri asiende mbinguni

bali alikuwa anamilikiwa na mfumo ambao hatima yake ni kuzimu.

***Lazaro***

Alikuwa ni mtu masikini sana. “Alimtegemea” tajiri kuishi maisha yake, “mafanikio yake” yalitegemea huruma ya tajiri na aligeuka kuwa mtumwa wa tajiri. Utasema pengine hakuwa mtumwa lakini jiulize tajiri alipata wapi ujasiri wa kumuomba Ibrahimu “amtume” Lazaro. Alikuwa anamuona kama mtumwa wake hata baada ya kufa. Hakuweza mtuma Ibrahimu. Lazaro “alimtegemea” tajiri lakini “alimilikiwa” na Mungu. Matokeo yake akaishi maisha ya shida, tabu, njaa, kuomba omba hapa duniani lakini alipokufa akaenda “mbinguni”. Alimilikiwa na Mungu lakini alikuwa hatekelezi agenda wala kusudi la mfumo unaommiliki.

Katika ili tunajifunza kuwa duniani kuna makundi mawili tu ya watu

1. Kundi linalotumiwa moja kwa moja na mifumo
2. Kundi linalotumiwa na wale wanaotumiwa na mifumo

Kundi la wale wanaotumiwa na mifumo ndio Ibrahimu na tajiri. Hawa wanakuwa na Agenda maalumu wanazozitekeleza kwenye maisha kwa kadri ya maelekezo ya mifumo yao.

Hawa wanapokea maelekezo ya moja kwa moja ndani ya mioyo yao kuhusu agenda hizo na wamedhamiria kuishi. Maisha yao hayaongozwi na mahitaji bali kusudi la mifumo wanayoitumikia. Kazi, biashara na kila shughuli wanazofanya ni kwa lengo la kunufaisha mfumo

wanaoutumikia na rasilimali zao zote zinatolewa na mifumo hii. Kwa kuwa wananufaisha mifumo yao basi mifumo hii huwanufaisha wao pia. Na hiki ndio kiini cha kufanikiwa kwao na ndio maana wanakuwa matajiri.

Kundi linalotumiwa ama kuwatumikia wale wanaotumiwa na mifumo ndio Lazaro masikini. Hawa ni wale ambao wanamilikiwa na mfumo aidha feki(shetani) ama halisi(Mungu) lakini hawana agenda ambazo wanatekeleza kwenye mifumo hii. Wao agenda zao ni mahitaji yao; chakula, malazi, makazi, usafiri na mengineyo. Hawa hupokea maelekezo kutoka kwa wale wanaotumiwa na mifumo. Hawa huwa ni watumwa wa watu wanaotumiwa na mifumo. Rasilimali zao ni mabaki yanayoanguka kutoka kwenye meza za wanaotumiwa na mifumo.

Hapa utajua kuwa mtu anapokufa anaenda kule ambako anamilikiwa. Kama alimilikiwa na Mungu ataenda mbinguni bila kujali kuwa alifanikiwa ama hakufanikiwa duniani. Na kama alimilikiwa na shetani ataenda kuzimu bila kujali alifanikiwa ama hakufanikiwa duniani. Kuwa mtakatifu au muovu haifanyi mtu afanikiwe au asifanikiwe duniani. Kinachofanya mtu kufanikiwa duniani ni kutekeleza agenda za mfumo unaommiliki na kutimiza makusudi yake.

Jiulize unamilikiwa na mfumo gani? Unatekeleza agenda za mfumo wako unaokumiliki au unatumiwa tu na wanaotekeleza agenda za mifumo. Kazi, biashara, jitihada zako zote zinasukumwa na mahitaji au kusudi la mfumo unaokumiliki? Rasilimali zako zinatoka kwenye mifumo moja kwa moja au ndio unakula mabaki yanayoanguka kutoka kwenye meza za wenye agenda ya mifumo. Jiulize ukifa utaenda wapi kwa mfumo unaokumiliki sasa? Je,

umejiandaa kuwepo huko? Sasa una uamuzi wa kuchukua. Katika mfumo wowote ulioamua kujimilikisha hakikisha hauwi “vuguvugu”. Timiza agenda, liishi kusudi, na ukifa nenda ukapate thawabu yako kwa mujibu wa mfumo uliouchagua.

## SURA YA 10

# MAISHA YA NDEGE NA MAUA

---

Katika ufafanuzi wa mizunguko na mifumo ya maisha ya mwanadamu wa asili na feki, vifungu vyote vya biblia vinataja mimea na ndege. Kwenye Luka tunaona kuna kunguru na maua. Kwenye Yeremia kuna mti. Kuna nini tunaweza kujifunza kutoka kwenye maisha ya miti na ndege ambacho tunaweza kutumia sisi wanadamu ili tuweze kufanikiwa. Kimsingi Yesu aliwaambia wanafunzi wake wajifunze kutoka kwa kunguru na maua, jinsi vinavyoishi na kisha wajilinganishe wao ikiwa hastahili kuwa bora kuliko hivyo.

Mambo ya msingi tunayopaswa kujua kutoka kwenye maisha ya ndege na mimea;

- *Havitegemeani*

Umewahi kuona mti na mti vinalaumiana, vinaombana pesa na kukopeshana. Mti unakwazwa na mwingine, mmoja umeumizwa na mwingine. Umewahi kuona mti mmoja umeshindwa maisha umeenda kubebesha mti mwingine mzigo ambayo wenyewe umeshindwa kubeba. Kwamba mti ni mpweke, una wa mawazo. Au umewahi kuona chochote katika hayo kinatokea kwa ndege. Kwamba ndege mmoja ameenda kumshitaki mwingine kwa kumuumiza, kumzulumu, kumtapeli, kumnyima kitu fulani. Kwamba ndege huyu hakunipenda alinichezea, amenisaliti, amenizalisha na kuniacha, hajanipa hiki ama kile.

Kwa kiwango fulani huwa kuna namna miti na ndege vinasaidiana na kuwezeshana lakini havitegemeani. Hakuna kimoja kinachogombana na kingine kwa kushindwa kufanya jambo fulani. Hana ugomvi, vita, migogoro, chuki, hasira, uchungu Havina wivu, ubinafsi, ugomvi. Hawana vikao vya kulaumiana na kutuhumiana. Na hakuna mmoja ambaye maisha yake yanaathiriwa na udhaifu wa mwingine. Kimoja kikifa wengine wanaendelea na maisha. Hawana mfumo waliotengenezewa unaowalazimu kutegemeana kwa namna yoyote. Na kiini cha furaha, amani na mafanikio yao kipo hapa. Ni kutokana na kutokuwepo mfumo huo inakuwa ni rahisi sana Mungu kuvilisha na kuvivika.

- *Kila kimoja kimebaki kwenye mfumo unaovitegemeza*

Umewahi kuona mti umehama kutoka pale ulipopandwa. Mti uking'olewa ardhini unanyauka na unakufa. Chakula chake na matunda yake chanzo ni ardhi. Maji na chakula vinapatikana huko. Mafanikio yake yanapatikana huko. Na hivyo hakuna mti unaoweza kutoka kwenye chanzo chake cha maisha kwenda kugombana na mti mwingine maana inajulikana kuwa huko utakufa. Ndege nao kila wakati wapo hewani. Watatua kwenye matawi ya miti lakini wanajua kuwa hewani ndipo wapatapo chakula na kila wanachohitaji. Ukimnyima hewa anakufa. Hakuna kiwango cha ugumu wa maisha unaweza kushawishi mti utoke ardhini. Hata kama kuna ukame basi mti utangoja majira ya mvua ili uweze kuchanua tena. Haulamu mti mwingine.

Ndege hawana mfumo wanaotegemea kupata chakula na wala hawategemeani. Miti pia haina mifumo inayotegemea ili kupata chakula na kuvikwa na wala haitegemeani. Ni

kwa sababu hiyo inakuwa rahisi Mungu kuwatengenezea mfumo wa wao kula na kuwa hai. Shetani anajua namna bora ya kumnyausha mwanadamu na kumfanya aishi maisha ya shida ni kwa kumuondoa kwenye chanzo chake cha maisha yaani Mungu. Kumtenga mwanadamu na Mungu haina tofauti na kung'oa mti kutoka kwenye ardhi. Ni hakika utakufa. Unakumbuka kauli Mungu aliyomwambia Adamu kuhusu kula matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya? Alisema hivi;

*"siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika" (MWANZO 2:17)*

Neno "hakika" lilionyesha wazi kuwa Mungu alijua kuwa hakuna namna mtu anaweza kuwa salama nje ya uwepo wake. Atakuwa kama mti uliong'olewa kutoka katika ardhi. Hauhitaji ubobezi kujua kuwa utakufa. Wanadamu tunajua kuwa uking'oa mti, utakufa; ukimnyima ndege hewa, anakufa ila hatujui kuwa ukimtoa mtu kwenye uwepo wa Mungu anakufa pia. Kifo chake kinakuja taratibu sana ila kinaanza siku alipong'olewa.

Mti ukiung'oa hufa ghafla? Hapana. Huanza kwa kunyauka taratibu na huchukua siku na hata miezi kufa kabisa. Wakati fulani unaweza ukadhani kuwa umekufa lakini ukiuchukua ukaupanda tena aridhini huchipua. Hii ni kusema kuwa, mtu anapotolewa katika mfumo wa kumtegemea Mungu, kifo chake hakiji ghafla ila safari ya kifo huanza rasmi. Na dalili ya kuwa mtu anakufa taratibu ndio zile dalili za moyo mgumu. Karudi kuzisoma tena na kisha utambue kuwa ndio mti hunavyonyauka. Unaweza kuendelea kujitia moyo kuwa upo hai lakini taratibu uhai unapotea. Mara ghafla zile dalili zinakomaa mtu anafikia kuwa na mgonjwa ya ajabu ajabu, halali, kisukari, vidonda

vya tumbo, kansa; huo wote ni mnyauko unaendelea kumpata mtu. Katikati ya mnyauko mtu anapata msukumo wa kuwa na tabia za kujimaliza kabisa akiamini kuwa akifanya hivyo atapata nafuu. Ana msongo wa mawazo, anaamua kuwa mlevi, anaamua kuwa mzinzi, anaamua kuwa na tabia za hovyo kabisa. Asichokijua ni kuwa anachochea mchakato wa kufa mapema.

Angalia shetani anachofanya ni kimoja tu baada ya hapo vingine vyote sio shetani bali ni uharibifu tu wa asili ambao ni matokeo ya kile alichofanya shetani. Mti uking'olewa hatuhitaji kufanya chochote cha ziada kuukausha, asili itachukua mkondo wake na haijalishi mti utajitahidi vipi kupigania uhai wake, mwisho wa siku utanyauka tu. Ndivyo ilivyo kwa mwanadamu ambaye anaishi kwa kutegemea mfumo wa dunia hii na kuwatumainia wanadamu na moyoni mwake amemuacha Mungu. Atakemea pepo, atavunja laana, atakwenda kanisani, atafunga na kuomba lakini hivyo vyote havitamsaidia ikiwa hajarudi kujiunganisha na chanzo chake kinachomtegemeza. Atakuwa na bidii sana kwenye kazi zake, atafaulu vizuri masomo yake lakini kama hatojua namna mifumo hii inavyofanya kazi na kuishi katika kanuni hizo atanyauka tu. Mnyauko utampata maana anaishi kwenye ukame na njaa, mema yakija hataona, atakuwa kama mtu aliye jangwani kwenye ukame wa mvua nan chi ya chumvi isiyokaliwa na mtu. Ni muhimu kabla ya jitihada zote, utafute kwanza ufalme wa Mungu. Ukiupata, yale unayoyatafuta yatakuwa ni nyongeza maana aliyekuumba anajua kuwa unayahitaji hayo.

## SURA YA 11

# JUKUMU LA MWANADAMU

Mwanadamu hapaswi kumtegemea mwanadamu mwenzake. Hakuna mwanadamu aliyeumbwa kubeba mahitaji ya mwingine. Hakuna mwenye uwezo wa kutatua changamoto ambazo muhusika ameshindwa kuzitatua. Kama ilivyo kwa mti na ndege vivyo hivyo ilipaswa kuwa kwa kila mwanadamu. Jambo likimshinda anapaswa abaki kwenye ardhi yake(Mungu) na kusubiri majira ya kufanikiwa kwake. Hapaswi kutafuta mzazi, mlezi, uongozi, mume, mke, mtoto, rafiki, mchungaji wa kumsaidia. Kila mmoja alipaswa kutegemea kwa Mungu wake kwa kila kitu maana Mungu ana kila kitu na ni suluhisho la kila tatizo la mtu. Yeye Mungu ndiye anayejua namna ya kutuvisha na kutulisha hata kutufanikisha kwenye kila kitu.

Tunapaswa kuhusiana lakini hatupaswi kutumia mahusiano kama sehemu ya kutatua matatizo yaliyotushinda. Tusiwabebeshe tunaohusiana nao mahitaji yetu.

Tunapaswa kufanya kazi ila hatupaswi kutumia kazi hizo kama chanzo cha mapato ya kuendesha maisha yetu. Tusibebeshe mashirika, makampuni, serikali mizigo ambayo sisi tumeshindwa.

Tunapaswa tumtumikie Mungu ila hatupaswi kutumia utumishi wetu kama chanzo cha kuendesha maisha yetu.

Tusiwabebeshe washirika na wafuasi wetu mzigo wa mahitaji yetu ya kiuchumi.

Tunapaswa tufanye biashara ila biashara sio chanzo cha mafanikio yetu. Tusiwabebe wateja mizigo ambayo sisi tumeishindwa.

Tunapaswa kuoa na kuolewa ila mume hapaswi kumtumia mke kutatua changamoto na mahitaji yake na mke hapaswi kumtumia mume kubeba mizigo iliyomshinda.

Tunapaswa kuzaa watoto lakini hatupaswi kuwatumia watoto kutatua shida zetu za kihisia na kiuchumi.

Chochote tunachofanya wanadamu lazima tujue kuwa hatupaswi kutumia wanadamu wenzetu kubeba mizigo yetu. Huna mamlaka ya asili kumtumia mtu yoyote kutatua shida yako yoyote ila Mungu anaweza kumtumia mtu au mazingira yoyote kutatua shida na changamoto yako. Kama ambavyo Mungu ameweza kumtumia ndege kumfaa ndege mwingine, anavyotumia kivuli cha miti kuwafaa ndege na kuwaacha kujenga viota vyao, anavyotumia mti kuotesha miti mingine vivyo hivyo ilipaswa kuwa kwa mwanadamu. Ni Mungu atumie watu, kazi yako, biashara yako, bosi wako, serikali yako, mke wako, mume wako, mtoto wako, mchungaji wako; kuyabariki maisha yako na sio wewe uanze kudai kutoka kwa hao yaani kuhudumiwa nao.

Jukumu la mwanadamu ni kuwapenda watu na kuliishi kusudi la Mungu. Mungu ataamua amtumie nani, wakati gani, kwa nini na kwa jinsi gani ili kufanikisha kusudi lake kwenye maisha ya mtu husika.

Tunapoanza kuwa na madai ya kufanyiwa vitu na wanadamu ina maana tumeanza kuwategemea wao na kuacha kumtegemea Mungu.

- Tunapoanza kutegemea kazi zetu, tunaacha kumtegemea Mungu.
- Tunapoanza kutegemea biashara zetu, tunaacha kumtegemea Mungu.
- Tunapoanza kutegemea viongozi wetu, tunaacha kumtegemea Mungu.
- Tunapoanza kutegemea wafuasi wetu makanisani, tunaacha kumtegemea Mungu.
- Tunapoanza kutegemea watoto wetu, tunaacha kumtegemea Mungu.
- Tunapoanza kutegemea wenzi wetu, mke au mume, tunaacha kumtegemea Mungu.
- Tunapoanza kutegemea taaluma zetu, tunaacha kumtegemea Mungu.

Hao wote hapo juu ni aidha wanadamu ama mfumo wa dunia. Na utegemezi huo unatuweka kwenye hatari ya kuanza kugombana nao, kuchukizwa nao, kukwazana nao, kujeruhiwa nao, kuteswa na kunyanyaswa nao. Maisha yetu yanaweza kutawaliwa na wao, kuvurugwa na wao.

Hatupaswi kuwategemea watu ama kutegemea mifumo ya dunia hii kihisia, kifikra ama kiuchumi ijapokuwa tunafanya kazi katika hiyo, tunaishi kwa hiyo na tunahusiana na hao. Kuhusiana nao, kufanya kazi kwayo haipaswi kutufanya maisha yetu kuwategemea wao. Sisi tupo humo sio kwa kuwa tunataka kutimiziwa mahitaji

yetu bali kwa kuwa lipo kusudi la Mungu kwenye maisha yetu ambalo tunapaswa kulitimiza tuwapo hapa duniani.

Tunafanya kazi, biashara, huduma, tunaoa na kuolewa, tunazaa sio kwa ajili yetu bali kwa ajili ya makusudi ya Mungu. Tunapoenda kazini na katika shughuli zetu kila siku asubuhi, fikra zetu lazima zijue kuwa hatupo pale kwa ajili ya hela bali makusudi fulani ya Mungu, pesa ni nyongeza. Tunapokuwa wachungaji na viongozi wa dini, tunajua shida yetu sio pesa wala heshima bali kuna kusudi la Mungu, heshima na pesa ni nyongeza. Tunapokuwa viongozi wa taasisi, mashirika, serikali twajua kuwa shida yetu sio utajiri, heshima, hadhi bali kuna kusudi la Mungu, vingine ni nyongeza. Unapokuwa mke au mume, unajua kuwa lengo sio kupata suluhu ya matatizo yako ya kihisia na kiuchumi bali lipo kusudi la Mungu, vingine ni nyongeza.

Migogoro ya mahusiano, ndoa, kazini, biashara, makampuni, mashirika, serikali hata kwenye makanisa kiini chake ni watu kupambania mahitaji yao na kusahau suala la kusudi la Mungu. Kile ambacho tulipaswa tupewe kama nyongeza na Mungu baada ya kuupata ufalme wake sisi ndio tunakipa kipaumbele na tumeamua kutumia nguvu zetu kukipata. Tumeingilia jukumu la Mungu, tumeacha jukumu letu. Tupo na harakati za kutafuta hela, mavazi, chakula, malazi, usafiri, mke, mume, watoto ili kutibu mahitaji yetu badala ya kuishi katika kusudi la Mungu ili Mungu atupatie mahitaji yetu.

- ❖ Sasa ndoa ambayo mke na mume walioana kwa misingi ya shida na mahitaji binafsi tunatarajia vipi isiwe na migogoro?

- ❖ Kanisa ambalo mtumishi alianzisha kwa misingi ya maisha magumu akaamua kuingia kwenye utumishi tunatarajia vipi liponye watu?

- ❖ Ajira ambayo mtu aliipata kwa misingi ya shida ya hela, tunatarajia vipi asiibe akipata mpenyo?

- ❖ Uongozi ambao mtu kaupata kwa misingi ya kutafuta hela, sifa, heshima, hadhi; tunatarajia vipi asiumize watu kwa ufisadi, wizi na rushwa?

- ❖ Biashara ambayo mtu kaanzisha kwa misingi ya njaa na shida, tunatarajia vipi ikue wakati kila akipata faida anawaza kuila?

Tukiacha kutafuta nani tumtumie kufanikisha mambo yetu hapa duniani na kuanza kuongeza Imani yetu kwa Mungu tutakuwa tumepiga hatua moja kubwa na ya msingi kuondokana na moyo mgumu. Futa watu wote kichwani mwako unapokuwa na changamoto ya kutatua na anza kumtafuta Mungu. Futa mumeo, futa mkeo, futa bosi wako, futa wazazi wako, futa marafiki, futa serikali, futa mchungaji wako, futa watoto wako; futa benki, futa taasisi fulani, futa watu wote. Pale unapokuwa na changamoto, shida ama uhitaji. Unapokuwa na mradi fulani, mipango fulani, maono fulani; hakikisha hakuna jina la mtu ama mfumo unaokuja kwanza kichwani bali Mungu kwanza.

“Futa, futa, futa”. Ondoa watu wote kichwani.

Muache Mungu awatumie watu hao kukutatulia changamoto hiyo akiona ni vyema. Muache Mungu amtumie mke, mumeo, serikali, taasisi, watu, mchungaji. Sio wewe uwatumie bali Mungu awatumie kuyabariki maisha yako. Ukianza wewe kuwatumia uwezekano ni kuwa utaishia kuwa mzigo kwao na baada ya muda watakuchoka na pengine wataanza kukukwepa maana hata wao wana mizigo yao. Hapa waweza kujua ni kwa nini wakati mwingine mume anaanza kumkwepa mke, mke kumkwepa mume, watoto kuwakwepa wazazi, viongozi kuwakwepa wafuasi, bosi kuwakwepa wafanyakazi, ni dalili kuwa wameanza kuchoshwa na mizigo unayowatwisha.

Tukifikia hapa basi tujue kuwa;

- Sio lazima tulionao watufanyie wema tunaotarajia. Tunajua kuwa uwepo wetu kwenye maisha yao na taasisi hiyo ni kwa makusudi ya Mungu na sio kwamba tunataka kupata chochote kutoka kwa hao.
- Sio lazima furaha yako itoke kwa mumeo ama mkeo bali Mungu anaweza kuileta kwako kutokea sehemu nyingine kabisa ila wewe timiza wajibu wako wa ndoa.
- Sio lazima pesa yako itoke katika kazi na biashara hiyo pekee bali Mungu anaweza kuitumia hiyo ama akatumia mlango mwingine kubariki maisha yako bali wewe timiza vyema wajibu wako.
- Sio lazima elimu uliyosomea ndio ikupe ajira na mafanikio ya kiuchumi bali Mungu anaweza kuleta mafanikio yako kwa mlango na taaluma tofauti.
- Sio lazima kipawa hicho ulichonacho, ujuzi huo, uzoefu huo, kanisa hilo, nchi hiyo uliyopo ndio iwe chanzo cha mafanikio yako, wewe ni zaidi ya hicho

unachokiamini. Mpe Mungu nafasi ya kukufanikisha nje ya mifumo na watu uliowazoea.

## WAJIBU WA MKE NA MUME

Biblia ipo wazi sana kuhusu wajibu wa mke na mume kwenye ndoa. Mume ni kichwa na mke ni msaidizi. Swali ni;
Je! Mume anapata wapi rasilimali za kumuongoza mke, na mke anapata wapi rasilimali za kumsaidia mume?

Ikiwa mke atamtegemea mume kihisia, kifikra na kiuchumi badala ya kumtegemea Mungu basi hapo hatakuwa msaidizi bali mzigo kwa mwanaume. Rasilimali za kumsaidia mume wake, mke anapaswa kuzitoa kwa Mungu aliyempa jukumu na wajibu wa kuwa msaidizi. Hapa tunajua kuwa mwanamke hapaswi kumlaumu Mungu kwa namna yoyote ile anaposhindwa kumsaidia mumewe.
Kila hekima, maarifa, amani, furaha, pesa na mitazamo anayohitaji ili kumsaidia mumewe anavyo Mungu. Alishaandaa vyote kabla hajampa jukumu hilo na hivyo kushindwa kwake ni matokeo ya kutomtegemea Mungu. Akisema hajui amsaidiaje ni kwa sababu ameshindwa kupata rasilimali hizo. Kukosa rasilimali ndiko kunakomfanya ashindwe jukumu na sio kwamba tatizo ni mume. Kama kweli mume kashindikana basi anayetakiwa kutoa hitimisho la hilo ni Mungu, hivyo bado anawajibu wa kuendelea kumuhusisha Mungu kuhusu suala la jukumu la kumsaidia mumewe.

Ikiwa naye mume atakuwa kichwa kwa mkewe kwa kutumia rasilimali kutoka kwa mke anatengeneza tatizo

ambalo halikupaswa kuwepo. Hapaswi kumtegemea mke wake kifikra, kihisia wala kiuchumi.
Kwamba mwanaume anatafuta mwanamke ambaye yupo vizuri kiuchumi ndio amuoe ni wazi kabisa mwanaume huyu anajitafutia laana ya kimfumo.

- Kwamba mke ndo ampe mawazo ya jinsi ya kuendesha maisha.
- Kwamba hawezi kumudu hisia zake za kingono sasa anaona aoe ili mke amsaidie.
- Kwamba mke amekuwa ndio chanzo cha rasilimali anazozihitaji ili awe mume bora.
- Kwamba ubora wake wa jukumu la kuwa mume unategemea mwanamke.
- Kwamba alichepuka kwa sababu mkewe hamtii, hampi kile wala hamfanyii vile.
- Hatulii kwa kuwa kuna migogoro kati yake na mkewe.
- Kwamba mke ndio anaamua hatima ya mumewe.

Je! Hivi ndivyo unaweza kusimama mbele za Mungu na kusema Kwamba nilifeli maisha yangu kwa sababu ya ugumu wa moyo wa mke wangu?

Kama biblia imeagiza “mke kumtii mume” na “mume kumpenda mke”, wajibu huu haupaswi kutekelezwa kwa kumtegemea mwingine. Mume hapaswi kusema simpendi mke wangu kwa sababu hanitii, mke hapaswi kusema simtii mume wangu kwa sababu hanipendi.
Huo ni wajibu ambao kila mmoja anapaswa kupata rasilimali zake kwa Mungu ili kuutimiza. Mume na aombe neema ya kumpenda mke asiyetii, na mke na aombe neema ya kumtii mume asiyempenda. Na Mungu ndiye atakuwa hakimu wa kila mmoja.

Itoshe tu kusema kuwa mke hatakiwi kumtegemea mume kwenye kutimiza wajibu na majukumu yake aliyoagizwa na Mungu, na mume vivyo hivyo. Tusitegeane na kutegemeana, kila mmoja abaki kwenye chanzo chake cha rasilimali.

## SURA YA 12

# TABIA ZINAZOATHIRIWA

---

Moyo mgumu haumuachi mtu salama kwenye tabia na nidhamu za kiroho. Kuna madhara ya moja kwa moja anayopata mtu pindi anapokuwa na moyo mgumu na yanaathari kubwa sana jinsi mtu anavyoenenda katika masuala ya kiroho. Mtu anayemtegemea Mungu huwa na tabia tofauti sana na yule asiyemtegemea Mungu. Kuna namna wanatofautiana sana katika habari ya kujitoa na kumtolea Mungu.

***WARUMI 12:1-2***..*"Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, ITOENI MIILI YENU iwe DHABIHU ILIYO HAI, TAKATIFU, YA KUMPENDEZA MUNGU, ndiyo IBADA yenu yenye maana. Wala msiifuatishe NAMNA YA DUNIA HII; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu."*

Ibada yenye maana ambayo mtu anaweza kumfanyia Mungu ni kuuacha mwili wake utumike kwa ajili ya kutimiza makusudi ya Mungu hapa duniani. Sasa mtu anapotumia mwili wake kupambania mahitaji yake ya mwili ameondoa ibada yenye maana na ibada zingine zote anazofanya, ikiwa ni kuhudhuria kanisani, kusifu na kuabudu, kufunga na kuomba, kukesha, kusoma neno; vinakosa umaana. Kujitoa mwili wake dhabihu iliyo hai

inapaswa kuwa ni msingi wa ibada zingine zote. Zote zinapata umaana ikiwa amefanikiwa kutimiza ibada hii. Tumekuwa na watu ambao wanafanya ibada nyingi ila wamekwepa "ibada yenye maana". Ni kweli wapo kanisani, maombi na kufunga, wanatoa sadaka kubwa lakini kila wanachokifanya duniani ni kwa ajili yao sio kwa ajili ya kusudi la Mungu.

Kazi ni zao, ajira ni zao, biashara ni zao, ndoa ni yao, watoto ni wao, uongozi ni wao, huduma ni yao, pesa ni yao, kila kitu ni chao na hakuna nafasi ya kusudi la Mungu katika hivyo anavyovifanya. Akiamka asubuhi anakwenda kwenye kazi yake na huko wala hana fikra kuhusu kusudi la Mungu, biashara yake haina nafasi ya kusudi la Mungu, ndoa yake haina nafasi ya kusudi la Mungu, kanisa "lake" halina nafasi ya kusudi ya Mungu. Muda wake, pesa zake, afya yake na kila kitu chake hakitoi nafasi ya kusudi la Mungu.

Mtu wa namna hii anawekwa kwenye kundi la "watu wanaofatisha namna ya dunia hii" (mfumo wa dunia wa kuishi) na hajageuzwa nia yake hata kama hakosi kusanyiko hata moja la kanisani siku saba za wiki. Kibinadamu anaonekana ni mwenye bidii sana na ibada lakini "moyoni mwake amemuacha Mungu". Yupo ibadani lakini anategemea mifumo ya dunia na wanadamu kwenye kuishi maisha yake na hivyo inamfanya ashindwe kuutoa mwili wake dhabihu maana ameutoa kupambania mahitaji yake ili asife na njaa na kiu.

Mtu wa jinsi hii kuna shida ambazo ataanza kukutana nazo;

1. *Tabia ya kushindwa kumtolea Mungu kwa furaha.*

Mungu hakukusudia watu wamtolee Mungu wakiugua mioyo. Hata hivyo sadaka ni rasilimali ambazo Mungu huzitoa kwa watu fulani na kuzipeleka kwa wengine kwa makusudi ya kujenga ufalme wake hapa duniani. Ni muhimu kujua kuwa japokuwa fedha na mali ni mali ya Bwana lakini ni mali yake kwa kuwa yeye anamiliki mbingu na nchi na sio kwa kuwa yeye anazitengeneza hela. Hela zinatengenezwa kwenye mifumo ya duniani. Hivyo Mungu kama ambavyo hutumia rasilimali nyingine nyingi zilizopo duniani, hukusanya rasilimali hizo kwa kutumia watu fulani na kuzipeleka kufanya kazi kwenye mfumo wake ili kupeleka mbele ajenda yake hapa duniani. Hivyo sadaka ni jambo muhimu sana. Atambariki mmoja ili kumbariki mwingine.

Kanuni inabaki vile vile kuwa hapaswi mmoja kuchukua rasilimali kwa mwingine bali Mungu huweza kumtumia mmoja kumpelekea mwingine rasilimali. Mwenye pesa anapaswa kuwa na “moyo wa kumtolea Mungu kwa furaha” akijua kwamba hamtolei mwanadamu bali anamtolea Mungu. Yule anayepokea naye anapaswa kujua pesa ile sio kwa ajili ya shida na mahitaji yake bali kuna makusudi ya Mungu.

Ili mtu aweze kutoa kwa moyo wa furaha lazima pesa na mali alizonazo ziwe zimetokana na mfumo wa Mungu wa kumbariki na sio awe katumia jasho, nguvu na maumivu mengi. Kumbuka kuwa mtu anapoamua kuutoa mwili wake kupambania mahitaji yake, pesa yote anayopata inakuwa ni yake na hakuna suala la Baraka ya Mungu.

Hawezi kubarikiwa nje ya mfumo halisi wa maisha. Kama anatumia mfumo feki nguvu zake na akili zake ndio zimempa pesa hiyo na ni maalumu kwa ajili ya mahitaji yake. Pesa hiyo aliyopata kwa maumivu na nguvu zake na wala hakuona Baraka za Mungu lazima atapata ugumu kwenye kuitoa sadaka. Ndio maana tumekuwa na watu ambao wanapingana na suala la fungu la kumi bila kujua kuwa hiyo ni sadaka kama sadaka zingine tu na kama utafanikishwa na Mungu ni rahisi kutoa fungu la hamsini na wala hutakuwa na shida. Ugomvi kuhusu sadaka ni dalili ya ugumu wa mioyo ya watu na tukitaka ugomvi huo uishe lazima watu waondokane na moyo mgumu. Wakiwa na moyo mgumu hakuna kiwango cha maombi na mafundisho kinachoweza kuchochea utoaji na hata wakitoa wataumia mioyo na Mungu hatokuwa na radhi na sadaka hizo.

***MITHALI 10:22***..*"Baraka ya Bwana hutajirisha, wala hachanganyi huzuni nayo"*

Palipo na Baraka za Mungu hakuna huzuni. Hakuna kuona uchungu, hakuna uchoyo, hakuna kujizuia kutoa, hakuna kujisikia vibaya kutoa ama kuona kuna mtu unamtajirisha. Pale ambapo watu wanapata shida sana kumtolea Mungu ni dalili kuwa pesa zao ni matokeo ya bidii na juhudi zao na hawaoni kuwa Mungu amehusika kwa namna yoyote kuwapatia walivyonavyo. Wanaumia kuona jasho lao linaliwa. Unawaambia wakitoa watabarikiwa na wanashangaa kwa nini Mungu hakuwabariki ili watoe bali anasubiri waumie kuzitafuta halafu waje watoe ndo awabariki. Kwamba Mungu anavuna asipopanda. Kama Mungu anaona ni muhimu

wao kutoa na anazihitaji pesa kwa nini hakuwawezesha ili wamtolee alichoshiriki kwenye mchakato wa kupata.

Utata wa dhana nzima ya kutoa ili ubarikiwe unaanzia hapa. Kwamba watu wamepata pesa kwa jasho na huzuni nyingi na hivyo inawaletea ugumu kwao ukiwambia kuwa hizo ni matokeo ya Baraka za Mungu. Baraka za Mungu zinapaswa kuwa dhahiri sana kwa mtu. Kwamba apate pesa ambazo haoni kuwa amestahili au kuzifanyia kazi kubwa. Hii sio kusema mtu asifanye kazi bali apate pesa zaidi ya kazi aliyofanya. Aone urahisi wa kuzipata hizo pesa na aone kuna fursa na milango mingine ambayo sio akili na nguvu zake zimemfanya apate bali kuna kitu cha ziada. Ikiwa ni kazini, biashara ama huduma, lazima kuwe na namna ambayo kazi yake inakuwa nyepesi na anapata pesa halali kwa namna ambayo moyoni mwake anakiri kuwa huyu ni Mungu sio uwezo na nguvu zake. Ikifikia hapo mtu huyu hawezi kuwa na ugomvi na suala la kumtolea Mungu maana anajua hata alizonazo hakustahili. Na ikiwa Mungu alifanya jana basi anaweza kufanya zaidi kesho na sio kwa sababu ya bidii zake bali kibali na neema ya Mungu. Akiweza kutenganisha baraka za Mungu na bidii yake basi hapo ataona umuhimu wa kumtolea Mungu. Baraka za Mungu zinaanza kwa kutegemea mfumo wa Mungu wa kuwafanikisha watu na ili kuutegemea lazima mtu apone dhidi ya moyo mgumu. Kwa kutumainia mfumo wa dunia kufanikiwa, suala la utoaji litakuwa gumu na akifanya basi hatokuwa na furaha.

1. Tabia ya Kushindwa kuomba

Unawezaje kumuomba usiyemtegemea? Maombi ni ishara ya unyenyekevu. Msingi wake huanzia kwenye fikra kuwa

"nakutegemea wewe na siwezi bila wewe"

Kabla hujamuomba mtu lazima kwanza ukwame. Huwezi kuomba msaada ikiwa unamudu jambo hilo mwenyewe au una mtu mwingine unayemtegemea ama huna Imani kuwa yule unayetaka kumuomba atatatua changamoto yako. Sasa kama maisha ya mtu yana watu ama mifumo inayoitegemea, sababu ya kumuomba Mungu zinatoka wapi? Mbona ni rahisi sana kuomba wale ambao anawategemea kuliko kumuomba Mungu asiye mtegemea.

Mara nyingi tunatamani tabia ya maombi iwe kama desturi lakini ukweli ni kuwa watu wengi hawamtegemei Mungu, hivyo sio rahisi kuwa na desturi hiyo. Akiangalia pembeni ana mke au mume anayemtegemea, baba au mama anayemtegemea, muajiri wake, ndugu zake, rafiki zake, taasisi fulani, kiongozi fulani na nyakati hizi watu wanategemea hadi viongozi wa dini na pengine vifaa vya upako alivyopewa na kiongozi wake wa Imani. Aombe Mungu ili iweje wakati ana vitu na watu wengi ambao anaamini wanaweza kutatua changamoto zake.

Kwa kawaida Mungu akitaka kumfanya mwanadamu amtegemee Yeye huwa anaondoa kila anachokitegemea ili akiwa hana tegemeo alazimike kumtegemea Mungu. Sasa unapoona unatengenezewa mazingira ama unajitengenezea mazingira ya vitu na watu wengi unaowategemea basi tambua kuwa huo ni mtego kinyume na mpango wa Mungu hata kama umeletwa kwa jina la Mungu. Inaweza isionekana kuwa na athari kwako lakini

vitu hivyo vinaondoa kabisa utegemezi wako kwa Mungu na kuua Imani yako.

***ZABURI 20:7****…"Hawa wanataja magari na hawa farasi, Bali sisi tutalitaja jina la BWANA, Mungu wetu"*

Wanaomtegemea Mungu hudumu katika kumtumaini na kumuomba bila kujali wana nini cha kutegemea. Ukiri wa muandishi wa Zaburi unatuonyesha wazi kuwa ushindi na mafanikio yetu hautegemei wingi wa rasilimali tulizonazo bali Mungu. Hii haimaanishi tusiwe na rasilimali, ikiwa ni fedha, watu ama chochote lakini hatupaswi kuvitaja hivyo kama chanzo cha kufanikiwa kwetu. Hivyo vyote havipaswi kuathiri Imani yetu kwa Mungu.

Hii ina maana kuwa mtego mkubwa ni pale vitu na watu tulionao wanapotufanya tumuondoe Mungu katika maisha yetu. Tunapaswa kuwa na kila kitu na tumtegemee Mungu. Hii inawezekana kama tu mtu akipona dhidi ya moyo mgumu.